

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 3 Juni, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha Arobaini na Tatu. Katibu

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

#### HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, aah sasa hivi unavaa sketi ndefu, hataki ugomvi na Mgogo. (*Kicheko*)

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha tena kuhusu maswali ya kisera sio matukio, sio nini, ni ya kisera. Tunaanza na Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, maswali kwa kifupi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kwanza kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, swali langu litahusu sekta ya korosho. Mwaka huu tumepata taarifa kwamba Serikali ilijipanga kutupatia pembejeo wakulima wa zao la korosho kwa maana kwamba waje kuzilipa baadaye kwenye mjengeko wa bei. Hata hivyo, kuna taharuki kubwa kwa wakulima wetu wa korosho baada ya Bodi ya Korosho kuleta waraka kwenye Halmashauri zetu, wakiwaambia kila mkulima akipeleka zao lile kwenye mnada kila kilo moja itakatwa shilingi 110 bila kujali kwamba mkulima yule amechukua pembejeo kwa kiwango gani. Barua ile inasema kwamba jambo hili hata sisi Wabunge tumeliridhia.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna taharuki kubwa sana kiasi kwamba mpaka...

**SPIKA:** Swali lako ni nini katika jambo hilo?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na mkanganyiko huu ni nini kauli ya Serikali ili wakulima wetu waendelee kuchukua zile pembejeo maana sasa hivi wanaziogopa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara yetu ya Kilimo imetoa miongozo kadhaa ya kuboresha masoko ya mazao nchini ili kuwanufaisha wakulima kwenye mazao wanayoyalima ikiwemo na kuwarahisishia namna nzuri ya kupata pembejeo. Zao la korosho ni mionganoni mwa mazao ambayo Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeendelea kufanya mapitio ya maboresho ya namna nzuri ambayo wakulima ambao kwa sasa ndiyo wapo kwenye msimu wa kutumia pembejeo ili waweze kupata pembejeo wakulima wote na waweze kushiriki vizuri kwenye kilimo hiki.

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba ipo tataruki kwa sababu na mimi ni mdau pia wa zao hilo lakini tataruki hii imetokana na vikao vya awali vya majadiliano ya mfumo mzuri ambao pia wakulima nao wanaweza kushiriki vizuri kupata pembejeo. Si kwamba Wabunge wameshiriki katika kutoa maamuzi, hapana, bali Wizara inaendelea kuwa na vikao vya mara kwa mara ili kufikia hatua nzuri ya kuwezesha kila mkulima kupata pembejeo. Vikao hivi bado havijakamilika na kikao kikubwa kabisa kipo tarehe 6 ambacho kinaalika wakulima, viongozi wa ushirika, viongozi wa Serikali na Waheshimiwa Wabunge pia mtaalikwa ambacho sasa tutajadili namna nzuri ya kumwezesha mkulima kupata pembejeo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya awali ya kwamba kila mkulima atakatwa shilingi 110 yamesitishwa kwa muda ila wakulima wote waende kupata pembejeo zile ambazo zimepelekwa kwenye maeneo yale. Kiwango cha pembejeo kilichoagizwa kinatosha kabisa kwa kila mkulima kutokana na takwimu zilizopatikana kutoka vyama vyetu vya ushirika ili kila mkulima apate pembejeo ya kutosha kupuliza awamu zote nne kufikia kipindi cha uzalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kikao kile cha tarehe 6 ndicho kitakachotoa mwelekeo mzuri wa nini kitafanyika kwa

pembejeo ambazo zimetolewa na wala haitakuwa kumkata kila mkulima kwa kilo alioipeleka sokoni kwa sababu wapo wengine wana kilo mbili, wengine kilo 10 lakini wapo wamezalisha zaidi ya tani 20, sasa huwezi kukata kwa kila kilo. Kwa hiyo, hilo linafanyiwa kazi na Wizara na ufanuzi utatolewa siku ya tarehe 6 ambapo wadau wa zao la korosho kila mmoja atashiriki kwenye eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwasih i wakulima wa zao la korosho waendelee kupokea pembejeo zile. Serikali inaendelea kuangalia namna bora ya kumfanya mkulima aweze kupata pembejeo kwa gharama nafuu ili aweze kuendelea kulima zao hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka niongezee eneo lingine ambalo pia limeleta mkanganyiko kwamba mabenki ambayo miaka yote yamekuwa yakitoa mikopo kwa wakulima, mwaka huu walismama kutoa mikopo yao kwa hofu kwamba wakulima watakapopata pembejeo huku Serikalini hawataweza kulipa gharama ya mikopo ambayo wameikopa kwenye mabenki. Tumeruhusu mabenki yaendelee kukopesha wakulima kwa sababu bado kwenye zao la korosho kuna shughuli nydingi za kufanya; pamoja na kupilizia dawa lakini pia kuna kupalilia, kuokota na kuhakikisha zao linakwenda sokoni, yote inahitaji mtaji ambapo mkulima ambaye amelima, anajiamini kwamba atakopa na kurejesha, bado mabenki yaendelee kukopesha. Tumeshawapa maelezo hayo mabenki na wanaendelea na kukopesha. Kwa hiyo, wakulima waende wakakope kulingana na mahitaji yake ili alihudumie zao na hatimaye aweze kurejesha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka kwenye majimbo yanayolima zao la korosho muendelee kuiamini Serikali na mifumo ambayo inaendelea kuipanga. Mifumo hii haiamuliwi tu moja kwa moja na Serikali bali inashirikisha wadau na kwa zao la korosho wadau tutakutana siku ya tarehe 6. Kwa hiyo, siku hiyo tutatoa mwelekeo wa zao hilo sote kwa Pamoja.

Kwa hiyo, wawe na amani na waendelee na uratibu wa zao hili la korosho, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, uliza swali lako kwa kifupi.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa mujibu wa kifungu cha 64(2)(c) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2016, sambamba na Tangazo la Serikali Na.30 la mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi (*procuring entity*) zitenge asilimia 30 ya zabuni zake kwa mwaka kwa ajili ya vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na ulegelege katika utekelezaji wa takwa hili ambalo linawanyima fursa vikundi hivi muhimu, je, ni mkakati gani sasa ambao Serikali unauweka kuhakikisha kwamba takwa hili la kisheria linazingatiwa ili kuweza kuwapa fursa hizi vikundi vya akina mama, vijana na watu wenye ulemavu? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mavunde, Mbunge wetu wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumeweka sheria inayowezesha kila taasisi kutenga kiwango cha fedha kwa ajili ya kukopesha makundi kama alivyoyataja Mheshimiwa Mbunge lakini tunatambua zipo changamoto kwa baadhi ya taasisi kutotekeleza sheria hiyo huku wakitakiwa kutekeleza sheria hiyo. Serikali inaendelea kusisitiza na kuhamasisha taasisi zetu kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na hasa kwenye eneo hili la mikopo kwa sababu tunahitaji sasa Watanzania wanaotaka kujishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi au masuala ya kijamii wapate uwezesho wa kumudu kutekeleza wajibu huo. Maelekezo

ambayo tunayo kwa sasa ni kuhakikisha kwamba kila mtumishi wa umma aliyepo kwenye kitengo ambacho kimetakiwa kutoa mikopo hii, lazima afanye hivyo kwa sababu tayari pia Serikali huwa inatenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali na wale wote ambao wanatakiwa kupewa mikopo hiyo ikiwemo wanawake, vijana na wale mavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, msisitizo wa Serikali kwa kila mmoja kujishughulisha na masuala ya kiuchumi ni msisitizo ambao unatokana na malengo yaliyowekwa na utekelezaji ambao upo kwa taasisi hizo. Kwa hiyo, bado nitoe wito kila taasisi ambayo imetenga fedha hizo na sheria inamtaka kutoa mikopo hiyo bado waendelee kutoa mikopo kwa wahitaji ili kila mkopaji aweze kupata fedha hizo na aweze kuendesha miradi yake kadiri alivyojipanga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachotaka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kusisitiza kuhakikisha kwamba kila mmoja anatekeleza sheria ili wanufaika waweze kunufaika kwa utaratibu ambao tumejiwekea. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala.

**MHE. IDDI S. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tunatambua kwamba Serikali yetu ilizua kabisa usafirishwaji wa makinikia nje ya nchi na kwa sasa tumeshuhudia makontena ya makinikia yakisafirishwa kuititia barabara ya Bulyanhulu – Kahama na Bandari yetu ya Dar es salaam hivyo kupelekeea taharuki kwa Watanzania na kwa wananchi wa Jimbo la Msalala. Nini sasa kauli ya Serikali juu ya jambo hili? Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nami nimeona pia kwenye mitandao watu wakionesha kwamba wanaona makontena ya makinikia yakisafirishwa kwenda nje. Nataka niwakumbushe Watanzania kwenye hili kwamba mwaka 2017/2018 tulizuia usafirishaji wa makinikia kwenda nje ya nchi kwa sababu yalikuwa hayajafuata utaratibu lakini pia kulikuwa na udanganyifu mkubwa. Tulipozuia makontena zaidi ya 300/400 yaliyokuwa bandarini yalikaa pale mpaka tulipoweka utaratibu. Utaratibu uliowekwa na Serikali kwanza kuwatambua ni nani wanasafirisha makinikia kwenda nje na ni nani wametoa vibali hivyo kwenda nje na tukazuia kabisa tukaanza utaratibu mpya.

Mheshimiwa Spika, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano alilisimamia na kwa kuunda timu iliyofanya uhakiki wa sekta yote ya madini ikiwemo na eneo hili la usafirishaji mchanga ambalo kwa kweli tulikuwa tunaibiwa kwa kiasi kikubwa. Ufumbuzi wa ile timu ni kuanzisha kampuni ya Watanzania kwa ushirikiano na makampuni ya nje yaliyopo hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo hii tunayo kampuni inaitwa *Twiga Minerals* ambayo ni ya Watanzania kwa maana ya Serikali ambayo imeingia ubia na hao wachimbaji wakubwa wa madini kwenye mgodi kama ule wa kwako Mheshimiwa Mbunge wa Bulyanhulu lakini wa pale Kahama Mjini Buzwagi na kule Tarime North Mara. Migodi hii mitatu chini ya Barrick tumetengeneza kampuni ya pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza wataalam baada ya kuchimba tunapitia kujua aina zote za madini. Mwanzo tuliambiwa madini yaliyopo pale ni ya aina moja tu dhahabu lakini kumbe kule ndani baada ya ukaguzi na uchunguzi wa wataalam tumegundua tuna aina tano za madini. Kwa hiyo, leo hii kupitia Kampuni yetu ya Serikali, inauza madini ya aina zote 5 siyo moja kama zamani. Mbili; tukishapata ule udongo na ukaguzi huo na kugundua aina zote, tunayaiza hapahaha ndani ya nchi, sio nje ya nchi. Makontena yote yanayosafirishwa tayari yameshauzwa, Serikali imeshapata fedha yake na fedha imeshahifadhiwa

kwenye akaunti zetu kwa hiyo Watanzania hatupati hasara. Hatua inayofuata mnunuzi anakuwa huru kuyapeleka anakotaka na ndio hayo ambayo yanaonekana kutoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Watanzania kuyaona makontena yakipita na hofu ya awali, nataka niwaondolee kuwa makontena hayo yameshauzwa tayari na huyo ni mnunuzi. Kwa hiyo, waondoe mashaka juu ya usafirishaji wa makontena hayo yenye makinikia kwa sababu Serikali iko makini sana. Inayo timu palepale kwenye mgodi ya kuhakiki lakini pia ya mauzo na kuhakikisha fedha inalipwa na hakuna kontena linatoka nchini bila kuuzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeweka timu pale bandarini kuhakikisha kwamba kila kontena la makinikia linaloingia pale lina nyaraka zote baada ya kufanya mauzo hukohuko kwenye mgodi, kwa hiyo, hakuna kontena linaabiwa. Kwa hiyo, Watanzania muondoe mashaka, Serikali ipo makini, watu wetu tulioaweka kwenye maeneo haya kuhakiki kuwepo kwa nyaraka zote za kuuza makinikia hayo zipo makini na kwa kweli tunaingiza fedha za kutosha; sina takwimu za kutosha lakini tuna fedha ya kutosha kwa sasa. Mheshimiwa Waziri wa Madini alipokuwa anawasilisha bajeti yake hapa alitoa ufanuzi na kuonesha namna ambavyo kwenye madini tumepata fedha kiasi kikubwa sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elibariki Kingu, uliza swali lako.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali langu; sasa hivi pamekuwa na utaratibu ambapo Serikali inapopeleka fedha za maendeleo kwenye Halmashauri hasa fedha zinazopelekwa kuanzia miezi ya Machi, Aprili na Mei, fedha hizi zinapokuwa hazijatumika zote pamekuwa na utaratibu

wa miaka mingi mwaka wa fedha unapoisha zinarudishwa hazina na hivyo kuathiri sana utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi. Natoa mfano Jimbo la Singida Magharibi na Majimbo mengi Tanzania tumepokea fedha za ujenzi wa vituo vya afya, hosteli na mabweni lakini fedha hizi zimepokelewa kuanzia mwezi wa Aprili na Mei ni wazi itakapofika mwisho wa *financial year* fedha hizi zitakuwa hazijatumika zitarudi Hazina na hatujui zinakwenda kutumika namna gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali yangu haioni umuhimu wa kusitisha mpango huu na kuruhusu fedha hizi ambazo tayari zinawagusa wananchi wanyonge zisirudi Hazina zaidi sana ukawekwa mpango wa *kuzi-monitor?* (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu unasubiriwa na Waheshimiwa Wabunge wote hawa kwa majibu ya swali hili muhimu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, najua jambo hili lilzungumzwa hapa na wewe mwenyewe ulionesha *interest* kubwa lakini na pia kuitaka Serikali ilifanyie kazi. Nashukuru leo limerudi tena naomba kutoa ufanuzi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapeleka fedha nyingi sana sasa hivi kwenye Halmashauri kwa ajili ya

maendeleo. Upelekaji huu ni wakati wote, toka tulipoanza mwanzo wa mwaka wa fedha na tutaendelea kupeleka mpaka mwisho wa mwaka wa fedha ili kuwafanya wananchi waweze kupata maendeleo kuititia miradi inayolengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuliliwekea sheria ambazo zinataka fedha inapofika angalau tarehe 15 ya mwezi wa Juni wa mwisho wa mwaka wa fedha kama Halmashauri hajamudu kufanya matumizi lazima zirudi halafu tuliweka utaratibu wa kama Halmashauri imeperekewa fedha na wamefika muda wa mwisho wa kushika fedha na kutaka kuzirudisha, waweze kuandika barua ya kuonesha kwamba mpaka tarehe hii bado tuna fedha ambazo hazijatumika kwa sababu ya taratibu za manunuzi labda kwa sababu pia kwenye taratibu za manunuzi unapotengeneza mradi unalipa kadiri hatua fulani inavyofikiwa.

Kwa hiyo, inawezekana kuna miradi ambayo inafikiwa mwezi Juni tarehe 15 ipo kwenye hatua labda ya lenta na hajakamilisha kwenye *finishing*. Utaratibu huu unawezesha pia Wizara ya Fedha kuzirudisha fedha hizi kwenda kwenye Halmashauri ingawa kuna changamoto ambayo Mheshimiwa Mbunge ameionesha hapa na Waheshimiwa Wabunge wote tumeshuhudia kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nini Serikali inafanya kweli hili; niliwaagiza Wizara ya Fedha kubadilisha utaratibu na kufanya maboresho kwenye Kanuni zetu ili kuweka Kanuni ambayo angalau inaweza kuruhusu miezi kadhaa baada ya mwaka wa fedha wa bajeti ili fedha zile ziweze kukamilisha kazi hiyo. Ingawa kwenye hili, hatutahitaji mwanya wa wazembe kukaa na fedha bila kuzitumia akitegemea ataongezewa muda. Pamoja na Kanuni hiyo ambayo tutaiboresha lakini bado tutaweka kipengele kinachombana mwajiri/mtendaji wetu kule kuhakikisha kwamba kila fedha inayoingia lazima itumike kwa kipindi kinachotakiwa kwa sababu wengine wanawenza kukaa na fedha mpaka miaka miwili, sasa hilo hatutaruhusu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaangalia ni miezi mingapi inaweza kutufaa ambayo itaingia mwaka wa pili wa fedha ili fedha hii iweze kukamilisha miradi hiyo lakini kwa barua vilevile inaonesha kwamba amepata fedha tarehe fulani labda ndani ya Juni yenye we na mradi umeshaanza kutekelezwa upo hatua fulani na lazima tukakague tuone kama kweli fedha ile imebaki na inatakiwa itumie kufikia kipindi hicho, huyo tutamridhia. Vinginevyo hatutaruhusu mtendaji yejote akae na fedha kwa uzembe tu halafu ategemei kupata *offer* ya kuongezewa miezi mingine, hao watachukuliwa hatua kali ili tuweze kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha kwa sababu wananchi wanahitaji miradi na kuona fedha inatumika vizuri na Waheshimiwa Wabunge kama Wenyevitii wa Kamati za Maendeleo kwenye Jimbo ni lazima na ninyi mridhike kwamba fedha iliyokwenda imetumika kwenye mradi kusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inafanya maboresho hayo na tutatoa taarifa katika kipindi hikihiki cha Bunge ili muondo ke hapa mkiwa na uhakika kwamba fedha iliyotumwa kwenye maeneo yenu inaweza kutumika lakini pia imepata fursa ya kutumika kipindi kijacho cha fedha. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, uliza swali lako tafadhali.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, zao la chai lina soko kubwa sana hapa nchini na hata soko la dunia. Nini kauli ya Serikali juu ya wakulima wa chai wanaolima chai lakini chai hiyo inauzwa kwa bei ya chini sana na kuwanufaisha watu wa katikati ambao wao hawawezi kusaidia hawa wakulima wakaweza kukidhi mahitaji yao?

Naomba kauli ya Serikali juu ya bei ya chai hapa nchini Tanzania. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu ya swali hilo, tafadhalii.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakagenda, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mazao yetu haya chai ikiwemo Serikali inaendelea kuyasimamia kuanzia kilimo mpaka masoko yake na malengo ya Serikali ni kumnuifaisha mkulima aweze kupata tija ya kutosha kwa kuuza bei nzuri kwenye masoko yetu.

Nakiri kwamba tunayo changamoto kwenye masoko ya zao la chai, hata tulipokuwa kwenye kikao pale Njombe miezi miwili iliyopita tulizungumza kwa kina juu ya tatizo la soko la zao la chai ambalo kwa sasa minada yake inategemewa sana kufanywa nchini Kenya kwenye Jiji la Nairobi pekee badala ya minada ile kuendeshwa hapa nchini na kuongeza gharama za uendeshaji wa zao hili kuliko kama tungeweza kuanzisha mnada hapa. Makubaliano ambayo tumefanya pamoja na wadau ni kuanzisha soko hapahapa ndani ya nchi ili kuwezesha zao hili kupata bei nzuri kwenye masoko yetu na kuwataka wanunuzi waje nchini wanunue hapa na kwa hiyo itapunguza gharama za uendeshaji wa mkulima mwenyewe na wengi wapo kwenye ushirika na ushirika wenyewe ili bei ile iweze kumsaidia mkulima kuweza kulilima tena zao hili na kulifanya kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika miaka/mitatu iliyopita tumepata changamoto sana, nimetembelea Rungwe kwa Mheshimiwa Mwakagenda, nimetembelea kwenye kiwanda lakini nimezungumza na wakulima pale Rungwe nimeona tatizo kubwa miaka hii miwili/mitatu unaotokana na ugonjwa wa Covid kwamba masoko yetu kule tumeshindwa kuyafikia na kwa namna hiyo hata wanunuzi wamekuwa hawaamini kununua mazao kwa umbali pamoja na kwamba tuna mifumo ya kielektroniki, hata hivyo bei zake zimekuwa za chini sana. Kwa hiyo, tunachofanya hapa, tunaendelea kupunguza hao watu wa kati ambao wanazidi kupunguza

faida ya mkulima na kumfanya mkulima moja kwa moja kupitia ushirika wake aingie kwenye mnada ambao tumeupanga kuufanya humuhumu ndani. Hivyo ndio njia sahihi ambayo tunadhani inaweza kutusaidia pia kumfanya mkulima apate fedha yake moja kwa moja badala ya watu wa katiba ambao wakati mwengine wanafanya thamani ya zao kupungua.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali tunaendelea kuona na kubaini masoko kupitia Balozi zetu kuona ni Balozi ipi nchi hiyo inahitaji chai ili tufanye mauzo ya moja kwa moja na nchi hiyo ili zao letu kwa kweli liweze kupata bei. Kwa hiyo, jitihada za Serikali zinaendelea na niwahakikishie Watanzania kwenye mazao yote chai ikiwemo, tunaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba tunapata masoko ya uhakika ili wakulima wetu wote wapate faida kwenye kilimo wanachokilima na hasa kwa kutafuta mifumo mizuri ya masoko. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mbunge wa Kibamba, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushuruku kwa kunipa nafasi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na adha kubwa sana ya mafuriko ya mara kwa mara hasa nyakati za mvua nyingi hapa nchini na hasa katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Mafuriko haya yamesababisha changamoto kubwa sana kwa wananchi kwa kuondokewa na nyumba lakini pia taasisi za Serikali kama shule na maeneo mengine. Je, ni upi mkakati sasa wa Serikali katika kumaliza kabisa changamoto hii? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mmh! Waheshimiwa hili swali niliruhusu kweli?

**WABUNGE FULANI:** Hapana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, uliza swali lako.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu imeendelea kutoa matumaini makubwa kabisa kwa wawekezaji kuja kuwekeza hapa nchini. Hivi karibuni tumeona mfanyabiashara mkubwa kama Dangote amejenga imani na kuahidi kuwekeza zaidi hapa nchini lakini kumekuwa na changamoto nyingi sana katika kuwekeza hapa nchini. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha sasa hivi inatengeneza sheria bora na kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza zaidi hapa nchini kwetu? Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Hili nalo pana mno, Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali. Mnauliza maswali mapana mno.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabati, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameomba kujua mkakati wa Serikali na maboresho yake kwenye uwekezaji. Watanzania wote mtakiri kwamba Serikali yetu imeweka msisitizo wa kuhakikisha kwamba tunapanua wigo unaowawezesha wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza nchini kwa sababu fursa, malighafi na *labor* tunazo za kutosha. Sisi tunavutia uwekezaji kwa sababu maeneo mengi ya uwekezaji pia yanapunguza changamoto yetu ya ajira kwa Watanzania. Kwa hiyo, mfanyabiashara Dangote aliyejukua ambaye amewekeza kwenye kiwanda cha saruji Mkoani Mtwara ni mionganini mwa wawekezaji wakubwa nchini ambao pia tumetoa fursa za kupanua wigo wa uwekezaji wake.

Mheshimiwa Spika, nini Serikali inafanya kupanua wigo wa uwekezaji? Kwanza tunafanya maboresho ya sheria na kanuni zetu kwenye uwekezaji ili kujenga mazingira mazuri wezeshi ya uwekezaji nchini ili kila mwekezaji anayekuja kuwekeza apate huduma hiyo kwa ukaribu. Tumeanzisha taasisi inaitwa *Tanzania Investment Center* ambapo mwekezaji atapata huduma zote kuititia taasisi hiyo tunaita *One Stop Center* na tunaweza kumpa ardhi na aina yoyote

ya msaada ambao anauhitaji katika uwekezaji wake.  
*(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania ya leo hatuna shida ya ardhi, ardhi tunayo, umeme upo wa kutosha, maji tunayo, barabara zetu nzuri na mazingira ya uwekezaji Tanzania sasa ni mazuri. Sheria hizi ambazo tunaendelea kuzirekebisha na kuzifanya kuwa sheria wekezi zitasaidia sana wawekezaji kuja nchini kama ambavyo tunaona sasa kasi ya wawekezaji kuja kwenye maeneo haya imeongezeka. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wawekezaji wote mliopo ndani ya nchi na walio nje ya nchi kuja Tanzania kuwekeza kwa sababu mazingira ya uwekezaji yanaendelea kuboreshwa. Sasa hivi tunakaribia kuweka ile sheria ambayo imekusanya changamoto nyingi ambazo zillikuwa zinawakwaza wawekezaji na mengine ni ya kisheria kwa hiyo tunafanya maboresho ya sheria ili kuondoa vikwazo vyta uwekezaji Tanzania. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, pia tunataka tuainishe huduma ambazo sisi tunazitoa au fursa zilizopo Tanzania ili kuhakikisha kwamba tunafanya wawekezaji kuwa na imani nasi. Wiki iliyopita nilikuwa Mkoani Mara kwenye mkakati wa kutangaza vivutio vyta uwekezaji. Huu ni mwendelezo wa kutangaza fursa za mikoa yote nchini ambapo mpaka sasa tumeshafika mikoa 24 kuhakikisha kwamba tunawaonesha wawekezaji nini kipo kwenye mkoa huo ili kila mmoja aamue kwenda mahali anapotaka. Tuna malighafi nyingi sana zinazogusa kwenye sekta ya kilimo, madini na maliasili, hizi zote pia zinasaidia uwekezaji. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kufanya maboresho haya mara kwa mara ya kupitia changamoto tulizonazo na tunazziingiza kwenye sheria ili tuwe na sheria endelevu ambayo pia inaweza kutusaidia kuwekeza. Yale yote ambayo yanajitokeza kwa sasa tunayachukua, tunayafanya utaratibu wa kuyaboresha hivyo na kurahisisha

uwekezaji huo kwa yejote anayetaka kuwekeza hapa nchini.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Spika, hata hili suala la vibali nya kazi tumeendelea kufanya maboresho ili wawekezaji sasa wawe na uhakika wa kuleta watu wao kuja kuwekeza hapa na mambo mengi ya uwekezaji ambayo yapo kwenye kile kitabu kinaitwa *Blue Print* ambacho kina maelekezo yote ya uwekezaji. Niendelee kuwahakikishia Watanzania fursa tulizonazo zitatusaidia pia sana kunufaisha Taifa letu.

Kwanza mwekezaji akija tutapata kodi lakini mbili ushiriki wa Watanzania, tatu ajira lakini nne malighafi na mazao tunayoyalima pia yanapata soko. Kwa hiyo, jambo hili kwa ujumla wake lina faida kubwa na sisi tunalismamia kuwa linaleta tija kwa Watanzania. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, naomba kulijibu kwa upana huo ili wawekezaji wote wanaotaka kuja nchini waje kuwekeza na sisi tunawakaribisha. Ahsante sana. *(Makof)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga, uliza swali lako.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania imeweza kusaidia baadhi ya nchi za Afrika kujikomboa katika uhuru wa nchi zao. Moja ya nchi hizo ikiwa ni Afrika ya Kusini, Angola, Zimbabwe, Msambiji na maeneo mengine. Katika nchi yetu ya Tanzania, maeneo ambayo yalishiriki katika mkakati huo wa kuzisaidia nchi hizo ni pamoja na Kongwa, Mazimbu Morogoro, Nachingwea na maeneo mengine. Nini kauli ya Serikali kwa Mataifa haya kuhusu kuchangia maendeleo katika maeneo haya ambayo nimeyataja nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.  
*(Makof)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, najua swali hili una maslahi nalo kwa sababu Kongwa ni moja kati ya maeneo ambayo wanaharakati hawa wa kupata uhuru kwenye nchi zao waliishi. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali na Taifa letu la Tanzania limefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kuwa nchi zetu za Bara la Afrika zinapata ukombozi kwa kukaribisha hapa wanaharakati wao kuja kuweka mikakati ya kwenda kukomboa nchi zao na nchi nyingi zimefanikiwa. Mkakati huu ulisimamiwa sana na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye pia alikuwa na ndoto ya kuona Afrika imejitawala na tunaiona imefikiwa, Bara la Afrika kwa kweli sasa hivi kila nchi imejitawala yenye na inaendelea na shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, sasa maeneo yaliyotumiwa na hawa wapigania uhuru kwenye nchi yetu ikiwemo na Kongwa kama alivyosema lakini pia Dakawa, Wilaya ya Kilosa, pale Mazimbu Morogoro hata kule Nachingwea Mkoani Lindi yametoa mchango mkubwa sana ya ukombozi wa maeneo ambayo wapigania uhuru walikuja hapa. Maeneo haya namna ambavyo yanaendeleza hayana mchango mkubwa sana kutoka kwao lakini tunaendelea kufanya mawasiliano nao kwa utaratibu ule wa kujenga mahusiano na nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, bado tuna mahusiano na nchi zote ambazo zimepata uhuru kwa kuwa na wapigania uhuru wao hapa nchini na wao wanatambua mchango huu ingawa mchango wa kuboresha maeneo haya si mkubwa sana kwa sababu ya kubadilika kwa vizazi kwenye nchi zao na kutambua umuhimu wa Tanzania kwenye ushiriki wa ukombozi wa nchi zao. Hata hivyo, tumeimarisha sana

kwenye sekta ya kiuchumi, kisiasa lakini pia kijamii pale ambapo tumefungua Balozi kwenye nchi zao, tunayo mawasiliano na nchi nyingi zipo kwenye Jumulya ya SADC ambayo pia tunakutana mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya viongozi wa nchi hizo wanapokuja Tanzania wanapata hamu ya kwenda kutembelea maeneo haya. Wote mnakumbuka mwaka 2020 kulikuwa na Mkutano wa SADC hapa na Mheshimiwa Rais Ramaphosa mionganoni mwa Marais waliokuja, alipata nafasi ya kwenda Mazimbu na mimi niliandamana naye kwenda kuona eneo lile na akaambiwa changamoto zilizopo pale na ahadi ambazo amezitoa. Tunaamini viongozi hawa ambaobado wana kumbukumbu sahihi na kuona uthamani wa Tanzania kwenye uhuru wao wataendelea kuutambua mchango wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini na sisi tunayo namna ya kuwakumbusha, tunapokuwa na matukio tunawakumbusha na wao wakiwa na matukio yao ya uhuru wanakumbuka nchi yetu Tanzania. Ni vile utofauti sasa wa yule aliyesiriki kwenye ukombozi namna alivyokuwa anathamini nchi yetu; wote mnakumbuka Mheshimiwa Mandela alipotoka gerezani nchi ya kwanza kuitembelea ilikuwa Tanzania, hii ni kwa sababu alikuwa anajua umuhimu wa Tanzania na uhuru uliopo sasa Afrika Kusini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunatarajia pia na Marais wengine kuititia taratibu zetu za Kidiplomasia wataendelea kuitambua nchi yetu na maeneo ambayo wamepatia uhuru kwa kuungana na maeneo hayo kuyaboresha na kuweza kuyafanya kuwa endelevu kama maeneo ya kumbukumbu kwao na sisi pia. Kwa hiyo, tunaendelea kushirikiana na nchi hizo ili kujenga mahusiano ya karibu zaidi kwa Bara la Afrika. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekamilika. (*Makofii*)

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaendelea na maswali ya kawaida na tunaanza na swali la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

Na. 361

**Barabara ya Kisamba – Salama Kuhudumiwa  
na TANROADS**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Kisamba – Sayaka hadi Salama inayounganisha Mkoa wa Mwanza na Simiyu itaanza kuhudumiwa na TANROADS?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mbunge wa lleje, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Godfrey Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG.  
GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kisamba – Sayaka hadi Salama ni barabara ya Wilaya inayohudumiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijiji (TARURA).

Mheshimiwa Spika, ili barabara yoyote iweze kuhudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) zipo taratibu ambazo lazima zifuatwe ikiwa ni pamoja na maombi ya kupandishwa hadhi ya kuwa barabara kuu ama ya mkoa kuwasilishwa kwenye mamlaka zinazohusika kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa kwenye Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 ambayo

imeainisha pia vigezo vinavyohitajika katika kupandisha hadhi barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza lakini nina maelezo kidogo. Taratibu zote za kisheria zimeshafanyika kutoka *DCC* mpaka *RCC* kwa maana ya mkoa. Barabara hii ina sifa zote za kuhudumiwa *TANROADS* kwa sababu ni barabara inayounganisha mkoa kwa mkoa na ina kilometra 24, inaingia kwenye Wilaya ya Busega maeneo ya Mwamagulu kuelekea Tisamba pamoja na Bariadi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Sasa swali.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, swali ni kwamba kwa kuwa barabara hii ni ya muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Magu, Busega pamoja Simiyu, je, Wizara ipo tayari kukasimiwa barabara hii kuihudumia ili kuondoka *TARURA* kwa sababu ni barabara muhimu?

**SPIKA:** Unaomba isiwe *TARURA* iende *TANROADS*?

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ikasimiwe kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS* kwa sababu ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa wilaya tatu hizi kwa maana ya mikoa miili.

**SPIKA:** Si ndiyo swali lako la msingi linasema hivyo?

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Ndiyo.

**SPIKA:** Ameshajibu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma.

Na. 362

### **Barabara ya Kilosa - Mikumi**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Kilosa hadi Mikumi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer Godfrey Msongwe.*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilosa – Mikumi ni sehemu ya barabara ya Dumila – Rudewa – Kilosa – Mikumi yenyе urefu wa kilometra 142.3 ambayo ni ya Mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kuitia Wakala wa Barabara nchini *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara kutoka Dumila hadi Rudewa yenyе urefu wa kilometra 45 ulishakamilika na barabara inatumika.

(ii) Ujenzi wa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara kutoka Rudewa hadi Kilosa yenyе urefu wa kilometra 24 ulianza Februari, 2019 na unatarajiwा kukamilika mwezi Oktoba, 2021.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya barabara iliyosalia kutoka Kilosa hadi Mikumi yenye urefu wa kilometra 73.3 kwa lengo la kujenga kwa kiwango cha lami imeshakamilika. Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu hiyo ya barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nashukuru kwa ujenzi unaofanyika. Licha hivyo nina maswali mawili mafupi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tukiwa tunasubiri upatikanaji wa fedha na kwa kuwa upembuzi yakinifu umefanyika kwa muda mrefu, je, kuna mkakati gani wa Serikali wa muda mfupi wa ukarabati na kutambua sehemu korofi za barabara hii ya Mikumi – Kilosa ambaa unaweza ukafanyika kwa upande wa lami nyepesi kwenye sehemu korofi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa barabara hii inaendelea mpaka Magore, Tuliani, Mziha, Handeni kule Tanga; na sehemu ya Tuliani mpaka Mziha bado hajajengwa kwa kiwango lami. Ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami ili barabara hii ikamilike? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri Ujenzi, Mheshimiwa Eng. Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara kipande cha kuanzia Kilosa mpaka Mikumi fedha ya matengenezo ipo.

Kwa kuwa mvua ilikuwa inanyesha baada ya mvua tu kukatika wakandarasi watakwenda kazini kuhakikisha kwamba maeneo yote yale ambayo yalikuwa yana tatizo yanarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kuweka lami nyepesi itakuwa ni gharama kwa sababu barabara hiyo iko kwenye mpango wa matangenezo na fedha inapopatikana tunaendelea kujenga. Tutakachofanya tu ni kuikarabati kwa kiwango cha changarawe ili iendelee kupiditika lakini tutakapopata fedha tutajenga barabara zote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu barabara ya kuanzia Mziha – Turiani, katika bajeti ya mwaka huu fedha imetengwa kwa ajili ya kuendelea kuanzia Turiani na kuendelea upande wa kwenda Tanga. Kwa hiyo, kama ataangalia bajeti ili yopitishwa fedha imetengwa kwa barabara zote hizo mbili kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaelekea Maliasili na Utalii swalii la Mheshimiwa Atupele Mwakibete.

Na. 363

**Serikali kutoa Maeneo ya Hifadhi ambayo  
hayatumiki - Busokelo**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa wananchi maeneo ya Hifadhi ya Kitulo ambayo hayatumiki ili wayatumie kulisha mifugo yao hususani eneo la Kwipanya?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary F. Masanja, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa Kitulo ilianzishwa kwa GN. Na.279 ya mwaka 2005. Maeneo yote yaliopo ndani ya Hifadhi ya Taifa Kitulo likiwemo eneo la Kwipanya yamehifadhiwa kisheria kulingana na umuhimu wake kiikolojia, kijamii, kitamaduni na kiuchumi. Miogoni mwa sababu zillizopeleke Serikali kuanzisha Hifadhi hii ni pamoja na:-

(i) Kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo vinatoa maji yanayoenda kwenye Bonde la Ziwa Nyasa na Bonde la Mto Rufiji ambapo kwa sasa maji hayo yanachangia kwenye miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo Mradi wa Kufua Umeme wa Maji ullipo katika Bwawa la Julius Nyerere pamoja na Bwawa la kufua umeme wa maji la Mtera;

(ii) Eneo hili linahifadhi uoto adimu wa asili wa misitu na maua uliopo katika eneo husika;

(iii) Kutunza makazi ya wanyama adimu duniani kama vile Kipunjji na Minde; na

(iv) Pamoja na kuhifadhi mandhari ya asili ya milima kwa ajili ya shughuli za utalii.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhifadhi eneo hili la Taifa la Kitulo kutokana na umuhimu wake. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa muuliza swali, endelea.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyogeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba mipaka ya Hifadhi hii ya Kitulo ilikosewa kwa sababu walikuwa wanatumia vijana ambao walikuwa wakibeba zile zege au *beacon* na kwa kuwa zilikuwa ni nzito sana walikuwa

wanatua mahala ambapo siyo mipaka. Maana wanapotua ndio hapo hapo wanafanya mpaka na kusababisha baadhi ya taasisi kama shule mbili pamoja na jamii/familia/kaya kuwa ndani ya hifadhi. Je Serikali iko tayari sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi kwenda kurekebisha mipaka hii ili iwe na uhalisia ama *original* yake ilivyokuwa inatakiwa iwe? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Hifadhi ya Kitulo inajulikana kama bustani ya Mungu kwa sababu ina maua ambayo yanachua na ni hifadhi pekee kwa Afrika ambayo ina maua mazuri sana na kwa bahati mbaya sana hajitatangazwa ipasavyo. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba Hifadhi hii ya Kitulo inatangazwa ili ijulikane kama zilivyo hifadhi nyine? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Atupele Mwakibete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipaka kwamba ilikosewa, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaongozana na yeye pamoja na watalaaam wa Wizara ya Maliasili na Utalii lakini pia nitaomba wataalam wanaotoka katika Wizara ya Ardhi ili twende kuangalia. Pale ambapo itathibitika kwamba mipaka hii ilikosewa basi tutaweza kuirekebisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala hili linalohusiana na utalii, nimhakikishie tu Mbunge kwamba bajeti ya mwaka 2021/2022 imezingatia maeneo muhimu likiwemo eneo hili la Hifadhi ya Kitulo kuitangaza kwa nguvu zote na ukizingatia kwamba hifadhi hii ni ya kipekee hapa nchini. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba hifadhi hii itatangazwa kwa nguvu zote ili watalii waweze kufika katika hifadhi hiyo.

**SPIKA:** Tuendelea Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda. Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Kutokana na changamoto zinazojitokeza katika tafsiri hasa ya mipaka kwenye maeneo ya wananchi pamoja na hifadhi, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii tutaweka utaratibu ambao tunakwenda kupitia mpaka mmoja baada ya mwingine ikiwemo hata ile ya Kazimzumbwe ambayo imekuwa na shida nydingi. Kwa hiyo, tutaifanya kazi hiyo tukishirikisha na wananchi wa maeneo husika ili tuweze kupata tafsiri sahihi tujue ni kweli mipaka imehama au namna gani kwa sababu kumekuwa na kelele nydingi kuhusiana na maeneo ya hifadhi na wananchi. (*Makof*)

**SPIKA:** Yako mambo mengine tumewahi kusema humu ndani, watu wa hifadhi bwana ardhi mnapewa na wananchi, wewe unaendaje kuchukua shule zao zote mbili nazo unazziingiza kwenye hifadhi? Mheshimiwa Waziri mwende mkawe wakali kwa maafisa wenu. Unaona kabisa shule hizi unaweka *beacon* huku na wewe Mkuu wa Hifadhi upo pale pale kwa nini usirudishe hiyo *beacon* nyuma, labda ni mita 100, mita 200 ambayo ina *affect* nini sasa hii? (*Makof*)

Wakorofsi sana watu Maliasili muwe mnawaambia. Sasa unachukua shule za wananchi unaweka ndani hifadhi watoto wakasome wapi? Hata kama mkichukua basi kajengeni shule nydingine kule kijijiini. (*Makof*)

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara na swali la Mheshimiwa Agnes Hokororo.

Na. 364

### **Kufufua Viwanda vya Korosho Masasi na Newala**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafufua Viwanda vya Korosho vilivyopo katika Wilaya za Masasi na Newala ili kuchakata korosho ghafi na kuongeza bei ya zao hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya za Masasi na Newala zilikuwa na viwanda vitatu vitatu vya kubangua korosho vilivyokuwa vikimilikiwa na Serikali na hatimaye kubinafsishwa. Viwanda hivyo ni *Masasi Cashew Factory, Newala I Cashew Factory* na *Newala II Cashew Factory*.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Korosho cha Masasi kilichopo Masasi killibinafsishwa na kuuzwa kwa Kampuni ya *BUCCO Investments Holdings Limited* ambayo ilishindwa kukiendeleza kutokana na Benki ya *CRDB* kuzuia mali za kiwanda baada ya kiwanda kushindwa kurejesha mkopo waliookopa. Hatimaye Kiwanda kiliuzwa na Benki ya *CRDB* kwa Kampuni ya *Micronix Export Trading Co. Ltd* kwa njia ya mnada. Kampuni ya *BUCCO Investments Holdings Limited* hawakuridhika na utaratibu uliotumika kuuza kiwanda hicho. Walifungua kesi mahakamani na kuishtaki Benki ya CRDB. Kesi hiyo bado ipo mahakamani hivyo uendelezaji wa kiwanda hicho umesimama kusubiri maamuzi ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha *Newala I Cashew Factory* kilinunuliwa na Kampuni ya *Micronics System Ltd*, Kiwanda hiki kinaendelea kufanya kazi. Kiwanda cha *Newala II Cashew Factory* kilinunuliwa na Kampuni ya *Agrofocus (T) Ltd*. Tangu kibinafsishwe, Kiwanda hicho hakijawahi kufanya kazi. Hivyo, mwaka 2019 kilirudishwa katika umiliki wa Serikali chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kiwanda hicho kama vilivyo viwanda vingine vilivyorudishwa Serikalini kipo katika utaratibu wa kupatiwa mwekezaji mwingine mwenye uwezo wa kukiendeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo, nimekuona.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa katika majibu ya msingi Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kujenga kongano ya kubangua korosho katika eneo la Masasi, je, ni lini ujenzi huo utaanza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, baadhi ya viwanda vya kubangua korosho vimekuwa vikinunua korosho katika minada ya awali ili kuwezesha viwanda hivyo kubangua korosho na kuongeza thamani. Hata hivyo, imeonekana pia vimekuwa vikibangua korosho kiasi kidogo na nyingine kuuzwa ghafi. Serikali ina utaratibu gani wa kudhibiti jambo hili? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Naibu Waziri Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnes Hokororo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa mfuatiliaji sana kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya korosho na hasa katika uwekezaji kwenye viwanda vya kubangua korosho.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ni kweli Wizara na jukumu la Serikali ni kuhakikisha mazao ya kilimo ikiwemo korosho yanapata soko lakini pia yanaongezewa thamani kwa kuchakatwa katika viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa iliyokuwepo ni kuona korosho hizo zinapata wanunuzi na ndio maana tumeanzisha kongano au *cluster* ya korosho ili kuwahusisha pia na wajasili amali wadogo waweze kushirikki katika kuongeza thamani ya zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilikuwa tumetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kongano hilo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022 kazi hii ya ujenzi itaanza kwa sababu tayari fedha hizo zimeshatengwa kwa ajili ya kujenga kongano hilo la wajasiliamali kwa ajili ya kubangua korosho kwenye maeneo ya Masasi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda na kupata korosho katika minada ya awali, ni kweli ni utaratibu ambao Serikali imeuweka baada ya kuona viwanda vingi vinakosa malighafi ambayo ni korosho kwa ajili ya kubanguliwa katika viwanda hivyo. Kwa hiyo, utaratibu sasa kama alivyosema ni kweli kuna minada ya awali ili angalau viwanda hivi visikose kupata malighafi. Baada ya viwanda hivi kununua korosho hatua ya pili ni mnada ambao sasa unashirikisha na makampuni mengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti viwanda hivi inategemea kwa sasabu kama kiwanda kimeshatosheka na malighafi inayohitajika katika kuchakata korosho basi wana uhuru wa kuuza nje. Kama tunavyojua Tanzania tuna *competitive advantage* kwa maana ya kuzalisha zaidi korosho kuliko maeneo mengine. Kwa hiyo, tukitosheka sasa katika viwanda vyetu *then* korosho inayobaki inaweza kuuzwa kwenye minada ya nje ambapo wanaweza kusafirisha nje kama ambavyo wanafanya sasa.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na swali la Mheshimiwa Kasheku.

Na. 365

### **Tatizo la Maji Vijiji vya Jimbo la Geita**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Mradi wa Maji ambao ulishafanyiwa upembuзи yakini kwa Wananchi wa Vijiji vya Nkome, Mchangani, Katome, Nyamboge, Nzera na Rwezera?

**SPIKA:** Majibu ya Swali hilo Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa maji ambaao utahudumia Vijiji vya Nkome, Mchangani, Katome, Nyamboge, Nzera na Rwezera utaanza katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mradi huo umetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kuanza kazi ambazo itahusisha ujenzi wa chanzo cha maji na kituo cha kusukuma maji kwa maana ya *booster*; ulazaji wa bomba zaidi ya kilometra 70, ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji pamoja na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. Aidha, mradi huo umepangwa kunufaisha Vijiji vingine vya Mnyala, Ihumilo, Nyambaya, Nyakazeze, Itale, Njingami, Lukaya, Chelameno, Bugando, Igate, Bweya, Idosero na Nyarubanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali na wananchi wa Jimbo la Geita Vijiji wamekusikia. Hata hivyo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa majibu haya sasa ni mara ya pili napewa katika katika Bunge lako Tukufu, namuomba Mheshimiwa Waziri yupo tayari sasa baada tu ya Bunge hili kuambatana nami kwenda kuona mazingira halisi ya wananchi wangu wanavyokaa ili aweze kutekeleza mradi huu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mradi huu unaishia katika Kijiji cha Idoselo, Vijiji vya Mkorani, Ibisabageni,

Dubanga, Isulobutundwe vijiji ambavyo wananchi wake wanachota maji umbali wa kilometra tisa, 10 mpaka 20. Je, Wizara haioni umuhimu wa kunipatia angalau visima wakati wao wakisubiri mradi huu wa maji uende mpaka kwao?

**SPIKA:** Hili la kufuatana mpaka uombe kibali kwa Spika. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunilinda suala la kuambatana na Mheshimiwa Musukuma lakini mara baada ya kutoa kibali hicho nitakuwa mtiifu kwako nitakwenda kutimiza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusiana na visima, nimtoe hofu Mheshimiwa Musukumu tutakuja kuangalia hali halisi, wataalam wetu tutawaagiza wafike pale. Tumetenga visima vingi sana ili maeneo yote ambayo ulazaji wa mabomba unakuwa ni mgumu basi huduma ya visima vyta maji iweze kupatikana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo, litaulizwa kwenye Wizara ya Madini na Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali hili na naomba sasa swali kwa ajili ya watu wa Ndanda Wilaya ya Masasi na Kata ya Chiwata namba 366 lipate majibu ya Serikali.

Na. 366

### **Utafiti wa Madini ya Graphite – Ndanda**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali baada ya kukamilika kwa Mradi wa Utafiti wa Madini ya Graphite Kata ya Chiwata?

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka hili ni moja ya swali tulilolirudisha siku za nyuma likajibewe vizuri. Sasa Naibu Waziri anarudi na majibu Mheshimiwa Profesa Manya. Majibu ya swali hilo tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa shughuli za utafiti wa madini ya kinywe katika Kata ya Chiwata ambayo ipo Jimbo la Ndanda, Wilayani Masasi, mpango wa Serikali ni kutoa leseni ambapo hadi sasa leseni mbili za uchimbaji wa kati zimekwishatolewa kwa Kampuni ya *Volt Graphite Tanzania Limited*.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupewa leseni, ni wajibu wa kampuni iliyopewa leseni sasa kuendeleza mradi huo kwa kuanza uchimbaji.

**SPIKA:** Jibu zuri kabisa *straightforward*. Mheshimiwa Cecil Mwambe. (*Makofî*)

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kutokana na kutokuanza kwa mradi huu imesababisha kukosekana kwa shughuli za *CSR* kama ambavyo nilisema wakati uliopita. Kwa hiyo, Mji wa Chiwata na Jimbo la Mtama kwa sababu kuna sehemu inagusa mradi huu, Jimbo la Ruangwa pamoja na Jimbo la Newala *DC* imesababisha kutokuwepo kwa ajira zaidi ya 1,500 za moja kwa moja na zingine za kwenye mgodi na kukosekana kwa mapato ya Serikali pamoja na Halmashauri hizo nilizositaja kiwango cha dola milioni 62. Sasa swali langu...

**SPIKA:** Eehe swal!

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo iliyosababisha tufike hapa, hawaoni kwamba wanafanya hujuma kwenye uchumi wa maeneo haya niliyoyataja?

Mheshimiwa Spika, swal la pili, kutohana na Sheria ya Madini iliyobadilishwa mwaka 2018 ndiyo hasa chanzo cha mgogoro huu na kampuni zinazotaka kuwekeza, Serikali sasa haioni haja ya kufanya mabadiliko ya sheria hii ili wawekezaji hawa waweze kuja na mitaji yao badala ya kulazimishwa kukopa kwenye benki za ndani? Ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Profesa Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama kuna maeneo ambayo yamefaidika na mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 ni pamoja na *CSR* na *local content*. Yawezekana kweli katika maeneo ambayo miradi haijaanza Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuwa hawajaona faida ya mabadiliko ya Sheria ya Madini ila Wabunge walioko katika Mkoa wa Geita katika mikoa ambayo kuna migodi mikubwa tayari watakubaliana na Serikali kwamba ndipo mahali ambapo Serikali imeweza kubainisha sheria pamoja na kanuni za *CSR* na kuweza kufanya bora zaidi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara mradi utakapokuwa umeanza Serikali itasimamia sheria zake pamoja na kanuni za *local content* na *CSR* ili kuona kwamba wananchi wa maeneo husika wanaweza kupata faida.

Mheshimiwa Spika, swal la pili linahusu mabadiliko ya sheria. Mabadiliko haya yalipita katika Bunge lako Tukufu na

kwa mahali ambapo sheria hizi zimetekelezwa vizuri tumeona kwamba kuna tija.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aone kwamba wawekezaji wengine wameshindwa kupata mitaji na wawekezaji wake hawa ni watu wa Australia na Australia ni mahali ambapo kulikuwa kuna *total lockdown* ya *COVID* kwa hiyo kupata mitaji mahali hapo imekuwa ni shida. Hata hivyo, tunaona kwamba wengine wanaona kwamba Tanzania bado ni mahali pazuri pa kuwekeza na Serikali kwa kweli milango ya Wizara iko wazi kuendelea kujadiliana ili tuone kwamba wawekezaji wanakuja, wanachimba na kama ilivyo sera ya Serikali wao na sisi tuweze kupata. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Naambiwa mgodi huu maeneo haya yanagusa Jimbo la Mtama. Mheshimiwa Nape Nnauye swalii, tafadhali.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Serikali ikumbukwe kwamba maeneo haya yalichukuliwa karibu miaka sita iliyopita kwa upande wa Jimbo la Mtama, ikafanyika tathmini wananchi hawakulipwa fidia kwa hiyo maisha yao yamesimama kwa miaka sita. Huu mchakato umeendelea unakwenda unarudi na wananchi hawajui wafanye nini. Serikali iko tayari kutoa fidia pamoja na ile ambayo ilifanyika lakini fidia hii ya miaka sita ambapo maisha ya wananchi hawa yamesimama hawaendelei na maisha yao ya kawaida wakisubiri fidia kwa miaka sita? Serikali iko tayari sasa kutafuta namna ya kuwafidia au vinginevyo tufute wananchi waendelee na maisha yao.

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Nape, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tukubali kwamba mambo haya yalifanyika wakati wa *transition* ambapo Sheria ya Madini ilikuwa inabadilika. Ni kweli kwamba jambo hili lilionekana kama linaleta hofu na wawekezaji walirudi nyuma. Pia sheria inatoa muda wa kwamba kama fidia imefanyika na ikapita miezi sita basi fidia hiyo inaweza kurudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu sasa mazingira yanaboreshwu tutawaomba tena tufanye fidia upya ili wananchi hatimaye waweze kulipwa. Nadhani hilo liko katika utaratibu wa sheria na hivyo sisi tutahimiza sheria ifanye sehemu yake ili fidia iweze kurudiwa na hatimaye wananchi waweze kulipwa na mradi uweze kuanza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Madini.

Waheshimiwa Wabunge, ushauri tu wa jumla. Siku unapotunga swalii kabla ya kulipeleka ofisini kwa Katibu wa Bunge ndiyo siku unapotunga swalii la nyongeza, siku hiyo hiyo. Ukipikirii unatunga swalii halafu swalii lako linapangwa leo ndiyo unatafuta nyongeza unaweza usiipate. Kwa hiyo, pale pale lazima unapotunga swalii lako unabakiza kipande fulani hivi kwamba Waziri akija hivi mimi nitatokea huku. Huu ndiyo utungaji wa maswali lakini ukisubiri limepangwa hapa siku ya *Order Paper* halafu ndiyo unanyanyuka na swalii la nyongeza utajikuta unarudia lile lile na hasa kama ulikuwa umelifunga lile swalii lako jumla yake liliivyo huna namna ya kupata swalii la nyongeza.

Kwa mfano, wewe nia yako ni kuhamisha barabara itoke *TARURA* iende *TANROADS* sasa usitaje, unasema tu Serikali ina mpango gani wa kurekebisha au kuboresha barabara ya kutoka mahali fulani hadi mahali fulani, basi. Sasa Waziri atajibu tuna mpango hivi na hivi, utakapouliza la nyongeza ndiyo unasema kwa kuwa matengenezo haya hayawi mazuri kwa sababu barabara iko *TARURA*, je, Serikali ina mpango gani wa kuhamishia *TANROADS*? Sasa ukishataja na *TANROADS* halafu na nyongeza *TANROADS* sasa inakuwa hujafika sana mbali. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, pia maswali mengine niwafundishe, ule mpango wa Serikali ukishatajwa humu, wana nia sijui ya kufanya kitu gani jimboni kwako ndio siku unapotunga swali kuhusu kile kitu ambacho Serikali imeahidi humu. Sasa Serikali ikijibu wewe unachukua *ownership* ya kile kitu kama Mbunge na mwakilishi. (*Makofi*)

Tunaendelea na wageni waliopo jukwaani. Kuna Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Singida na Mbunge Mstaafu Mheshimiwa Diana Chilolo. Mheshimiwa Diana Chilolo karibu sana hapa Bungeni. Tunafarrijika sana kututembelea, alikuwa pamoja nasi kwa miaka kadhaa na alikuwa muuliza maswali maarufu sana. Safari moja akalalamikiwa na Wabunge maana alikuwa anakaa *center* kwa nini kila akisimama Spika waliokuwepo wakati huo wanampa maswali ya nyongeza? Wengine wakasema kwa sababu ni mweupe, mrembo. Karibu sana Diana, karibu dada yetu. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni 55 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaao ni wafanyakazi na wanafunzi wa UWATA *Pre & Primary English Medium School* iliyoko Jijini Mbeya wakiongozwa na Ndg. Veronica Kamanzi. Wale wanafunzi kutoka Mbeya, karibu sana watoto wetu na walimu wao, mmesafiri kutoka mbali Mbeya mpaka Dodoma Bungeni, hongereni sana. Ahsanteni sana na karibuni. (*Makofi*)

Tuwaombe shule nytingine nchini, kidogo kidogo vijana wawe wanatembelea Bunge. Vijana wakiwa wadogo kama hawa wakitembelea Bunge ile kumbukumbu yake inakaa nao hata mpaka wakizeeka, wanakuwa na kumbukumbu kubwa sana. Ahsanteni sana kwa kufika. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mussa Zungu ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Amos Makalla ameambatana na Ndg. Hamis Ngoda na Ndg. Grayson Silayo. Mheshimiwa Makalla, yupo? Mtu wa *camera* nikitaja wageni basi unanisaidia, hawajaingia nafikiri, wataingia

baadaye. Mheshimiwa Zungu bado hawa wageni wako hawajaingia. (*Makofi*)

Wageni 42 wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini ambao ni wanafunzi na walimu wa Taasisi ya Teknolojia ya *DOMACC* kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Chuo hicho Ndg. Happy Mwajunga. *DOMACC*, hawa pia hawajapata nafasi, unajua *gallery* yetu leo imeja full.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Waziri wa Nishati ambao ni Wakurugenzi wa kampuni ya *TANALEC* ya Jijini Arusha Ndg. Zahir Saleh, Ndg. Victor Omino na Ndg. Edrick Mwenda. Karibuni sana *TANALEC*, yale majiko yenu ya *TANALEC* hayaonekani siku hizi bwana, Yalikuwa maarufu sana zamani. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wengine watatu wa Mheshimiwa Kalemani kutoka Chato Mkoa wa Geita ni kaka yake Ndg. Masalu Kalemani na ndugu zake Ndg. Selfu Mahumbi na Ndg. Didi Deogratius. Karibuni sana ila muangalie msipotee Dodoma hii maana ninyi bwana ninyi. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda Waziri wa Kilimo ni viongozi wa Mkao wa Iringa wakiongozwa na Mkuu wa Mkao wa Iringa Mheshimiwa Queen Sendiga. Hawa Wakuu wa Mikoa naona hawajafika bado.

Mgeni wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati ambaye ni kaka yake kutoka Bukoba Mkoani Kagera Ndg. Amani Kajuna. Ahsante sana na karibu sana. (*Makofi*)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Geofrey Pinda, Naibu Waziri Katiba na Sheria ambao ni watumishi na wanafunzi kutoka Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi kilichoko Mikwambe Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkuu wa Chuo hicho Ndg. Agnes Kajungu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 25 wa Mheshimiwa Gregory Malima ambao ni wanakikundi cha *Wanyausi Group* kutoka Morogoro wakiongozwa na Canon Pangapanga. Wale wa kutoka Morogoro, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Gregory Malima anao wageni watatu wengine ambao ni Wachungaji kutoka Kanisa Anglikana ambao ni Mch. Kenneth Chimwaga, Mch. Canon Meshack Sudai na Mch. Sokoine Mkwama. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni 79 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambao ni Umoja wa Mafundi Cherehani kutoka Kongwa na Dodoma Mjini (UMACHEDO) ambao Mheshimiwa Mavunde ni mlezi wa umoja huo wakiongozwa na Ndg. Sadock Kasuka. Karibuni sana, baadhi wanatoka Kongwa na hapa Dodoma. Mkiona Mheshimiwa Spika amependeza kwa suti zake mjue ni mafundi wangu wa Kongwa hao wanashona. Kwa hiyo, Waheshimiwa mwende mpime suti baadaye kidogo. (*Makofi/ Kicheko*)

Wageni 40 wa Mheshimiwa Antipas Mngungusi, wanamichezo, ma-*Dj* wa muziki na jamaa zake kutoka Shekilango *Family* Dar es Salaam wakiongozwa na Ndg. John Mwansansu Mwenyekiti wa Shekilango *Family* na Ndg. Mashinda Martin. Shekilango *Family*, karibuni sana. Hawa ni wanamitindo, safi sana. Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, hawa wanamitindo kuna wakati waliwataka watutengenezee vazi la Taifa. Sasa zoezi hilo sijui liliishia wapi, labda tukipata vazi la Taifa haya maneno ya kushindana kuhusu mavazi humu Bungeni yanaweza yakaisha. Ahsanteni wanamitindo. (*Kicheko*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*); Ndg. Lonyori Mollel, Ndg. Ngitoria Mayani na Ndg. Leyesu Larmanie. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni tisa wa Mheshiwa Kassim Haji, walimu na wanafunzi wa Chuo cha Abdulrahman Al-Sumait na *Micro-*

*Tech Institute of Business* kutoka Zanzibar wakiongozwa na Mhadhiri Msaidizi Ndg. Abdulhamid Ahmed. Wale wa kutoka Zanzibar, nafikiri hawajapata nafasi pia, *gallery* zetu ziko *full Waheshimiwa*.

Wageni 20 wa Mheshimiwa Daniel Awack, ambaao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango cha Dodoma wanaotoka Wilaya ya Karatu wakiongozwa na Ndg. Yakin Leng'atu. Chuo cha Mipango kutoka Karatu? Pia nao hawa labda watakuwa huko *basement*.

Mgeni wa Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa ambaye ni ndugu yake kutoka Zanzibar Ndg. Issa Juma. Sasa ofisi yangu ni vizuri muwe mna-*cross check* wageni mnaoletewa kama wamefika vinginevyo inatupoteza muda kusoma wageni ambaao *after all* hawapo.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambaao ni viongozi wa CCM Kata ya Nyalumbu, Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata Ndg. Khalid Humel. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni 22 wa Mheshimiwa Abubakari Asenga kutoka Kilombero wakiongoza na Ndg. Nicholaus Mbaga. Wale pale karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni 16 wa Mheshimiwa Shaaban Shekilindi ambaao ni wa kutoka *UDOM* wakiongozwa na Ndg. Mwingo Calvin. Karibuni sana vijana wangu kutoka *UDOM*. Ninyi wote mnatoka Lushoto kule? Inaelekea hivyo, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Atupele Mwakibete ana wapiga kura kutoka Jimbo la Busokelo wakiongozwa na Ndg. Rehema Ulimboka. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni saba wa Waheshimiwa Wabunge kutoka Mkoa wa Njombe ambaao ni viongozi wa *New Life in Christ* wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndg. Esward Mabena. Wale kule, karibuni sana kutoka Njombe. (*Makofii*)

Wageni wa Mheshimiwa Joseph Mkundi ambaye ni Afisa Ardhi Wilaya ya Ukerewe Ndg. Pendo Mwakila. Karibu sana Pendo. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Biharamulo. *UDOM* – Biharamulo, wanaweza kuwa wamekosa nafasi.

Wageni 67 wa Mheshimiwa Cecilia Parezzo ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndg. Sunday Mmbongo. Ooh, karibuni sana. Sasa endeleeni kusimama kidogo, wale wa *UDOM* wote na wale wa mwanzo hebu simameni, karibuni sana. (*Makof*)

Kwa kuwa mnakuja na sisi tunafurahishwa na kuja kwenu na mimi nikiwa mmoja wa waanzilishi wa Chuo cha *UDOM*, wachache wanajua kwa sababu kwenye Bodi ya kwanza kabisa, *University Council* ya kwanza, *University Senate* na nilikuwa ni Mwenyekiti wa *Audit Committee* kwa miaka mitatu ya mwanzo ambayo ndiyo tulifanya *ground work* ya *UDOM*, nafarijika sana napoona matunda ya kazi ya mikono yetu. (*Makof*)

Sasa leo nawapa neno moja tu na kupitia ninyi kwa wanafunzi wengine wa vyuo vikuu, mnasoma elimu ya chuo kikuu, Mungu atawasaidia mtamaliza, cheti kile mnachomaliza nacho isije ikawa ninyi ni watumwa wa cheti hicho. Elimu ya chuo kikuu ikusaidie kukupanua mawazo na kichwa chako, fikra zako na uelewa wako wa mambo. Ukishatoka pale *the sky is the limit*, pambana, changamkia fursa, tajirika na uajiri na wengine. (*Makof*)

Sio lazima maisha yako yote uwe mtumwa wa cheti kile; kwa kuwa ulisoma ualimu basi wewe mwalimu mpaka Mungu akuite, kwa kuwa ulisoma sijui maendeleo ya jamii basi wewe maendeleo ya jamii weee, kwa kuwa ulisoma sijui kitu gani, hakuna hiyo, dunia ya leo ile *degree* sawa unaweka mfukoni unapotoka unaangalia wewe vipawa vyako vya Mungu viko upande gani unasongea mbele. Msikae kusubiri ajira sijui ya Serikali au ya mtu binafsi, ukipata ajira sawa,

usipopata pambana na maisha tajirika, muwe ndio ma-Dangote wetu ninyi. Ahsante sana. (*Makof*)

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati  
kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Kama mnavyojua leo bado tunaendelea na Wizara ya Nishati, lakini Mezani hapa nina kimbembe. Wachangiaji wa CCM peke yake ni 50, walio wachache ndio bado wachache na ninyi mnaweza mkaongeza jina moja mawili pia ili mpambane. (*Kicheko*)

Sasa tuta-fit vipi ni kwamba, kwanza itakuwa dakika tano-tano, ndiyo ukweli wenyewe, maana tunafanyaje katika hamsini hii? Hilo ya kwanza, lakini la pili, ukiitwa hupo ndiyo imetoka hiyo hutaweza kupata nafasi tena, kwa hiyo, tutajaribu tunavyoweza.

Kwa hiyo, moja kwa moja tunaanza na Mheshimiwa Selemani Kakoso na atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nishukuru sana kunipa nafasi ya kuwa mionganoni mwa wachangiaji wa kwanza asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niipongeze sana Serikali kupitia kwa Waziri mwenye dhamana kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya, hasa kwenye mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambapo naamini mradi huu ukikamilika utatua tatizo la umeme kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya Mradi wa *Standard Gauge*. Sisi kama Kamati ya Miundombinu tumeikagua reli, tumeshuhudia jinsi Serikali ilivyozanza kujenga vituo vya kupozeshea umeme kuititia Shirika la *TANESCO* ambalo naamini kabisa ndiyo tunategemea huo umeme uweze kuendesha Shirika hilo la Reli kuititia reli ya mwendokasi. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sana mradi wa *Grid* ya Taifa, hasa kwa Mkoa wa Katavi. Mkoa wa Katavi unakua, una mahitaji makubwa lakini kwa bahati mbaya sana tunatumia umeme wa ma-*generator* ambao kimsingi haukidhi mahitaji ya watumiaji. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri afanye mikakati ya haraka kuhakikisha Mradi wa Umeme wa *Grid* ya Taifa kutoka Mkoa wa Tabora kuititia Wilaya ya Sikunge uweze kukamilika haraka na ule mradi ambao unatokea Mkoa wa Mbeya, Songwe, Sumbawanga kuja Katavi nao ukamiliike. Pia naomba ule Mradi wa Malagarasi, sisi Mkoa wa Kigoma ni jirani naamini ukikamilika utasaidia sana wananchi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Mradi wa *REA*. Tunaishukuru sana Serikali imeleta Mradi wa *REA* kwenye maeneo ya Jimbo langu, Wilaya ya Tanganyika lakini vipo vijiji vingi ambavyo bado havijapata umeme. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aweze kukamilisha miradi kwenye Kata ya Mishamo, Kata ya Bulamata, Ipwaga na Ilangu ambapo kwa ujumla vijiji vilivyobaki vipo 26 kwenye Jimbo la Wilaya ya Tanganyika. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na kutuletea mkandarasi ni vyema akawa na usimamizi wa karibu sana ili kuhakikisha miradi hii inakamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kuleta wakandarasi, vipo viko vijiji ambavyo kwenye Mradi wa *REA* //vilisahaulika, hasa kwenye Tarafa ya Karema, kipo Kijiji cha Kasangantongwe. Naomba Mheshimiwa Waziri watakapokuwa wanakuja kukamilisha kwa sasa na vile vijiji vilivyokuwa vimesahaulika viwekwe kwenye mpango ili viweze kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, visto vijiji ambavyo vilishapelekewa umeme. Kwa bahati mbaya sana vimepelekewa umeme lakini kwenye maeneo ya mitaa na vijiji, vitongoji vimekuwa havipati umeme wa kutosha. Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kukamilisha taratibu za kupeleka umeme kwenye vitongoji kwani tunapopeleka umeme kwenye vijiji, tusipeleke tu pale kijijini, tunahitaji uwafikie wananchi kwenye mitaa mbalimbali. Naomba suala hili alishughulikie, naamini Mheshimiwa Waziri ni msikivu, ni Waziri pekee ambaye anawasikiliza sana Wabunge na anaenda kila sehemu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, amefanya ziara kwenye jimbo langu, naamini vijiji vingi ambavyo naviongelea yeye anavifahamu. Amefika pale Kasekese, Mchakamchaka, Ifukutwa, sehemu zote hizo amezindua miradi ya maendeleo ya *REA Phase III*. Kwa hiyo, naomba hivyo vijiji viliwyobaki avifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso. Nilishakutaja Mheshimiwa Zacharia Issaay na utafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia mada hii iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji wa miradi ya *REA* nchi nzima. kwa ujumla Serikali imefanya kazi kubwa kuanzia Serikali ya Awamu ya Tano na hii ya sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri Kalemani na timu yake bila kinyongo kwa moyo mweupe maana kati ya miaka hii mitano iliyopita na kipindi hiki tulichoanza wamejtahidi sana kwenye miradi hii ya *REA*. Mimi niseme tu kwamba Waziri amejtahidi sana, ameenda kwenye Jimbo langu karibu mara tatu, nampongeza na kumshukuru na

Mungu aendelee kumbariki. Mchango wake ulikuwa mkubwa kwa mimi kurudi hapa Bungeni kutokana na hii miradi aliyotekeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kidogo kwenye Wizara hii. Kwanza mradi huu unaokuja tunauomba uanze na kata ambazo zimerukwa. Kuna kata ambazo aliahidi kule kwangu akiwa Naibu Waziri na baadaye Waziri; Kata za Murai, Silaloda, Masieda na Nasei.

Mheshimiwa Spika, eneo hili limetusumbua kwa sababu ya jiografia na umbali kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakandarasi mliowateua, niwapongeze wale waliowasiliana na Wabunge wao lakini nimewasiliana na Wabunge wa Mkoa wa Manyara kwa kweli, mkandarasi wetu hadi sasa hajaweza kuonesha utayari wa kuwasiliana na sisi ili tuje mipango yake anayokwenda kutekeleza ikoje. Hii itasaldla sana ikiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge watafahamu jinsi ambavyo miradi hii itakavyotekelawa ili baadaye tuwe kitu kimoja na hata tunapokwenda kwa wananchi tuwe na kauli ya pamoja tukijua utekelezaji wa mradi utaendaje.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye utekelezaji pia wa Mradi wa Ujazilizi. Nina kata 17 ambapo saba ziko mjini na 10 ziko vijijini, lakini watu wa *REA* wanasema wewe wa mji huduma yako ni *TANESCO* na *TANESCO* hata miaka 10 hawataweza kupeleka umeme kwenye kata hizo kwa sababu, mbili hazikupelekewa umeme moja kwa moja Kata ya Silaloda, lakini pia na Kata ya Ilboru kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kama itawezekana, kata zile zilizoko pembezoni kwenye eneo la mji wangu au eneo la Mji wa Mbulu ziingie kwenye *REA* kwa sababu bado hazijafikiwa. Kama nilivyokudokeza Mheshimiwa Waziri, wewe ni msikivu na pia unatusikiliza sana huku Bungeni, lakini tuna hofu kidogo na utekelezaji wa ahadi zako unazotoa. Ukiwaagiza wao hawana majawabu na pia hawatekelezi kwa wakati, utakumbuka mwaka 2019 tulikwenda Mbulu, tulifanya ziara, ukaagiza umeme uende

Gunyoda na Murai, lakini mpaka leo bado. Sasa kupitia hii *REA* inayoanza waanze na kata hizo ili wananchi wale waone ahadi ya Waziri ni ahadi ya Serikali na hiyo ahadi ya Serikali iweze kutoa matokeo chanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kama kuna maeneo ya namna hii, kwa mfano kwenye Jimbo la Mbulu Mji kuna vijiji toka 2009/2010 wamepelekewa umeme kwa kaya kama 20 mpaka 50, kaya nyingine bado zinasubiri kwenye maeneo ya vijiji. Najua timu ya Wizara ilipita wakati ule ikatambua maeneo ambayo umeme haujapelekwa na ramani ilishachorwa basi waanze kwenye hivyo vijiji ambavyo vinahitaji ujazilizi kwa ajili ya kufanikisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa magenge na kuchukua fedha za wananchi. Kumekuwa na tatizo kubwa wananchi wanahitaji umeme, wanaambiwa umeme utakuja, baadaye wanaambiwa hampo kwenye orodha. Kwa hiyo, kuna uchukuaaji rejareja wa fedha kwa wananchi Sh.50,000, Sh.100,000, mianya ambayo sio mizuri sana kwa taswira ya Serikali yetu. Nashauri kama itawezekana watu hawa wadhibitiwe na *TANESCO* na mamlaka zilizoko na pia wananchi wahojiwe kwa nini nguzo tatu zilipelekwa kwa fulani ambaye yuko kijiji fulani badala ya ule mradi unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la muhimu sana na kwa namna ya pekee nashauri kama itawezekana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100, tuko pamoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Niashati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa *message* uliyotoa kwa vijana wetu ni nzuri sana wakaifanyie kazi. Cheti siyo *issue*, *issue* ni Maisha, kwa hiyo, mnasoma mpate vyeti ili muingie kitaa mpige kazi siyo kung'ang'ana kutuma *CV*kwa Wabunge kutafutiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya. Wabunge wote tuliomo humu hakuna Mbunge amepata kura bila kutaja Wizara ya Nishati, hasa upande wa umeme. Ni kazi nzuri, tunaendelea kumwombea Waziri pamoja na wataalam wote wafanye kazi bila kuogopa, najua mtapigwa mishale, lakini sisi Wabunge tunawategemea maana 2025 tutategemea tena kuisema vizuri kulingana na ile ahadi waliyosema watamaliza vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili niseme kuhusu suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere. Niwapongeze sana Serikali na Waziri, sisi kama Kamati tulienda kutembelea mradi ule. Ni heshima kubwa sana, asilimia 85 ya mradi wasimamizi wake ni wazawa. Hii ina tafsiri nzuri, baadaye tutakapoanza kujenga mabwawa yetu mengine tutakuwa na wataalam waliobobea ambao tumewajengea uwezo kwa kuwapa zile nafasi za kusimamia mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu naomba nizungumzie suala la *depotza* mafuta. Ndiyo maana mimi huwa nikisema humu kuna watu wanani piga mishale, sisi Watanzania ni wazuri sana kupanga mipango; Serikali iliamua kupanga mipango na kuwashamasisha wawekezaji wa ndani kwamba mnataka kuwa na *depot* Mtwara na *depot* Tanga ili kupunguza msongamano wa malori Dar es Salaam, lakini pia kulinda hata barabara zetu kule Dar es Salaam, mkahamasisha watu wakawekeza Mtwara na Tanga na Serikali Mheshimiwa Rais na viongozi wote wakubwa wameenda kukagua *depot* zile. Cha kushangaza baada ya wazawa hawa ku-*invest* kwenye

hizo *depot*, wamekopa benki, Serikali imewatelekeza. Katika mpango mliokuwa mmepanga na tulipitisha sheria hapa kwamba mafuta sasa yatanunuliwa kikanda; Kanda ya Kaskazini watanunua *depot* ya Tanga, Kanda ya Kusini watanunua *depot* ya Mtwara, lakini hata yale mafuta yanayoenda nje ya nchi kwenye nchi zinazopakana na Tanzania baada ya ku-*invest* mpango huu umekufa, watu wamekopa hela kwenye mabenki sasa wako taabani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri ile sheria tulioipitisha hapa ya kwamba mafuta yauzwe Kikanda, *depot* zipo na Serikali ninyi ndiyo wajibu wenu miletta mpango huo mkawaingiza chocho wafanyabiashara, ni lini mnaanza kuusimamia mpango huu? Sheria na *fine* tulishapitisha hapa Bungeni watu waende huko, hata nchi kama Rwanda na Uganda mnaweza mkawapeleka Tanga wale wanaotoka Msumbiji wakaenda Mtwara. Hii mnakuza na miji mingine, unapopeleka malori zaidi ya 1,000 unafungua fursa za *ma-guest* na vitu vingine na hii inasaidia hata hiyo mikoa iliyoko pembezoni kuwa na uchangamfu. Mungu hakufanya makosa kutupa ziwa na tukaligawa katika bandari hizi tatu, nashauri sana Mheshimiwa Waziri akija hapa aje na majibu sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine, tulienda kukagua sehemu ya uagizaji wa mafuta kwa pamoja (*PBPA*), ukiangalia kwa mwaka mzima kampuni za nje tu ndiyo zinachukua kazi hiyo, sisi kampuni za Tanzania tumekuwa kama wasindikizaji. Sababu ni nyepesi, mwanzoni walikuwa wanaagiza kwa pamoja na kampuni zote zilikuwa zinatakiwa ziwe ni za Watanzania, lakini baadaye sheria ikabadilika kwamba tuingize na kampuni za kimataifa, kampuni nyingi zinazo-*bid* na kushinda ni kampuni za nje lakini zina kampuni za kitanzania, hazitumii kuomba kwenye kampuni za kitanzania zinatumia kampuni za nje. Sasa wanaposhindana na Watanzania, Mtanzania ana mkopo wa asilimia 14 wa *CRDB*, hawa wenzetu wana mkopo wa asilimia 1 benki za nje. Cha kushangaza zaidi ikitokea Mtanzania umeshinda baada ya kulipa kodi zote za mafuta unatakiwa ulipe *income*

*tax na service levy, mtu akishinda na kampuni ya nje halipi income tax wala service levy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana, mimi niko kwenye Kamati hii, hiki kitu hakiwezekani Mheshimiwa Waziri lazima abadilishe sheria, atenganishe sehemu waagize wazawa na sehemu nyingine waagize hao wa nje. Ama zile kampuni za nje watumie zile kampuni zake za ndani ili Serikali iweze kukusanya kodi. (Makofi)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba sana wapangajili muwe mnaniipanga siku ya kwanza. Hizi dakika tano mashine inachemka, naambiya ahsante. Nakushukuru Mheshimiwa. (Makofi/Kicheko)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Musukuma. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Kalemani na Naibu wake, Mheshimiwa Stephen Byabato. Bahati nzuri Waheshimiwa Madiwani kutoka Ludewa walikuja, Mheshimiwa Kalemani aliwapokea, alizungumza nao, alisikiliza changamoto za Ludewa, kwa hiyo, nampongeza na namshukuru sana. Halikadhalika Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Byabato, naye nampongeza anatupa heshima

sana wanafunzi tuliomaliza Chuo Kikuu cha Tumaini pale Iringa. Hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali kwa bajeti nzuri ya Wizara ya Nishati kwa sababu umeme siyo anasa ni maendeleo. Nadhani kila mtu anaelewa, kwa hiyo, ni vema sana kuhakikisha kwamba hii mipango ambayo inatekelezwa inapewa fedha za kutosha ili wananchi waweze kupata umeme wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika niishukuru sana Serikali tulipata mkandarasi, kule Jimboni kwangu Ludewa kuna kata zile za mwambao ambazo zina mazingira yenye changamoto sana kutokana na uwepo wa Ziwa Nyasa na milima mikali sana. Hata hivyo, nashukuru kwenye Kata za Lupingu, Lifuma na Makonde tayari mkandarasi ameshapeleka nguzo za umeme, kwa hiyo, wananchi wanamuomba tu aongeze kasi zile nguzo wameziona vyta kutosha sasa wanatamani kuona umeme. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba utusaidie hapo. Halikadhalika tumempata mkandarasi mwингine kwa ajili ya kata zilizosalia; Kata za Ibumi, Lumbila na Kilondo, tunashukuru sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na pongezi naomba Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba kuna kata tano za kule Ludewa zina changamoto sana ya umeme; Kata hizo ni Milo na Mawengi. Kata hizi mbili zina mradi ambao ulikuwa unasimamiwa na mzalishaji binafsi ambaye alikuwa chini ya Kanisa Katoliki. Tumshukuru sana Baba Askofu Alfred Maruma huko aliko apumzike kwa amani, alitusaidia sana kupata umeme kwenye Kata za Milo na Mawengi kabla maeneo mengi nchini hayajapata umeme. Kwa bahati mbaya ule umeme sasa hivi unasumbua sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iingilie katika ili wananchi wa Kata za Milo na Mawengi waweze kupata umeme wa uhakika kwa sababu kata hizi mbili zina wakazi wasiopungua 21,000, hospitali kubwa ya Milo ambayo iko chini ya Kanisa la Anglican, shule za sekondari na zahanati ambazo zinahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, pia kuna umeme ule wa Lugarawa ambaao unahudumia vijiji 20 kwenye Kata za Lupanga, Madilu, Lugarawa, Mlangali, Lubonde na Madope. Nako huku kuna wakazi wasiopungua 51,000 na umeme huu pia ulikuwa chini ya mzalishaji binafsi unakuwa wa mgao zaidi ya saa 12 vilevile mzalishaji anashindwa kuuza umeme kwa maelekezo ya Serikali kwa sababu gharama zake za uzalishaji ziko juu. Kwa hiyo, wananchi 51,000 katika vijiji 20 kupata umeme wa mgao wa saa zaidi ya 12 na wakati mwингine mitambo ile inazima kwa muda mrefu inakuwa siyo sawa. Mheshimiwa Waziri niombe kwanza tuwashukuru wale wazalishaji binafsi kwa sababu walitusaidia sana lakini Serikali iweze kuingilia kati kwa sababu tayari TANESCO wameshaingia mkataba mdogo kununua umeme kwa kampuni ile ya Madope basi inunue umeme wote ili shughuli ya kusambaza na changamoto nyingine ziweze kufanywa na Serikali. Wananchi hawa wa vijiji 20 ndiyo wallokichagua Chama cha Mapinduzi, kwenye kata hizi zote wamechagua madiwani wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kamonga. Mheshimiwa Benaya Kapinda, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangila, Mheshimiwa Jerry Silaa na Mheshimiwa Anatropia ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nami niunge mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, nitachangia eneo la Mradi wa Umeme Vijijini (*REA*). Katika jimbo langu utekelezaji wa mradi huu hauendi vizuri. Nimekwenda mara kadhaa kwa Mheshimiwa Waziri, nimemuomba afanye ziara aje ashuhudie kinachoendelea. Bahati nzuri aliniahidi mwezi wa pili tungeenda naye lakini bahati mbaya mambo yaliingiliana hakufanikisha. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri afanye ziara hiyo kwa sababu haiwezekani hapa kila Mbunge anayesimama anampongeza ameenda mara mbili, tatu au

nne kwenye jimbo au wilaya yake, sasa mimi nashindwa kusema. Kwa hiyo, naomba na mimi nataka nije hapa kusema alikuja jana, juzi na siku nyingine.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ni vijiji 34 tu ndivyo vilivyofungiwa umeme kati ya vijiji 117, kata 16 zote hazina umeme ziko gizani. Hata hivyo vijiji 34 ni kituko, utakuta kijiji kimoja ni nyumba sita tu ndiyo zimeingiziwa umeme. Sasa hivi kuna wananchi 2,100 waliomba kufungiwa umeme katika nyumba zao, wameshafanya kila kitu na wamelipia mita, ni zaidi ya miaka mitatu baadhi ya wananchi hawa hawajafungiwa umeme. Navyomuomba twende akashuhudie tafadhali afanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, wiki iliopita Baraza la Madiwani limekaa kikao na lilitoa maazimio. Azimio mojawapo ni la kunitaka mimi nishike shillingi mpaka Waziri aende kule akawaambie ni lini watafungiwa umeme hawa wananchi 2,100 ambaa zaidi ya miaka miwili, mitatu wamelipia umeme lakini hawafungiwi; mita hazipo, vifaa fulani havipo, sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu kuna Kata tatu za Matilli, Mkumbi na Litembo tulisema miradi ingekamilika Desemba lakini haikukamilika. Miradi hii mingine ni ndani ya miaka mitano ya kipindi kilichopita leo zinakuja nguzo, kesho wanaleta nyaya, keshokutwa wanachimba mashimo mpaka leo miradi hii wananchi hawajaona umeme. Kwa hiyo, ni kero kubwa sana mpaka wanasesma hivi sisi tunachagua CCM kwa nia ipi? Wanakuwa na mawazo mengine, sasa si vizuri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ukatikaji wa umeme, Wilayani Mbanga umeme unakatika sana yaani usipokatika chini ya mara 15 siku hiyo kuna umeme, ni mara 20 mara 40 na kuendelea. Hali hii imesababisha wafanyabiashara kupoteza mali zao na mitaji yao na sasa hivi wengi hawafanyi biashara, shida ni nini Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sisi pale tuna vyanzo vya umeme pale pale; kuna watu binafsi wanazalisha umeme wa kutosha lakini unaenda kwenye Gridi ya Taifa hapa Mbinga kilometra 2 tu hamna umeme. Kuna mwingine anazalisha mjini pale lakini hamna umeme. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majumuisho hapa atuahidi anakuja lini lakini hizi kata ambazo zina mradi sasa hivi umekaa miaka mitano hauishi lini tunaenda kuwashaa umeme? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mengi lakini naona muda huu hautoshi, niseme tu naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga, kwa kweli umeeleza kwa uchungu sana lakini naamini ujumbe umefika, hongera sana. (*Makofii*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Neema Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Jerry Silaa na Mheshimiwa Anatropia ajiandae.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na nianze kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kusema kwamba ajira yangu ya kwanza ilikuwa kwenye sekta hii ya nishati na madini. Kipekee kabisa napenda kumshukuru yeye mwenyewe Waziri Kalemani, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo pamoja pia na Mheshimiwa Jenista Muhagama kwa ulezi bora walionipa hadi kufikia hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia eneo la usambazaji wa gesi nchini. Wengi tunafahamu kwamba *TPDC* haitekelezi zoezi la usambazaji wa gesi nchini kwa kasi inayotakiwa vilevile nchini Kenya na Uganda wanahitaji kununua gesi kutoka kwetu. Napenda kugusia Sheria ya *Oil*

*and Gas Revenue Managementya 2015 ambayo Bunge lako Tukufu liliipitisha.*

Mheshimiwa Spika, kwenye sheria hii ilikuwa imesema kwamba kutakuwa kuna mfuko maalum ambapo fedha zile zitatumika kuendeleza sekta ya mafuta na gesi nchini. Hivi sasa tunapoongea kutokea 2015 mpaka sasa mfuko huu una takriban shilingi za kitanzania bilioni 400 ambazo zimekaa tu kwa sababu kwenye sheria kiliwekwa kifungu kwamba fedha ile haiwezi kutumika mpaka mfuko ufikie asilimia 3 ya *GDP*.

Mheshimiwa Spika, itatuchukua muda mrefu sana kwa mfuko ule kufikia hiyo asilimia 3 na ndicho kiwango cha zaidi ya asilimia 3 ndipo ambapo *TPDC* itaruhusiwa kutumia kwa ajili ya kuwekeza kwenye mafuta na gesi asilia. Kwa hiyo, kwa unyenyekevu mkubwa sana napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri ailette ile sheria hapa Bungeni ifanyiwe maboresho ili sehemu ya ile shilingi bilioni 400 ambayo sasa hivi imekaa *TPDC* waweze kuitumia ili waweze kuendeleza miundombinu ya gesi, usambazaji wa gesi lakini pia kuuza gesi hii nchini Kenya na Uganda jambo ambalo litaendelea kutupa rasilimali fedha ambayo tunahitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengi tunaendelea kulalamika kwamba *TPDC* ipewe fedha lakini tofauti na *REA* mfano Wizara inatoa kiwango cha fedha kwenye *REA* lakini *TPDC* halipewi fungu lolote kwenye hili eneo la uendelezaji wa hii miundombinu kwenye sekta ya gesi asilia. Kwa upande mwagine tunayo shilingi bilioni 400 ambayo imefungwa kutokana na kile kifungu cha sheria. Kwa hiyo, naomba sana kwa unyenyekevu Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie ni lini atawezekutuletea maboresho ya ile sheria ili sisi kwa umoja wetu tuweke vifungu na maelekezo ya namna gani ambavyo *TPDC* itawezekutumia sehemu ya fedha iliyopo ili isiendelee kukaa huku na sisi tunaendelea kupoteza mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba niongelee Mkoa wangu wa Kagera. Sisi Mkoa wa Kagera toka Uhuru mpaka leo hatujawahi kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa

tunategemea umeme wa Uganda na uhitaji wa umeme Uganda nao umezidi kukua kiasi kwamba hata na wao wanunuua umeme kutoka kwetu. Kwa hiyo, napenda kupata kauli ya Mheshimiwa Waziri ni lini sisi Mkoa wa Kagera tutaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa kwa sababu hali ilivyo sasa kuendelea kutuweka gizani; moja ni hatari kwa sababu sisi ni mkoa wa mpakani, lakini pili unaendelea kudhoofisha ukuaji wa uchumi wa Mkoa wetu wa Kagera. Kwa kuzingatia kwamba sisi ni mkoa wa mpakani na ni hatari kuendelea kutuweka gizani, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atupe uhakika ni lini atatuletea Gridi ya Taifa mkoani Kagera tukizingatia imeshafika mpaka jirani yetu Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana naunga tena mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Lugangira. Mheshimiwa Jerry Silaa atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia na Mheshimiwa Martha Mariki ajiandae.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kunipa nafasi kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza, niungane na Wabunge wengine kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyo fanya katika usambazaji wa umeme wa *REA*. Sisi Wabunge wa majimbo ya mijini tunanufaika na usambazaji wa umeme wa Mradi wa *Peri-Urban* kwenye kata zote za Jimbo la Ukonga na kazi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu napenda kujikita kwenye maeneo mawili. La kwanza ni ujenzi wa *LNG Plant* kule Lindi.

Niipongeze Serikali na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 68 ameелеza hatua zilizofikiwa na mipango ya Serikali ya kuhakikisha ujenzi huu unakwenda kwa kasi ama mazungumzo baina ya Serikali na wawekezaji yanakamilika kwa wakati kama vile Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan alivyoelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kutumia timu ile iliyopata uzoefu kwenye Mradi wa Bomba la Mafuta la Uganda ama *East Africa Crude Oil Pipeline* kuitumia katika *negotiation* ya mradi huu. Niiombe Serikali ifanye kila liwezekanalo kuhakikisha mazungumzo haya yanafanyika kwa wakati, lakini katika kuzungumza huko Serikali ijitahidi sana kutumia haraka lakini kuweka mbele maslahi mapana ya Taifa. Kwenye hotuba ya Waziri ameелеza kwamba tayari fidia ya eneo imeshafanyika sasa zile hatua zilizobaki za *pre-FEDD decision*, *FEDD decision* yenewe lakini *final investment decision* na mpaka mradi uanze zifanyike kwa utaratibu mzuri ili Taifa liweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kuishauri Serikali wakati *negotiation* zinaendelea ifanye *micro and macroeconomic study* ili kuweza kuona mradi ule pamoa na faida zile za kifedha zitazopatikana kwenye mradi lakini faida nyingine mtambuka kwenye maeneo yale ya Lindi na Mtwara na maeneo mengine ya Taifa letu. Faida hizo ni muhimu ziweze kufahamika na kujulikana ili Serikali inapoingia kwenye mradi ule iingie kwenye jambo ambalo ukiangalia mtazamo mzima wa *negotiation* kwenye *open book economic model* haziangaliwi basi ziweze kuwa *covered* kwenye *micro and macroeconomic study*.

Mheshimiwa Spika, lakini tujifunze kwa Mozambique, wenzetu wameanza wako katika hatua nzuri sana na hivi tunavyozungumza mnafahamu vinafanyika vikao vya SADC katika kuangalia hali ya usalama ya Msumbiji. Niiombe Serikali itumie vikao hivi hivi kuweza kujifunza kwa wenzetu ili na sisi tufahamu hivi tunavyo-*negotiate* hatuhitaji msaada wa utaalamu maeneo mengine, hatuhitaji ushauri wa majirani zetu ili mradi huu uweze kufikiwa na Tanzania iweze kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, kwenye huu ukurasa wa 68 mradi huu utagharimu siyo chini ya dola bilioni 30 sawa na trillioni 70 za kitanzania. Mradi huu ukianza kuzalisha mapato yanakadiriba kuwa siyo chini ya dola bilioni 3 kama trillioni 7 kwa taifa letu. Niombe kuungana na wachangiaji wa jana

akiwemo Mheshimiwa Getere kama itaipendeza Serikali akina Mheshimiwa Kalemani hawa wakipatikana wawili mmoja akahangaika na huu umeme wa *REA* akapatikana Kalemani mwingine kuhangaika tu na mradi huu wa gesi asilia itasaidia taifa kuweza kuongeza kasi na ufanisi katika kutekeleza mradi huu. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuchangia kama walivyosema wachangiaji wenzangu, niipongeze Waziri, Naibu Waziri na uongozi wa Wizara kwa kushirikisha Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) katika kufanya kazi adhimu ya kulinda kodi na mafuta ya nchi yetu. Ziko dhana nyangi wakati mwingine sisi wenyewe Watanzania tunapenda kujidharau na kuthamini vitu vya nje. Naomba Serikali katika jambo hili ilitilie mkazo na ilifanye kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme Waziri wa Viwanda na Biashara ama Serikali kwa ujumla *TBS* iwezeshwe iweze kufanya kazi hii kwa ufanisi. Nasema hivyo maana hivi tunavyozungumza vifaa vidogo tu vya *detection* ya vinasaba bado *TBS* hawajapeleka *EWURA*. Wizara ya Viwanda na Biashara iko hapa, Serikali iko hapa iweze kuongeza nguvu, jukumu walilopewa ni kubwa iongeze nguvu *TBS* ifanye kazi hii kwa ufanisi kwanza kwa usalama wa Mtanzania lakini pili kwa usalama wa Taifa letu lakini tatu tunaamini Shirika hili ni la kizalendo na ni la Tanzania ambapo manufaa yoyote yatayopatikana yatakuwa kwa Watanzania. Serikali ifungue macho zaidi maana inawezekana Shirika hili likakwamisha mradi huu ili kuonekana tumefeli kuweza kujenga hoja maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofij*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia dakika 10.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii ambayo kimsingi ndiyo inaakisi uchumi tunaoutaka.

Kimsingi ndiyo inaakisi tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda kwa kiwango gani. Nishati ya umeme ndiyo inahitajika katika kuendesha viwanda lakini je tumewekeza kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, nimepitia Mpango uliopita wa Taifa wa Miaka Mitano ambao ilikuwa 2015 – 2020, tulikuwa na lengo kwamba tunavyofika 2020 tunahitaji kufikisha megawati zaidi ya 4,000 ambayo ni 4,600 *plus* kutoka kwenye *megawatt* 1,500 kuja mpaka *megawatt* 4,000 *plus*. Sasa katika hii miaka mitano tumeweza kufika *megawatt* 1,600 *plus* ambayo ni ongezeko la *megawatt* kama 100.2 ambayo sasa ukii *quantify* kwenye *percentage* unakuta ni asilimia 2.1 au tumefeli kwa asilimia 97. Kwa hiyo, ni kweli kwamba hatujafanya vizuri kwa sababu kama tunahitaji uchumi wa viwanda ni lazima tuwekeze kwenye nishati ya umeme na hayo ndiyo yalikuwa malengo yetu ya muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kusaidia viwanda kuweza kutumia gesi asilia, kupitia *TPDC* tulikuwa tunaona mipango mizuri kwenye makaratsi na kwenye maelezo ya Mawaziri kwamba wanaenda kuunganisha viwanda Dar es Salaam na maeneo mengine ili waweze kutumia gesi asilia na wazo liliikuwa zuri sana. *TPDC* walikuja na mpango mzuri kabisa wa miaka mitatu na miaka mitano na wakaonyesha kabisa tutapata faida kiasi gani lakini ukweli ni kwamba kazi kubwa haijafanyika. Hata viwanda tu 11 ambavyo walijiwekea kwa Mkoa wa Pwani kwamba vitaunganishiwa nishati ya gesi asilia iweze kutumia hiyo nishati havijafikiwa; viwanda viwili tu wamemaliza kufanya uchambuzi na kila kitu lakini umeme wa gesi haujaanza kutoka. Kwa hiyo, naamini kwamba kama tunahitaji kufanya vizuri ni lazima nguvu iwekezwe *TPDC* kwa sababu gesi asili inabaki kuwa *cheap* lakini pia tunayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kulikuwa na mipango kabambe ya wakazi wa Dar es Salaam na mikoa mingine kuanza kutumia gesi asili majumbani kwamba watatengeneza miundombinu hizo gesi asilia sasa zianze kupatikana kwenye majumba ambapo itasaidia gharama

kuwa chini. Waliweka *pilot* kwamba wataunganisha viwanda 1,000 na makazi 300 leo ni zaidi ya miaka minne hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, nadhani *TPDC* inahitaji kufanya kazi kubwa kama tunataka tuone mabadiliko kwa macho.

Mheshimiwa Spika, pia walieleza kwamba maeneo ya Kawe, Tegeta na maeneo ya viwanda yataweza kuunganishwa na umeme wa gesi asili lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika. Jambo ambalo limenisikitisha *TPDC* kuanzisha *deposit* ya mafuta kwamba wataweza kuwa *wana-retain petroleum* wakachukua zaidi ya milioni 675 wakakarabati *tank* Na. 8, walivyoanza kukarabati wakagundua kumbe gharama ya kukarabati ni kubwa kuliko kujenga upya wakaahirisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata *CAG* kwenye ripoti yake amesema haya ni matumizi mabaya ya fedha kwa sababu *feasibility study* ilipaswa kufanyika na kuona kipi kifanyike. Nadhani milioni 675 ni fedha nydingi sana. Hata hivyo, lakini bado lengo liko pale pale, naendelea kuishauri Wizara ni lazima tuimarishe *TPDC* na ifanye kazi kwa sababu tunaihitaji. Tayari tumewekeza vya kutosha katika gesi asilia hebu tuitende haki tutaona matokeo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nipongeze kwamba kuna kazi imefanyika na inaonekana imefanyika hasa kwenye suala nzima la *REA*. Mwaka 2015 vijiji vilivyokuwa vimeunganishwa na umeme vilikuwa 2,018 lakini leo tunaongelea vijiji 10,018, ni kazi ya kuigwa. Hata hivyo, hakuna mafanikio yasiyokuwa na changamoto, kuna maeneo mengine kinahesabika kijiji kimeunganishwa umeme lakini ni wakazi 20 tu. Nadhani hapa changamoto inabaki kuwa namna ya kuunganisha umeme.

Nitoe ombi kwa Serikali kama inawezekana, kupeleka umeme vijijini tayari mmetumia gharama ya kutosha, mkandarasi yuko *site* anapaswa kuunganisha umeme kwenye majumba lakini watu hawako tayari kuunganisha umeme. Nadhani ile gharama ya Sh.27,000 ikiwezekana Serikali iibebi, iwaunganishie watu umeme halafu waanze kukatwa kwenye ankara zao, hapo tutaweza kuona matokeo

ya kuunganisha umeme. *Otherwise umeme utakuwa unafika kijiji ni watu hawawezi kuunganisha, ndiyo ushauri naoutoa.* (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Halmashauri yangu ya Kyerwa. Sisi Kyerwa tuna vijiji 99, tunaipongeza kabisa Serikali vijiji vyetu 70 vina umeme, lakini bado tuna vijiji 29 havijapata umeme na REA sasa hii Awamu ya Tatu inaonyesha kwamba mtaunganisha vijiji 19, kwa hiyo vinabaki vijiji 10 ambavyo havijui hatima yake. Niombe sana Serikali hebu muiamini Kyerwa muwape umeme, haya ni maeneo ambayo yalibaki pembezoni, ni maeneo ambayo yamekuwa hayana maendeleo kwa mudu mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia ni lazima tuangalie na umeme tunaopata, tumekuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme kiasi kwamba mtu anaona bora nisilwashe umeme kwa sababu itaenda kuniaribia kila kitu kwa sababu kila baada ya dakika tano umeme unakatika. Kwa hiyo, naomba nivitaje hivi vijiji, kuna Vijiji vya Rwakabunda, Kagu, Omswekano, Ibale, Muleba, Rwanashaju, Kishanda, Ruita, Kishanda, Rurama, Omkitembe, Ibamba, Ruko, Kitoma, Nshunga, Rushe, Kakerere, Nyamweza, Kitega, Bugara, Mugaba, Businde, Nyakasheni, Nyakatera, Kibale, Kigorogoro, Kijumbura, Mgorogoro na Mkombozi. Hivyo ni vijiji vyetu 29 ambavyo havijafikiwa na nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimeeleza kwenye muhtasari wangu kwamba bado vijiji vilivyowekewa umeme ni wakazi wachache sana wana umeme. Nikatoa rai kwamba hebu tubebe hii gharama na tuwe tunawakata kwenye ankara kidogokidogo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, hayo ndiyo nilitaka kuongea. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Anatropia. Mheshimiwa Martha Maliki nilikutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema. Kipekee sana napenda kumpongeza Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Medard Kalemani na Naibu wake kwa jinsi ambavyo wanaendelea kufanya kazi kwa umakini mkubwa na nampongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee sana naipongeza sana Serikali yangu Tukufu kwa kutekeleza mradi wa Mwalimu Nyerere. Mradi huu utakwenda kuleta tija na mapinduzi makubwa sana katika Taifa letu la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali kwa ajili ya mradi wa REA. Katika Mkoa wetu wa Katavi wananchi wanaipongeza sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeleta umeme katika vijiji mbalimbali. Hata hivyo kuna maeneo ambayo bado hayajafikiwa na umeme huu. Hivyo, niiombe sana Serikali kupitia Waziri wetu Mheshimiwa Medard Kalemani vijiji hivi viweze kupata umeme huu ili kuleta tija kwenye uzalishaji katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi ni pamoja na Viji vya Mwamkulu. Kata ya Mwamkulu inaongoza sana kwa uzalishaji wa mpunga lakini kwa masikitiko makubwa bado haijaweza kupata umeme. Hivyo kumekuwa na changamoto katika mashine zile za kukoboa mpunga wananchi wamekuwa wakikwamisha na umeme.

Mheshimiwa Spika, pia katika Kijiji cha Kakese na chenyewe kina uzalishaji mkubwa sana wa mpunga lakini hakina umeme. Baadhi ya vijiji ambavyo pia havina umeme ni pamoja na Viji vya St. John, St. Maria, Mkwajuni na Ikokwa. Tuiombe sana Serikali yetu sikivu...

**SPIKA:** Vyote viko katika Wilaya gani?

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, viko katika Wilaya ya Mpanda, Jimbo la Mpanda Mjini lakini ni Pembezoni, Kata ya Mwamkulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika Wilaya hiyo Mpanda maeneo ya Ulila kuna Kijiji cha Usense na chenyewe hakina umeme, maeneo ya Ugala, Kambuzi na Litapunga. Tunaiomba sana Serikali vijiji hivi viweze kupata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Katavi kwa muda mrefu sana tumekuwa tukitumia umeme wa *generator*. Upo mkakati wa kuleta umeme wa Gridi ya Taifa lakini tunaomba sana Wizara iweze ku-*push* na kuhakikisha kwamba mradi huu unaenda kukamilika kwa muda uliopangwa ambapo umeme huu ambao unatokea Sikunge kuititia Inyonga umepangwa kukamilika mwezi Septemba.

Mheshimiwa Spika, pia ombi letu sisi wananchi wa Katavi, wananchi wa Wilaya ya Mpimbwe wanasesma kwamba kwa kuwa mradi huo utakwenda kukamilika kule Inyonga na Inyonga mpaka Mpimbwe ni takribani kilomita 135, wanaomba kuungiwa *line* ili umeme uweze kutoka Inyonga kwenda Mpimbwe. Kwa kuwa hiyo ni wilaya moja na ni karibu sana tungeomba sana na wananchi wa Mpimbwe waweze kuungiwa *line* hiyo ili umeme uweze kutoka Inyonga na kufika Mpimbwe. Kwa kuwa wananchi wa Mpimbwe wamekuwa wakipata adha kubwa wanatumia umeme wa gridi ambao unatokea Zambia kuititia Rukwa na umeme huo umekuwa ukikatika mara kwa mara kutokana na matumizi kuwa makubwa. Hivyo, tunaiomba sana Serikali yetu siku kuhakikisha kwamba mkakati huu unaenda kukamilika na wananchi wa Mpimbwe, Inyonga na Katavi yote wanapata umeme ili waweze kufanya shughuli zao za uzalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la kukatikakatika kwa umeme limekuwa ni changamoto kubwa ambayo pia imekuwa ikiwakwamisha sana baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Katavi hususani vijana wenzangu ambao wamekuwa

wakijikita katika shughuli za uchomeleaji. Hivyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kuhakikisha changamoto hii inatatuliwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mariki. Nilikuwa namwangilia Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda hapa anasikia mambo ya Mpimbwe kule na wapi anatabasamu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Elibariki Kingu, atafuatiwa Mheshimiwa Noah Saputu na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, tunasema kwamba tunapaswa kutambua na kuthamini kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka mitano nyuma katika suala la nishati na umeme.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na kwa kweli katika hili mimi nitajikita zaidi katika kutoa *complement* na kuongelea maeneo mawili, matatu ya kitaifa, lakini pale ambapo tunaona Wizara zinafanya vizuri na kuleta mapinduzi chanya yanayobadilisha uchumi wa Taifa sisi kama Wabunge tuna nafasi ya kutoa *complement* ili Taifa lijue nini kimefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwa dhati ya moyo wangu uzalendo ulionyeshwa na Waziri Kalemani, mimi kwa hili naomba niwe wazi. Nasema kwa dhati kabisa unyenyekevu wa Waziri Kalemani kwa kiasi kikubwa sana umefanikisha mapinduzi makubwa katika sekta ya kusambamba umeme nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hili kuweka rekodi katika Bunge lako Tukufu. Waziri huyu ukimpigia simu saa sita ya usiku lazima akupokelee na Waziri huyu ukimtumia ujumbe lazima akujibu. Kwetu sisi Wabunge kama kuna jambo linatupa faraja ni kuona namna tunahitaji kufanya mawasiliano na Mawaziri na wanakuwa wepesi katika kuitika. Kwa dhati ya moyo wangu, naomba nitumie Bunge lako kumpongeza sana Waziri Mheshimiwa Kalemani hili ameweza kulishinda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini nampongeza tena Waziri huyu Mheshimiwa Kalemani, juzi tuliona sintofahamu ikitokea katika Shirika letu la Umeme la *TANESCO*, LUKU zikaleta matatizo. Mimi kwa upande wangu nilihisi ni *some sort* ya *sabotage* kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi lakini nampongeza sana Waziri alichukua hatua za haraka za kuwasimamisha kazi watumishi wa *TANESCO* na Waziri Mkuu akaliunga hilo mkono kwa kuruhusu uchunguzi zaidi ufanyike, hilo tunawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niseme Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani, Rais wa Awamu ya Sita kwa muda mfupi na kwa haraka ameshasaini mkataba wa zaidi ya shilingi bilioni 300 kwa ajili ya kuzalisha umeme mwininge kule Kigoma. Naipongeza sana Wizara na Serikali ya Awamu ya Sita kwa sababu changamoto zinazozungumzwa kwa watu wa Katavi ni wazi umeme utakaozalishwa sasa katika Mkoa wa Kigoma utaingizwa kwenye Gridi ya Taifa na utahudumia mikoa ambayo ilikuwa haipati umeme wa Gridi ya Taifa, kwa hilo pia tunawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa natoa pongezi kwa sababu wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi wamepata faraja. Waziri alipotoa namba za wakandarasi waliowapa kazi mimi nimepigiwa simu na mkandarasi anaitwa Central, nimepewa uhakika tutaanza kusambaziwa umeme katika vijiji vyote 34 kuanzia mwezi huu. Mheshimiwa Waziri tunakushukuru na tunakupongeza sana wewe na Serikali na tufkishie salamu hizi kwa Mheshimiwa Rais maana huenda tulidhani kwamba vijiji 2,000 vilivyoahidiwa na Serikali ya

Serikali ya CCM kwenye uchaguzi uliopita vinaweza vikasusua. Peleka pongezi kwa mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu ametutendea haki Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na wapiga kura wote kwa kuyaenzi na kuyashikilia yale mapambano yaliyoanzishwa na Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli katika suala zima la kusambaza umeme kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina taarifa Vijiji vyangu vyaa Mwaru, Mduguyu, Mlandala, Kaugeri, Mpungizi, Irisya, Munyu, Mwasutianga, Mtunduru, Kintandaa, Maswea, Jerumani na vingine vingi siwezi kuvitaja vinakwenda kuanza kuunganishiwa na umeme. Hapa mimi nasema, Mungu akinipa uzima mwaka 2025 nachukua, ninaweka waaa, kwa maslahi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuiomba Wizara, Singida tuna mradi mkubwa wa kutengeneza umeme kwa kutumia upepo. Mradi huu umezungumzwa kwa muda mrefu, kaka yangu Mheshimiwa Kalemani unajua watu wa Singida tunakupenda pamoja na Naibu wako mdogo wangu Mheshimiwa Byabato, mdogo katika umri lakini kiongozi wangu kwa maana ni Naibu Waziri, nawaomba kabisa kwa niaba ya watu wa Singida...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, oooh, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhili nisipompongeza sana Waziri na timu yake nzima kwa maana ya Naibu wake pamoja na Wizara yake kwa ujumla ikiongozwa na Katibu Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kusema kwamba katika usambazaji wa nishati kwa maana ya umeme Tanzania kwa kweli tumevida hatua kubwa sana. Ukipita kwenye mapori na maeneo mbalimbali ukiona jinsi ambavyo nguzo zinapita utaona jinsi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi kwa kiwango kikubwa mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutekeleza llani ya usambazaji wa umeme bado tunaendelea kusema tunakwenda kusonga mbele na kuikumbusha Serikali kuendelea kumalizia maeneo ambayo bado. Katika usambazaji wa umeme wakandarasi ambao walikuwa wamepewa kazi hii wengine wamekuwa siyo wazuri sana, siyo wote lakini siyo wazuri sana. Hivyo, Wizara ni vizuri ikaangalia kwa makini sana wakandarasi hawa ambao wamekuwa hawafanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye Jimbo langu la Arumeru Magharibi mkandarasi aliyepewa kazi pale amechimba mashimo kwenye maeneo mengine hajaweka nguzo, amesimamisha nguzo hajaweka waya, maeneo mengine hayajakamilisha miradi kwenye vijiji na na kadhalika. Uchimbaji wa mashimo umewafanya wananchi, ng'ombe na mbuzi kuvunjika miguu. Naomba Wizara chini ya Waziri wetu Mheshimiwa Kalemani (mchapakazi) afike kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi ili kuweka msukumo katika usambazaji wa umeme kwenye Kata za Bwawani, Nduruma, Kisongo, Musa, Mwandeti, Lingijale, Lemanyata, Kimyaq, Sambasha, Ikiding'a, Oljuroto, Tarakwa, Oturumet, Matebesi, Naroi na Oljoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Sjpika, kama unavyofahamu Jimbo la Arumeru Magharibi ni jimbo ambalo limeweka Jiji la Arusha katikati, kwa hiyo sisi tumezunguka Jiji la Arusha kama yai, wananchi wale wanahamu sana ya umeme. Kwa hiyo,

nimuombe sana Mheshimiwa Kalemani aweze kutembelea na kuweka msukumo wa usambazaji wa umeme kwenye jimbo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu suala la bei ya nguzo. Suala hili limekuwa kizungumkuti kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekuwa akijitahidi sana kutumia nguvu kubwa kueleza kwenye mihadhara mbalimbali kwamba usambazaji ni shilingi 27,000 lakini jambo hili *TANESCO* wanapolitelekeza linakuwa kinyume chake. Sasa inawezekana tunailamu *TANESCO* lakini kuna nini huko ndani? Naomba Mheshimiwa Waziri aweze kufafanua zaidi kupitia waraka maalumu, kama ameandika sijui, lakini kama hajaandika atoe waraka *TANESCO* kwa maana ya *TANESCO* mikoa yote Tanzania, umeme wa *REA* ni shilingi 27,000, je, miradi ya *TANESCO* yenye ni shilingi ngapi, ni shilingi 177,000 au kuna tofauti illi mwisho wa siku wananchi waweweze kuelewa gharama hii ya shilingi 27,000 na shilingi 177,000. Suala hili ni kizungumkuti katika utekelezaji, Waziri anatamka lakini utekelezaji unakuwa mgumu labda kuna kitu ndani. Hilo nalo Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia na kulitolea ufanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la upandaji wa gesi. Ujio wa gesi umepunguza sana uharibifu wa mazingira na huko vijiji ni gesi hizi ndogondogo kwa mfano hii ya kilo sita imepanda kutoka shilingi 16,000 hadi shilingi 20,000. Sasa hali hiyo inaenda kutusababishia uharibifu wa mazingira, wananchi watarudi tena kwenye kukata miti na kuharibu mazingira. Naomba pia hili Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa nini gesi ile ya kilo sita ipande kutoka shilingi 16,000 mpaka shilingi 20,000? Hili nalo ni jambo ambalo Wizara inatakiwa iliangalie kwa makini kwa sababu gesi imesaidia sana katika kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kukatikakatika kwa umeme. Kumekuwepo na tatizo la kukatika kwa umeme, hatukatai kwa sababu mitambo ni mitambo tu lakini pale ambapo umeme unakatika ghafla basi tunaomba Wizara isimamie *TANESCO* iweze kutoa taarifa kwa wananchi

kwamba umeme umekatika kwa muda huu na tunategemea uwake kwa muda fulani au siku tatu au nne. Kukaa kimya au kutowaeleza wananchi umeme umekatika kwa sababu gani na ni kwa nini inaleta wasiwasi na hofu na kurudisha pia maendeleo nyuma. Kuna watu umeme ukikatika dakika moja tu wanapata hasara kubwa sana katika kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, umeme ni nishati ambayo inahitajika sana kwa Watanzania kwa ajili ya kuleta maendeleo tena maendeleo endelevu. Kwa hiyo, niombe kukatika kwa umeme tuwape taarifa wananchi ili waweze kukaa tayari kujua kwamba kuna nini na baadaye watapata kwa wakati gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ole Saputu Noah kwa mchango wako.

Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Costantine Kanyasu, Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo na Mheshimiwa Japhet Hasunga. Mheshimiwa Esther dakika kumi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nishati ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu kwa maana nishati ni uchumi bila nishati hamna utekelezaji wa Tanzania ya viwanda. Pia nishati ikiwepo inaimarisha usalama popote pale Tanzania hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kama nchi au Taifa tuna *Vision 2025* na tumeigawa katika miaka mitano mitano. Malengo ya Mpango wa Pili ya Maendeleo ya Taifa kwa Wizara hii ya Nishati *targetilikuwa kuzalisha megawatt 4,915 kuanzia 2016/*

2017 mpaka 2020/2021 kutoka ile ambayo ilikuwepo ya 1,501. Nimeneku kwenye hotuba ya Waziri mwenyewe anasema mpaka Aprili, 2021 tuna *megawatt* 1,605 kwa maana tofauti kwa miaka yote mitano hii tumeweza kuzalisha *megawatt* 104 tu. Katika malengo haya tulisema tutazalisha hizi *megawatt* zaidi ya 3,014 kwa kipindi cha miaka mitano ili iweze kutosheleza mahitaji ya ndani ya nchi na kuweza kuuza nje ya nchi. Sasa hatujafikia hayo malengo tumezalisha *megawatt* 401 tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nini kimepeleka hiki? Nimejaribu kupitia pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ibara ya 22 anaeleza bayana mathalani fedha tulizotenga hapa 2020/2021 shilingi trillioni 2.17 mpaka Mei walikuwa wamepokea shilingi trillioni 1.3 tu ambayo ni asilimia 60, anakiri hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwendo huu ndio maana tunashindwa kutekeleza mipango ya miaka mitano ambayo tulikuwa tumejiwekea kwa sababu haina uhalisia. Siku zote nimekuwa nikisema tuwe tunakuja na bajeti zenyе uhalisia ili tunavyojipangia tuwe tunajua kabisa kwamba tuna kiasi fulani cha fedha tunakipa kipaumbele ili kutekeleza mradi A kama ni mradi wa Julius Nyerere *Hydropower, LNG* kwa maana gesi asilia tuweze kujua ni kiasi gani kinaenda na kweze kutelekezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tukifikia malengo ya kuuza umeme nje na kuzalisha kutosheleza Tanzania bado umeme wa Tanzania ni ghali sana. Mathalani, wenzetu wa Kagera wanalamika kwamba hawajaunganishwa na Gridi ya Taifa lakini wanaponunua umeme kutoka Uganda kwa Sh.10 wanapata *unit* zaidi ya 80 lakini kwa *category* ile kwa Tanzania ukinunua umeme wa Sh.10,000 unapata *unit* 28. Kwa hiyo, kwanza umeme unavyouzwa kwa wananchi ni ghali sana, Serikali iangalie ni viyi inafanya *standardization* ya bei ili Watanzania wapate huduma hii, tunawapelekea lakini waweze ku-afford/kununua kulinganisha na nchi zingine lakini tunapofikia wakati wa kuuza nje pia bei yetu ikiwa ghali sana hatuwezi kupata wateja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho napenda kuzungumzia ni kutokuwepo na uhalisia wa takwimu ambao tunazitoa kwamba Watanzania wamefikiwa kwa kiasi gani. Nimesoma hotuba ya Waziri hapa anatuambia wameunganisha vijiji 10,312 kati ya vijiji 12,000 na zaidi, wanatuambia kwamba wameunganisha kwa asilimia 86. Wewe Spika umekalia Kiti jana na leo umeona kila Mbunge akisimama analalamika, Mbunge wa Mbinga Vijijini amesema ana vijiji 117 vimeunganisha 34, Mbunge wa Busanda jana amesema ana vijiji 83 vimeunganishwa 26 tu, nikizungumzia Mkoa wa Mara vijiji vilivyounganishwa ni chini ya asilimia 40. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa kila siku najiuliza hizi takwimu ambazo wanatuletea kwamba wameungnisha Tanzania kwa asilimia 86 zinatoka wapi? Wameenda mbali wakasema Watanzania millioni 47 wamefikiwa na nishati ya umeme. Wabunge tupo hapa tujulize kule tunapotoka kwenye wilaya yako umepata umeme kwa asilimia 86? Hii kitu ni hatari sana tukitoa takwimu feki Wizara husika au Serikali ina *relax* hata wahisani hawawezi kutusaidia wanajua tuna-*deficit* kuwafikia Watanzania wote asilimia 13 tu *which is a false*, tutoe takwimu zenye uhalisia ili tuweze kupanga bayana kuhakikisha kwamba umeme unawafikia Watanzania wote kuliko hizi *cooked data*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kingine hapo hapo napenda kushauri, tunapopitisha umeme tunasema tumepitisha kijiji fulani kwamba vijiji 10,000 ukiangalia miji 6, miji 10 kama ilivyo kwenye Sera ya Maji wanasema ndani ya mita 300 basi na sisi tuseme tunapopitisha huo umeme uwe ndani mita 400 au 300 au 200. Unapopitisha kwenye Kijiji A mtu yuko kilometa 8 au 10 unahesabu kwamba Kijiji cha Nyabilongo nipeleka umeme wakati ume-*cover only ten percent or twenty percent*. Hii siyo sawa tutakuwa tunajidanganya hatuwezi kulisaidia Taifa. Wana dhamira ya kweli na unyenyekevu kama wengine walivyosema, mimi mwenyewe nampongeza nikimfuata ni mnyenyekevu sana lakini tufikie *target* yetu, tuwafikie Watanzania kwa uhalisi sio kwa namba kwenye vitabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni uwiano wa mgawanyo wa fedha hizi. Wizara kweli inatengewa fedha nahaziendi kwa uhalisia lakini hata zinazoenda basi tuweze kuangalia hii miradi yote iweze kupata kwa uwiano ili tuweze kutekeleza miradi hii kwa wakati vinginevyo inasababisha gharama kuwa kubwa. Mathalani katika hizi shilingi triliioni 2.3 za mwaka huu zaidi ya shilingi triliioni 1.44 zinakwenda kwenye *Julius Nyerere Hydropower Project* ambacho mimi na-support kwa sababu mradi ule ukiisha utasaidia sana kupatikana umeme nchini lakini pia unaangalia kwenye REA, tunapeleka shilingi billioni 415 tu. Hizi takwimu zenu ndiyo zinasababisha mnapeleka fedha hizi, shilingi billioni 415 haziwezi kwenda ku-covermaeneo yote na sasa hivi hii ni *phase* ya tatu. Tuangalie tukipeleka kwenye REA zaidi ya asilimia 70 au 65 ya Watanzania wataenda kupata umeme tuwekeze fedha huko kwa uwiano amba unatoa uhalisia kuweza kutatua changamoto za nishati ya umeme kwenye maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kingine ni utekelezaji wa gesi asilia, kama nchi tukiamua kuwekeza kwa kasi kwenye mradi wa gesi asilia itasaidia sana. Kwenye hotuba yake amesema kwamba *target* ni kufikia nyumba 10,000 magari 700 na viwanda zaidi ya 20. Pia anasema *by 2021* wamefikia nyumba 1,191 tu *out of* nyumba 10,000 ina maana kutoka nyumba 500 za mwaka 2020 mpaka nyumba 1,191 ni nyumba 691, kwa hizo 10,000 ina maana tutachukua zaidi ya miaka 20 kuzifikia kufikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuamue kuwekeza, ndio maana nikasema uwiano na vipaumbele ni muhimu. Tukiwekeza kwenye gesi asilia kwanza hata kwenye magari inaondoa hata *environmental pollution*, ukitumia *petrol* na *diesel* tunajua uchafuzi wa mazingira amba unatokea. Tukiamua kuwekeza magari mengi Tanzania yakatumia hii gesi asilia tutakuwa tume-save matatizo ya kimazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa upande wa Tarime, nimekuwa nikiuliza sana na ndiyo maana nikirudi pale kwenye takwimu kwa mfano Tarime Mjini sjataka kwenda hata huko

Susuni, Mwema na wapi, nilikuwa namwambia Mheshimiwa Waziri kila siku tangia Bunge la Kumi na Moja kuna kata sita hazina umeme akasema vinaisha *by phase* // lakini hata *phase* /// bado umeme haujafika. Kwa mfano Kata ya Nyandoto, Mitaa ya Masulule, Nyagesese, Nyasebe, Kemonge, Itinunu Nyatenene hakuna umeme. Kata ya Kenyemanyori tunahitaji umeme Kebaga, Nyamitembe, Chila, Longa na Mwibari. Kata ya Nkende tunahitaji umeme Iteve, Mtulu, Lomoli, Kitale, Kirumi, Nyamitebe na Kalamoloni. Kata ya Ketale tunahitaji umeme Ntabulo, Binagi, Wigoronto, Nyagesese, Malulu *Center*, Nyamahisana, Tebakiri na Nyamihobo na Kata ya Tura tunahitaji umeme Gimanya na Kikogoo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi nilikuwa nikongoelea hapa ndani tunavyoenda kuwekeza tuwekeza basi umeme uende kwenye taasisi; sekondari, vituo vya afya na zahanati ili mfano kwenye sekondari watoto wetu waweze kujisomea baada ya masomo ya kawaida. Mama anavyokwenda kujifungua pale kama hamna umeme wanatumia vitochi au vikarabai hivi hatutakiwa kuwa hapo. Tunapoenda kupeleka umeme *priority* namba moja iwe ni taasisi muhimu tuhakikishe kwamba zimefikiwa na umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kuwapongeza, wameainisha kwenye hotuba yao kwamba kuna viwanda hapa Tanzania vinazalisha vifaa ambavyo vinaenda kutumika kwenye miradi ya ujenzi ya umeme ambapo tumeweza ku-save zaidi ya shilingi bilioni 162, kwa hilo nawapongeza sana. Tuendelee kuwashamishwa watu wetu waweke ili kuzalisha hapa nchi kuliko kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko kwa mchango wako. Mheshimiwa Costantine Kanyasu utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa nafasi ambayo umenipatia.

Mheshimiwa Spika, nami naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanafanya na wanaendelea kufanya.

Mheshimiwa Spika, pale Geita Mjini miaka miwili iliyopita tulizindua ujenzi wa *substation* katika Kata ya Mtakuja ambapo mimi pia nilikuwepo na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake aliahidi baada ya miezi nane watu wa *GGM* wataanza kutumia umeme kutoka kwenye ile *substation*. *Substation* ile inatoa *megawatts* 98 na imekwishakamilika nadhani sasa karibu mwaka. Pia katika ahadi zake Mheshimiwa Waziri alisema kwamba Kata hiyo ambayo *substation* hiyo ipo ya Mtakuja ambayo ipo kilometra mbili tu kutoka makao makuu ya mji itapata umeme kutoka kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza leo mradi ule umekamilika, Kata ile ina vijiji 11 hakuna kijiji hata kimoja kimepata umeme. Sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri sijui ilikuwa sio sehemu ya *package* ya mradi huo, sijui kama mradi huo unaendelea, kwa sababu mpaka leo navyozungumza nashindwa kwenda kuzungumzia ahadi alizozitoa kwa wananchi wa Mtakuja kwa sababu mkandarasi keshandoka *site* na wananchi hawajapata umeme mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, kata katika Jimbo la Geita Mjini zimechelewa sana kupata umeme katika awamu zote tatu. Nimeingia kwenye Bunge hili nikakuta nchi nzima vijiji 2,000 ndiyo vina umeme leo tunazungumzia vijiji 10,000 lakini katika Jimbo la Geita Mjini kata sita hazijapata umeme mpaka leo. Ukiwafuata *TANESCO* wanakuambia huko ni *REA*, ukiwafuata *REA* wanakuambia huko ni *Peri-Urban* ukienda *Peri-Urban* wanakuambia hawana pesa, amekuja mkandarasi wa kwanza, wa pili sasa wa tatu. Wananchi wa Jimbo la Geita Mjini wanakusikiliza Mheshimiwa Waziri, Geita Mjini siyo Mjini pale tuna kata 14 na kata zingine zote ziko nje ya Geita Mjini wanataka kujua wanapata lini umeme; Kata za Shiloleli, Bulela, Ihanamilo, Nyanguku, Mgusu na Mtakuja

ambako kule kote watu wako wa kufanya *surveywamefanya* zaidi ya mwaka mmoja lakini umeme haujaenda.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi sijui inakuwaje Mheshimiwa Waziri alikuja siku moja akazindua umeme kwenye kijiji kimoja alipoondoka hakuna tena kwenye kata hiyo kijiji kingine kilichopata umeme leo mwaka mmoja na nusu. Sasa sielewi anapoondoka anasimamisha zoezi la usambazaji wa umeme mpaka arudi tena au inakuwaje?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa kampeni tumefanya zoezi zuri sana la kutoa umeme mjini kuupeleka Nyanguku na Nyanamilo, mwezi wa saba mpaka leo nguzo zimesimama hakuna kinachoendelea. Ukiwaliza *TANESCO* wanakuambia subiri *Peri-urban* inakuja. Kwa sababu ya muda Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha naomba awahakikishie wananchi wa Geita Mjini kata hizo nillozitaja wanapata lini umeme.

Mheshimiwa Spika, nilizungumzia hapa wakati nachangia kwenye Mpango inawezekana shida iko sehemu moja, leo hii pale pale mjini watu wamelipia umeme wana miezi saba hawajapata umeme. Wanalipia umeme palepale mjini wanasubiri miezi sasa nikasema inawezekana *centralization* yenu ya *supply* inachelewesha watu kupata umeme. Kwa nini msitafute mfumo mwингine wewe unazalisha umeme *running cost* zako ziko *constant* unahitaji wateja wengi uweze kupata faida inachukuaje miezi saba unafanya biashara hujamuungia mtu umeme na mteja yupo?

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri angalie vizuri watu wake wa *planning* na biashara kwa nini hawawezi kutafuta mbinu mbadala, unakaa na wateja 400 wamekulipa hauwaunganishi umeme kila siku unawaambia vifaa hakuna, vifaa hakuna wapi? Kama haiwezekani wewe *ku-centralize supply* tafuta watu ambao utakuwa na uhakika na *quality* za vifaa vyako ili mtu anapolipia leo kesho apate umeme. Haiwezekani wewe unazalisha umeme lakini wateja wapo halafu mtu amekulipa miezi sita yupo anasubiri, akienda hapa anaambiwa vifaa hakuna au hiki hakuna, kwa

nini wakati *source* zipo? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tazama vizuri hawa watu wako inawezekana kupata *source* za vifaa sehemu zingine kwa *quality* unayoitaka kama wanavyofanya watu wa idara zingine ukawenza ku-supply umeme bila kumchelewesha mteja kwa miezi mingi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nakushukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mbunge wa Geita. Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Nyamoga na Mheshimiwa Shigongo wajiaandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara hii ya Nishati ambayo kimsingi ni Wizara ya kazi, kimkakati na maendeleo na bajeti nzima *percent* 98 ni maendeleo tu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote kwenye Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanafanya pamoja na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ukiangalia jinsi ambavyo mambo yanakwenda sasa hivi kuhusu hii bidhaa ya umeme nchini utaona kwamba kuna tofauti kubwa sana. Kabla ya mwaka 2015 ukitaka kupata umeme ilikuwa ni kizungumkuti lakini siku hizi ukitaka umeme unafungiwa na unaelewa ufuate hatua gani ili uweze kupata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeza sana Waziri, naungana na ndugu yangu Mheshimiwa Elibariki kwa kweli Waziri Kalemani na Manaibu wake ni watu wastaarabu, wapole, unazungumza nao na wanaonyesha kabisa wana kiu ya kufikia malengo yao. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pia mafanikio kwenye Bwawa la Nyerere, nilikwenda kule mwaka juzi mwishoni nikiwa chini ya Wizara ya Maliasili na Kamati yetu kazi ambayo ilikuwa imefanyika ni kidogo sana. Sasa hivi bwawa limetengenezwa kwa kiwango cha *percent* 52, ni kazi kubwa napongeza sana Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba sasa nizungumzie kidogo habari ya jimbo langu kuhusu umeme wa *REA*. Kuna mafanikio makubwa sana *over all* ni *percent* 86 lakini ukija kwenye jimbo langu zipo *percent* 43 tu za kazi iliyofanyika. Kwa faida ya Wizara na Waziri naomba nitaje vijiji ambavyo viko gizani, jimbo upande wa Mashariki na Kusini liko gizani; Kata ya Kingori, Vijiji vya Muungano, Oldonyongilo, Ngonoheri, Mboleni, Ngosio, Nsengoni viko gizani. Kata ya Malula; Vijiji vya Kolila, Ndumangeni, Malula, Ngajisosia, viko gizani. Kata ya Maruwango; Vijiji vya Mowaro, Maruwango yenye, Mbasenyi, Nombele, Songambele viko gizani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kata nyingine ni Kata ya Ngarinanyuki iko gizani kabisa, Olukung'wado pale mjini wana umeme kidogo sana. Kata ya Uwilo; Kijiji cha Kimosonu wako gizani, Ngwandua Kijiji cha Nkoavele wako gizani. Kata ya Songolo; Vijiji vya Ulishe, Songoro, Malula, Kilinga wako gizani. Kata ya Kikatiti; Sakila Juu, Sakila Chini, Njeku, Nashori Kikatiti wako gizani. Kata ya Maroroni; Migadini, Kwaugoro, Samaria wako gizani. Kata ya Ngwalusambu; Kijiji cha Mfuloni, Ngwalusambu yenye, Kimundo wako gizani. Kata ya Maji ya Chai; Vijiji vya Maji ya Chai, Kitefu, Lerai, Ngurudoto wapo gizani. Kata ya Mbuguni; Kambi ya Tanga, Kikileto, Migungani wako gizani. Kata ya Shabarahi; Bulka na Karangai wako gizani. Kata ya Kwikwe; Luwainyi na Malala wako gizani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi pamoja na kwamba *over all* kazi iliyofanyika ni nzuri lakini kwa kweli jimboni kwangu hali si nzuri. Hivi vijiji viko karibu karibu kama Wizara ingejipanga vizuri ile kazi isingekuwa ngumu sana. Nadhani kuliwa kuna tatizo kidogo wakati wa kuanza kazi hii nakumbuka walileta

nguzo sehemu zingine wakachimba mashimo wakayaacha wazi, wakaacha nguzo zikaendelea kuoza pale, kuna hadithi nyingi ambazo kwa kweli hazifurahishi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu hii bei ya kuunganisha umeme wa *REA* Sh.27,000, bado ni kizungumkuti. Kuna watu ambao walikwenda wakajaza fomu wakitegemea kwamba wanaunganishiwa kwa Mpango wa *REA* wakapelekewa bili kubwa badala ya Sh.27,000 anapelekewa bili ya Sh.337,000, kiwango ambacho kimkuwa kigumu sana kwa wao kuweza kufungiwa umeme.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, naskuhukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Vwawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyamoga, Mheshimiwa Shigongo ajiandae, na Mheshimiwa Hussein Amar atafuatia.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, naomba niipongeze sana Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inashughulikia masuala ya nishati ambayo ni muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu. Naamini kwa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo wameianzisha, miradi kama ya *SGR*, Nyerere, Bomba na kadhalika, kwa kweli wakiisimamia vizuri itatoa mchango mkubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizipongeze taasisi ambazo ziko kwenye Wizara hii zinafanya kazi nzuri sana. Ni kwa mara ya kwanza nimesikia *TANESCO* wamepata faida kubwa, kwa kweli nawapongeza sana, nina imani kazi hii itaendelea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunahitaji nishati na Serikali ya Awamu ya Sita imetenga fedha zaidi ya shilingi trilioni 2.3 ili mambo kadhaa yajitokeze katika nchi hii. Sasa kwa sababu ya muda nitasema mambo makubwa matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, nishati itasaidia kuhakikisha kwamba kunakuwa na maisha bora kwa Watanzania wote. Watanzania wanaoishi mijini na vijijini, wanahitaji umeme wa uhakika, wanahitaji gesi, mafuta na kadhalika. Kwa hiyo, nina imani fedha hizi ambazo Serikali imewekeza zitachochea sana kuhakikisha maisha ya Watanzania yanaimarika na umaskini unapungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, fedha hizi zilizotengwa tunategemea zitatengeneza ajira nyingi kwa Watanzania ambalo limekuwa ni tatizo la muda mrefu. Ajira zitakazotengenezwa katika bomba la mafuta, gesi, mafuta na vituo vyta mafuta, zitawasakiya Watanzania. Nina uhakika kwamba iwapo vitasimamiwa vizuri, vitasakiya sana Watanzania kule vijijini kuanzisha biashara, kufanya kila aina ya kazi kwa sababu hivi vitu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, nishati ya uhakika itasaidia na kuhakikisha tunajenga viwanda vitakavyozalisha bidhaa mbalimbali za Tanzania. Hatuwezi kujenga viwanda imara kama nishati itakuwa siyo ya uhakika au kama tutakuwa na umeme unaokatikakatika. Kwa mfano, kama sasa hivi katika Mkoa wa Songwe, kuna tatizo kubwa sana la kukatika kwa umeme kila mahali. Unaweza ukakatika zaidi ya mara kumi kwa siku na kuna maeneo mengi hayana umeme. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo wameifanya *REA* na ambayo Mheshimiwa Waziri ameifanya lakini viro vijiji karibu 31 kwenye Jimbo la Vwawa havina umeme hadi sasa hivi. Bado kuna mitaa kadhaa haina umeme, Mitaa kwa mfano Isangu, ni kijiji lakini hakina umeme; Mitaa ya Rondoni na Shanko, kote hawana umeme. Vijiji kama Idunda, Ipyana, Iromba, Namwangwa, Nyimbili, Hantesya, Izumbi, Sakamwera, Mponera, Ipunga, Ipapa, Mpanda, Masangura, Ihoa, Welu II, Idibira, Rusungo, Namlonga, Maroro, Isararo, Sakamwera, Mantengu, Chizumbi, Rudewa, Msambavwanu, Kilimampimbi na Kata nzima ya Nyimbili; vyote havina umeme hadi sasa. Pamoja na kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Waziri, naomba vijiji hivi vyote vipatiwe umeme kama alivyosema na naamini tutakuwa tumefanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema nguzo hazilipiwi na wananchi watalipa Sh.27,000 wale ambao mitaa yao inafanana na vijiji. Mimi katika Jimbo la Vwawa bado ni vijiji na ndiyo maana tumehindwa kupata sifa ya kuwa Manispaa kwa sababu maeneo mengi bado ni vijiji lakini mpaka leo hii ukienda *TANESCO* wanakwambia lazima ulipie nyaya na nguzo na wanakwambia kwamba sisi hatuhusiani na *REA* labda ukitaka hivyo nenda *REA*, *REA* wanakwambia huko *TANESCO*.

Naomba masuala haya yaangalie vizuri toeni waraka wa kuwaelekeza watendaji wa *TANESCO* ili wazingatie maagizo ya Wizara. Ikitokea Wizara mnatoa maagizo na *TANESCO* wanasesma sisi hatutekelezi, hatuna waraka, kwa kweli mnaleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Huko ni Vwawa, Mheshimiwa Waziri una kazi maana mwakani ukija vijiji hivyo bado, navyomuona kama mwakani atakamata shilingi huyu. (*Kicheko/Makofi*)

Tunaendelea na nilikutaja Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Shigongo ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kupongeza kazi nzuri ambayo inafanyika hasa ya usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Katika jumbo langu ni kweli kumekuwa na utekelezaji mzuri sana kwenye awamu hizo zilizopita hadi maeneo ambayo kwa kweli ni ya mbali sana na kwa sababu eneo langu ni la milima, Kata kama zile za Kimala, Idete na Masisiwe, nyaya na mita zimefungwa lakini umeme bado haujawashwa. Nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri baada tu ya kumaliza bajeti hii twende naye kwa sababu wakimuona najua kabisa umeme utawaka kwenye kata zile. Kwa hiyo, naamini kwamba yuko tayari na tutaongozana na kwa sababu nimeona dalili kwamba baada tu ya kuwa nimeongeaongea watakuwa wanaendelea kuhakikisha kwamba wanakamilisha wakijua ziara yako inakaribia. Kwa hiyo, Kata hizi za Kimala, Idete na Masisiwe tunamsubiri kwa hamu ili umeme uweze kuwaka.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna kata tatu nzima ambazo hazijafikiwa na umeme. Kuna Kata nzima za Nyanzwa, Ukwega na Udekwa. Kwa mfano, Kata ya Ukwega kwenye Kijiji kile cha Ipalamwa kuna kituo cha afya kimejengwa kwa hisani lakini hakiwezi kufanya upasuaji hata kama wana vifaa kwa sababu hakuna umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi niliyoyataja haya tayari kuna kilimo kikubwa sana cha parachichi na watu wameshaanza kujenga majengo kwa ajili ya kuhifadhi mazao yale ambayo yanahitaji umeme. Kwa hiyo, naamini kwamba atakapokuwa ameshafikisha umeme kule basi shughuli za kiuchumi zitaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri nimeshaongea naye pamoja na Naibu

Waziri; pale kwenye Kijiji cha Kipaduka, Kata ya Wambingeto ambapo kulikuwa na mradi ulipeleka pale transforma, nguzo zipo, transforma ile iko kwenye ofisi za kijiji kwa muda mrefu na tatizo ni kwamba kuna afisa mmoja huko hajatoa kibali ili REA iweze kufanya kazi ile. Wale watu wa Kipaduka wamekaa na zile transforma kwenye ofisi ya kijiji muda mrefu mno, hawawezi hata kujua wafanye nini basi naomba yule anayetoa kibali kama yuko hapa kwa sababu najua maafisa wenu wanahudhuria akumbuke kutoa hicho kibali ili pale Kipaduka hilo tatizo liweze kuisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutaja pia Kata ya Ilole, kwenye Kijiji hichohicho cha Ilole kuna tatizo kwamba umeme haujafika na hakimo kwenye orodha ya vijiji ambavyo havijapatiwa umeme. Kwa hiyo, naomba nacho kiongezwe ili vijiji vile ambavyo havijapata umeme viweze kufika 22 vikiwa ni pamoja na Vlijji vingine kama Muhanga, Idunda na Ibofwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia suala la hifadhi ya mazingira, hasa kwa sababu Jimbo la Kilolo ni jimbo ambalo ndilo linalotoa maji mengi yanayotiririka kwa ajili ya Bwawa la Mtera.

Naomba kutoa angalizo hili kwa sababu tunajua kwamba umeme wa maji bila kuhifadhi haya mazingira inawezekana ikafika wakati tukakosa maji. Kwa sababu najua Waziri anayehusika na mambo ya mazingira yuko hapa pia, napenda kuhimiza kwamba ni suala la kuliangalia kwa sababu katika maeneo haya kuna kilimo kinaendelea kama tusipopanga vizuri na tukaweka hifadhi ya mazingira vizuri, basi upo uwezekano baadaye kuja kukosa maji. Hii inategemea na ufadhilli wa miradi iliyomo pembezoni mwa mito na hasa vile vijiji ambavyo maji yanatiririka kuelekea kwenye hilo eneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo. Sasa ni Mheshimiwa Eric Shigongo na atafuatiwa na Mheshimiwa Nassor Hussein Amar.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa sababu ya ufinyu wa muda, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia moja kwa moja mambo yanayohusu jimbo langu. Nimeshazungumza mara kwa mara na Mheshimiwa Waziri kuhusu tatizo kwenye Visiwa vya Zilagula pamoja na Maisome ambako wananchi wale wanategemea umeme kutoka kwa watu binafsi. Hivi ninavyozungumza wanunu *unit* moja kwa Sh.2,400. Huyu ni mwananchi wa kawaida, maskini, nimeshazungumza na Mheshimiwa Waziri naomba atakapokuwa anafunga hotuba yake hapa awaeleze wale wanaitwa Jumeme na *PowerGen*, alishatoa maelekezo wauze umeme kwa Sh.100 lakini baada tu ya Hayati kupumzika wamepandisha bei. Kuna maneno wanayasema kwamba aliyeikuwa anatusumbua ameondoka, hawajui kama mama Samia ni moto wa kuotea mbali. Kwa hiyo, mimi nina nia ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kama hatakuwa na maelezo ya kutosheleza kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nizungumzie maeneo ambayo bado kuna matatizo makubwa sana ya umeme kwenye jimbo langu katika Kijiji cha Itabagumba, Makafunzo, Bupandwa, Nyehunge, Kanyala, bado kuna shida kubwa sana ya umeme. Umeme uko kwenye *center* tu, ukizama huko ndani kuna nguzo na maeneo mengine hakuna nyaya. *REA* Mkurugenzi yuko hapa, Mheshimiwa Waziri na Naibu mko hapa mhakikishe sasa umeme unakwenda moja kwa moja mpaka kwenye maeneo ya ndani kabisa ili lawama hizi ziweze kupungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee kuhusu suala la nishati, kuna uhusiano mkubwa sana kati ya nishati na maendeleo ya watu. Taasisi moja inaitwa *MD/ilifanya* utafiti

wakasema unapoongeza matumizi ya umeme kwa asilimia moja, unaongeza pato la Taifa kwa asilimia 1.72. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana yangu hapa ni nini? Naomba kwanza nipongeze sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba umeme unapatikana kwa asilimia kubwa. Hii imeweza pato la nchi yetu kukua. Naomba kabisa tuendelee kutafuta nishati kwa gharama yoyote ili nchi yetu iweze kuwa *Africa Power House*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili likifanyika, hata kama tunapingwa, mimi nakumbuka wakati tunaanza ujenzi wa Bwawa la Nyerere tulipingwa, walisema kwamba kuna masuala ya mazingira. Namshukuru sana Hayati, namshukuru mama Samia, walisema hata kama kuna *issue* ya mazingira bwawa litajengwa na bwawa limejengwa. Jana nimesikla wameanza tena Wazungu kusema bomba la mafuta lina *issue* ya mazingira kwa hiyo hatutapewa mkopo; tusiwasikilize Wazungu, wanajua kwamba tukishakuwa na nishati tutakuwa na nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa, Mwalimu J. K. Nyerere alijua kwamba ili tukue kiuchumi tunahitaji nishati. Rais wetu, Hayati, alikuja hapa ametekeleza ndoto ya Baba yetu wa Taifa. Kweli tutakuwa na umeme wa kutosha katika Taifa letu na umeme utakuwa ni wa bei rahisi kuliko wakati mwingine wowote, wawekezaji watakuja na biashara zitaongezeka. Unapoongeza umeme, unaongeza *production* na *GDP* ya Taifa lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge tulioko hapa leo, tuna bahati ya kuwa ndani ya Bunge hili, wazee wetu waliotangulia wamefanya maamuzi mazuri sana sisi leo ni Taifa bora na sisi tulipo hapa ndani tufanye maamuzi bora kwa ajili ya watoto wetu watakaokuja baada ya sisi. Nataka Bunge la Kumi na Mbili likumbukwe kama Bunge liliyahakikisha Tanzania inakuwa *Africa Power House* kwa kuwa na *energy* ya kutosha ili tuweze kukua na uwezo huo tunao. *I don't care where the source is,*

*as long as ni power, leta power, hata kama ni nuclear power leta nuclear power ili tuweze kuwa na nguvu kama Taifa. Tukiwa na nishati hakuna atakayetutisha, uchumi wetu utakuwa. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu wake na moyo wa kujituma. Nampongeza sana Naibu wake, *TANESCO* na *REA*. Ninachowaomba sasa wakachape kazi zaidi ili Taifa letu liweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kama hakutakuwa na majibu ya suala la umeme *unit* moja Sh.2,400 nitashikilia shilingi. Naomba niishie hapo, Mungu ibariki Tanzania, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Eric Shigongo. Leo *galleries* zangu zimejaa wasomi wa vyuo vikuu. Niwaambie kwamba Mheshimiwa Eric Shigongo alimaliza darasa la saba enzi hizo akaendelea na kazi zake hapo katikati, baadaye kazi zake zile zikawa *rated* zikawa ni *equivalence* ya kumruhusu ku-*enroll* kwa *degree* ya kwanza ya chuo kikuu bila kupitia hii sekondari ya *O-Level* na *A-Level* kama ilivyo. Alipo-*graduate* chuo kikuu alipata zawadi ya *best academic student award* katika *degree programme* aliyokuwa anaifanya akiwa ni mwanafunzi wa kwanza darasani. Hongera sana Mheshimiwa Shigongo. Kwa hiyo, mambo yote yanawezekana. (Makof)

Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Genzabuke na Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Wizara hii; Katibu pamoja na watendaji wao wote kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kuzifanya. Pia napenda kuunga mkono hoja kutokana na hizo dakika tano kuwa ni chache sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba umeme ni maendeleo lakini pia ni huduma. Lengo la Serikali ni kusambaza umeme vijiji zikiwemo na taasisi za umma kama vile zahanati, vituo vya afya pamoja na shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu la Nyang'hwale nina vijiji 62, vijiji ambavyo tayari vimeshapitiwa na umeme mpaka sasa hivi ni vijiji 44 bado vijiji 18. Katika vijiji 44, nakuomba Mheshimiwa Waziri ongea na Waziri wa TAMISEMI ili sasa Wakurugenzi waweze kupewa maelekezo wa nchi nzima wakiwemo wa Nyang'hwale ili waweze kulipia zile gharama za Sh.27,000 ili taasisi zetu; zahanati, shule za msingi na sekondari ziweze kulipiwa na kupewa huduma ya umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la pili kwamba Wilaya ya Nyang'hwale ina wachimbaji lakini pia umeme tunauhitaji sana kwenye maeneo ya wachimbaji. Maeneo hayo ni kama vile Igalula, Isekeli, Ifugale na maeneo mengine, waweze kuvutiwa umeme kule ili waweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, shida kubwa iliyoko jimboni na maeneo mengine wamezungumza Waheshimiwa Wabunge, jambo la kukatikakatika kwa umeme linawatia hasara sana wananchi. Umeme kwa Jimbo la Nyang'hwale unakatika zaidi ya mara tatu au nne kutwa nzima. Vifaa vya umeme vinaharibika lakini pia bidhaa zilizomo ndani ya *freezer*, vinaharibika. Tatizo ni nini? Kwa sababu umeme unakatika unatutia hasara sana wananchi hasa tunaotumia umeme kwenye majumba yetu na shughuli zetu mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimepewa jina la mkandarasi wangu atakayeenda kusambaza umeme katika vile vijiji 18. Cha kushangaza na kusikitisha ni kwamba nimeongea naye jana akasema mpaka sasa hivi hajapata fedha kutoka *CRDB*, tatizo ni nini? Mheshimiwa Waziri lichukue jambo hili ongea naye kujua kwa nini hajapewa fedha mpaka sasa hivi ili aweze kwenda *site*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, gharama ya kuunganishiwa umeme ni Sh.27,000, lakini wananchi wetu wapo maeneo mbalimbali, unakuta kutoka eneo moja kwenda eneo lingine ni zaidi ya mita 500 mpaka mita 1000, je, huyu aliyeko kwenye mita 500 mpaka mita 1000 gharama ni hiyohiyo Sh.27,000, nguzo na nyaya hazimhusu? Kwa hiyo, pamekuwa na changamoto nyingi, kuna wananchi wetu wengine wamelipia muda sana zaidi ya miezi mitano mpaka mwaka mmoja hajavutiwa umeme anaambiwa tatizo ni nguzo, hasa tuambieni Sh.27,000 ukiwa ndani ya mita ngapi unafungiwa umeme kwa haraka? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi sina mchango mkubwa zaidi yangu ni hayo, lakini nampongeza sana Mheshimwia Waziri kwa kazi nzuri na Naibu Waziri na Katibu kazi zao ni nzuri na wanachapa kazi. Mheshimiwa Waziri yachukue haya ambayo nimeyachangia kwenye upande wa Jimbo langu la Nyang'wale.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Genzabuke atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa naomba niunge mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali ya CCM inayoongozwa na Jemedari Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu kwa kufanikisha mkopo wenyewe masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika. Tumeahidiwa dola za kimarekani 140 sawa na shilingi bilioni 324,000.4 kwa ajili ya ya utekelezaji wa mradi muhimu sana wa maji Mto Malagarasi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi huu utaweza kuwasaidia sana wananchi wa Mkoa wa Kigoma na mikoa jirani kwa sababu mradi wa umeme wa maji gharama zake ni ndogo kuliko za mafuta ambapo Mkoa wa Kigoma tumekuwa tukitumia *generator* kwa muda mrefu. Kupitia mradi huu ambapo tutakuwa tunatumia maji tutaweza kupata umeme wa uhakika na vilevile utakuwa ndio ukombozi wa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na mikoa ya jirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kuipongeza Serikali kwa miradi ya *REA* na kwa kutekeleza llani ya CCM kwa ahadi iliyotoa kwamba itaweza kuunganisha vijiji vyote kuititia miradi ya *REA*, naishukuru Serikali ya CCM. Sitaweza kuvitaja vijiji kwa sababu mimi ni Mbunge wa Mkoa nikianza kutaja vijiji vyote siwezi nikavimaliza, naomba vijiji vile ambavyo havijapatiwa umeme Serikali iweze kuwasimamia wakandarasi ili vijiji vile ambavyo havijapatiwa umeme viweze kupatiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kwa sababu kwa muda mrefu tumekuwa tukishauri kuhusu hifadhi ya mafuta ya dharura. Kwa kuwa na hifadhi hii nchi itaweza kufanya biashara na nchi zinazotuzunguka, kwa kuwa mafuta mengi yanayoingia nchini yanaenda nchi za nje. Kwa hiyo, nashauri Serikali iweze kuweka vivutio na kushauri wawekezaji wale wenyewe maghala waweze kujenga maghala mengine kusudi mafuta yaye yanahifadhiwa na hao wafanyabiashara na hatimaye mafuta yaye yanaweza kuuzwa nchi za nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba Serikali itusaidie Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu kwa

sababu idadi ya watu imeongezeka na kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu mahitaji ya kupata umeme nayo yameongezeka. Naomba Serikali ipeleke nyaya za kutosha ili wananchi waweze kupatiwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephine Gezabuke. Nilimtaja Mheshimiwa Stanslaus Nyongo na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na Mheshimiwa Ussi Pondeza, ajiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Ni Mheshimiwa Stanslaus Mabula siyo Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na angekuwepo ningemkalisha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa sababu ya muda na mimi nianze kwa kuishukuru sana Wizara ya Nishati, nimshukuru Waziri, Naibu Waziri na Wakurugenzi wake wote ambao wanashughulika kuhakikisha Watanzania wanapata umeme wa kutosha. Ukweli ni kwamba *TANESCO* pamoja na Taasisi hii wamefanya kazi kubwa sana. Ukikumbuka toka mpango huu uanze mwaka 2014 Awamu ya Tano ilipoingia, Awamu ya Sita leo tunaendelea nayo kumekuwa na jitihada kubwa sana na wananchi wetu mahitaji yao mengi ukitoa maji, umeme na barabara na afya jambo kubwa sana wanatutazama namna gani tunapata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niongelee mambo mawili tu, suala la usambazaji wa umeme, ukweli ni kwamba kazi kubwa sana imefanywa. Ukitazama scope ya kazi ambazo wanapewa wakandarasi zinakuwa ni ndogo sana kulingana na mahitaji ya maeneo husika. Kwa mfano, ukiangalia Jimbo la Nyamagana tumebahatika kupata

miradi ya *REA* na sababu na sifa tulikuwa nazo kwamba tunayo maeneo kwenye mitaa yana sifa sawa na vijiji.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yalistahili na unapopata kata kwa mfano ina mitaa mitano ambayo ipo eneo moja ina zaidi ya kilometra 100 kwa mfano au 80 inapata *LV* kilometra zisizozidi 20 peke yake ni kuendelea kuongeza lawama kwenye Serikali. Mheshimiwa Waziri nikucombe hata tunapofanya miradi ya *densification* tujitahidi sana kwenda mbaliya pale tulipoanza, kama tulitoa *LV* kilometra 12 tusirejee tena kutoa chini ya 12 twende mbele zaidi ikiwezekana 20 na kadhalika. Sisi kwa Nyamagana nataka nikuhakikishie kwamba Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa sana na hii kazi aliyofanya imewasaidia wananchi wengi wa Jimbo la Nyamagana kupata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nlongelee miradi ya *Peri Urban* itakuwa mkombozi na kulisaidia sana Shirika la *TANESCO*. Kwa nini *Peri Urban* ifanyike kwa kasi na jana nimeona Waziri ametoa orodha ya wakandarasi wa *REA* naomba na orodha ya wakandarasi wa *Peri Urban* tuipate ili tujue *scope* yetu imekaaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mwanza peke yake ukichukua llemela na Nyamagana Mheshimiwa Waziri nataka nikuhakikishie ukipeleka leo umeme wa *Peri Urban* malipo ya watu wake na *unit* wanazotumia kwa siku mpaka mwezi siyo sawa na maeneo mengine unaweza kuyalingalisha. Hatukatai umeme usiende kila sehemu lakini Waziri atakubaliana nami kuna sehemu unafunga *transformer* leo ya kuhudumia watu 50 miaka minne umewaunganisha watu wasiozidi kumi peke yake, hii ni hasara kwa *TANESCO* na lazima muangalie namna bora ya kuwasaidia mnapoweka miradi ya uzalishaji kwa haraka inasaidia sana maeneo yetu mengi.

Mheshimiwa Spika, ukienda Kata za Igoma, Kishiri, Lwanima, Buhongwa, Nyangu, Nyakabwe Mheshimiwa Waziri alitusaidia alipokua na Waziri Mkuu, lakini ukweli ni kwamba tatizo bado ni kubwa na eneo liliopata ni karibia kilometra 12

peke yake eneo liliowazi zaidi ya kilometra 32. Bado ni changamoto na wananchi wanalamika wanaona kama tumewatenga na tumewabagua lakini ukweli ni kwamba mahitaji ni makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu hata ukienda ilemela pale kwa mama yangu Mheshimiwa Angeline kule kwenye Kisiwa cha Bezi bado kuna changamoto kubwa hakuna umeme na uliopo ule wa Jumeme ni kama matatizo yaliyopo hapa kwa ndugu yangu Mheshimiwa Shigongo. Mheshimiwa Waziri umefanya kazi nzuri na kubwa sukuma hapa ulipobakisha, *umaligije ikazi ishile na tulole yingi lulu ihaha*, mambo yanakuwa yameenda hivyo vizuri au siyo bwana, lakini ukweli ni kwamba kazi kubwa mnaifanya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula *ng'welage geke.* (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, *ee welelagwa gete, welelagwa.* (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, kwenye hii miji tunayoitaja hata hasa kwenye majiji haya makubwa ni hizi ni fedha tumeziacha. Ukienda hata kwa Naibu Spika kule kwenye Kata za Iziwa, Itengano, Iduda hata Itende na kwenyewe ukifunga umeme wa *Peri Urban* una uwezo wa kuingiza hela nyingi sana Mheshimiwa Waziri na ikasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa sababu ya muda kumekuwa na mjadala mkubwa sana hapa ambao unaendelea...

## TAARIFA

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa hiyo inatoka wapi endelea na taarifa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumwambia mchangiaji Mheshimiwa Mabula kwamba hata maeneo ya Kibaigwa, Kongwa na Sengerema Mjini yote yanahitaji umeme. Ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Hata kule llemela kwa Mheshimiwa Angeline Mabula pia, endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataja miradi ya *Peri Urban* ambayo watu wa majiji tumeomba ili ije kutusaidia kupunguza mzigo mzito. Mwananchi wa kawaida kabisa anayeishi kwenye majiji ili aunganishiwe umeme anahitaji shilingi 512,000 au shilingi 321,000 ili aweze kufikishiwa umeme kwenye eneo lake. Siyo wote waliopo mjini wana uwezo wa kumudu gharama hiyo ndiyo maana tunaomba watu wa *Peri Urban*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kumekuwa na mjadala mrefu sana hapa siku mbili hizi zilizopita na uliuweka vizuri juu ya *TBS* kupewa zoezi la kuweka vinasaba kwenye mafuta. Nafahamu jana umetoa maelekezo mazuri sana na naomba wakati wanaandaa sheria tufikirie nje ya *box*, pale bandarini kuna watu wanaitwa Wakala wa Vipimo na Mizani wajibu na shughuli yao kila meli inapotoka na kuingia wanakwenda kupima idadi ya mafuta yaliyokuja, ikifika nje wanakwenda kupima.

Tunapozungumzia kupokea lita karibia laki tano na hao wote ni taasisi zilizoko chini ya Serikali kwa nini tusifikirie vizuri zaidi na Mheshimiwa Waziri hili wakalichakate, tunaweza kuwapa watu wa Wakala wa Vipimo na Mizani, watu wa *TBS* wakabaki na jukumu lao la kuhakiki ubora wa mali ambayo inaingia nchini kwetu, kwa sababu wamekuwa *accredited* na dunia wamejulikana na wanatambulika kwa kazi nzuri. Kwa hivyo, nataka niliache kwako, sheria zinapokuja tuzitafakari na tuone namna ya kuziweka vizuri ili tujue sehemu ya kutokea. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja asilimia mia. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabula, Mbunge wa Nyamagana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla nilikutaja na Mheshimiwa Ussi utafuata.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii ya kuchangia asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Kalemani na Naibu wake pamoja na Wizara kwa ujumla wake kwa kazi nzuri wanayofanya kwenye Wizara yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa na sehemu mbili, sehemu ya kwanza napenda kuchangia kuhusu uchumi wa gesi kwa sababu imekuwa bahati mbaya sana hatuzungumzii tena uchumi wa gesi katika nchi yet una nilidhani kwamba uchumi wa gesi pengine ungekuwa neema. Miaka ya 2010 wakati naingia hapa Bungeni tulizingumza sana kuhusu uchumi wa gesi.

Mheshimiwa Spika, kipindi kile matarajio kwenye uchumi huu wa gesi yalikuwa bei zingefika takribani dola 16 kufikia mwaka 2020 ilikuwa ni kipindi cha miaka kumi, lakini leo tunavyozungumza hapa bahati mbaya sana bei zimeshuka badala ya kwenda mbele kwenye hiyo dola 16 tuliyokuwa tunafikiria *per one British Thermal Unit*, leo hii bei zimeshuka mpaka dola nane. Ukitazama bei ya gesi kwenye soko la Japan, Korea ya Kusini na Ulaya unaona bei zinashuka tu badala ya kupanda na hapo nimeangalia takwimu za kabla ya mwaka 2020 ambapo hapa duniani tulikuwa hatujakumbwa na baa la *COVID 19* maana yake tungetarajia pengine bei zingekuwa zinapanda badala ya kushuka. Sasa ukiweka na *impact* ya *COVID 19* maana yake bei zitazidi kushuka.

Mheshimiwa Spika, lakini nimetazama makadirio ya bei kwa miaka 15 inayokuja yatakuwaje. Miaka 15 inayokuja bei ya milimita moja ya *BTU* ya gesi itakuwa dola 14 tu. Hii kwa sisi wana mazingira inatupa mtazamo tofauti kwamba pengine kizazi kinachokuja cha watoto na wajukuu zetu hakitozungumza aina ya nishati ambazo tunazitungumza leo, kwa sababu tungetarajia pengine gesi ingezungumzwa miaka kumi na tano, ishirini ijayo kama ndiyo *source* pekee ya *energy* lakini bahati mbaya haitokuwa hivyo. Kwa hivyo, sisi kwa bahati mbaya sana tusipoitumia ipasavyo gesi yetu leo, hii *resource* ya gesi tuliyoiopata leo itapotea bure na haitokuja kuwa na faida yoyote ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa kutoa ushauri kwa Serikali kwamba tufikirie kwa namna yoyote ile kuanza kuitumia gesi tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu leo badala ya kudhani kwamba tunaweza tukafaidika sana huko mbele kuliko ilivyo sasa. Hii ni kwa sababu hata yale matarajio tuliyokuwa nayo miaka kumi na moja iliyopita hayakuwa. Kwa hivyo, tunakoenda huko mbele tunaweza tukajikuta hatupati faida yoyote kutokana na hii gesi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba tutazame zaidi faida tutakayoipata kutokana na uwekezaji kwenye sekta ya gesi kwa kutazama zaidi *value chain impact* ya gesi kwenye uchumi, lakini pia kwa kutazama zaidi *local content* kwamba tunafaidikaje, wananchi wanafaidikaje kwa uwepo wa uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya gesi kuliko kuwaza zaidi kupata mapato ama mgao kutoka kwenye ile *actual gesi inayopatikana*.

Mheshimiwa Spika, miaka kumi na moja iliyopita tuliouwepo hapa Bungeni tuliona kilichotokea na pengine miaka kumi na moja inayokuja siku za mbele tutajaliwa kuwepo wengine bado wadogo tu, tutaweza kuyaona haya na tutakumbushana hapa ndani kwamba wakati huo uchumi wa gesi hautokuwa na maana yoyote ile kama tusipoamua leo *ku-tap into the potential that the gas economy is going to bring to our country* na badala yake tukawaza zaidi mapato. Nalisema hili kutokana na sheria tulizozitunga miaka

miwili, mitatu iliyopita hapo ambazo zinazidi kuweka ugumu kwenye majadiliano ya uwekezaji kwenye sekta ya gesi badala ya kuzitazama zile *PSA* kibashara zaidi, kuzitazama kwa mawanda mapana zaidi ya *impact* ya gesi kwenye *value chain* ya uchumi wetu, kwenye *local content* ya uchumi wetu tutajikuta tunapitwa na wakati. Hakuna uwekezaji utakaotokea na hatutokuja kupata faida ya hii gesi ambayo tumejaliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kulizungumza hilo, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani, miezi miwili iliyopita alikuja pale Jimboni kwetu Nzega Vijiji na akatuzindulia mradi katika Kata ya Isanzu wa kuweka umeme vijiji. Bahati mbaya sana alisema baada ya siku kumi umeme ungewaka leo imepita miezi miwili umeme haujawaka. Kwa hiyo, namuomba ahadi aliyoitoa kwa wananchi wale itekelezwe na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na Kijiji cha Isanzu kuna Kata nyingine kama za Tongi, Mizibaziba bado hazijawa na umeme na zote hizi walishafanya tafiti na zinahitaji kupata umeme.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla. Mheshimiwa Ussi Pondeza atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi niwe mionganini wa wachangiaji wa hotuba hii nzuri ya Wizara ya Nishati ambayo kusema kweli inafanya vizuri. Pia nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake, pamoja na

Naibu Waziri lakini na watendaji wote wa *TANESCO* kijumla wao wanafanya kazi moja nzuri sana ambayo wote tunaikubali. Kiukweli ni wizara ambayo kwa kiasi kikubwa imetutoa tongo machoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nina jambo moja ambalo nataka nilielezee au nimpe ujumbe Mheshimiwa Waziri. Kuna tatizo ambalo lipo muda mrefu baina ya *TANESCO* na *ZECO* kuhusiana na bei ya umeme. Mimi ni mjambe wa Kamati na mara nyingi nimekuwa nikilisema hili lakini utaratibu wake au hatua zake zinavyochukuliwa zinachukua muda kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo nimeamua kulisema hapa kama jambo mahsus, ambalo nataka niambie Serikali yangu na Mheshimiwa Waziri, tatizo ambalo lipo hapa *ZECO* wanauziwa umeme na *TANESCO* kwa bei ya Sh.160.4 kwa KVmoja. Hata hivyo, kutokana na uchumi wa Zanzibar, *ZECO* wanasema hawawezi kununua kwa bei hiyo, wana uwezo wa kununua KV moja kwa Sh.130. Hili suala limekuwa linakaliwa vikao muda mrefu bila kupata majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona mimi mpaka nikaamua kulizungumzia hapa, kama mtakumbuka ndani ya miaka miwili, mitatu nyuma kuna jambo lilikuwa kubwa zaidi katika mambo ya umeme baina ya *ZECO* na *TANESCO*. Hayati Rais aliyeppita wa Awamu ya Tano, Dkt. Joseph John Pombe Magufuli aliweza kutufutia Zanzibar deni la shilingi bilioni 22 kitu ambacho leo ukiwaauliza Wazanzibar mnakumbuka vipi Dkt. John Pombe Magufuli basi moja ya jambo ambalo Wazanzibar wataendelea kumkumbuka ni hili la kutufutia deni. Leo hii linakuja jambo lingine dogo hili la bei, kwa nini Waziri usiwaambie watendaji wako wakakaa na watendaji wa kule wakaangalia jinsi ya kulimaliza mapema suala hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, deni lile lilikuwepo mwanzo ambalo lilikuwa linaleta zogo na tafrani humu ndani ya Bunge, kama unakumbuka *TANESCO* wakija kwenye Kamati yetu tukiwaauliza mna madeni mangapi wanasema *ZECO* tunaidai

shilingi bilioni 132; *ZECO* ukiwaliza wanasema sisi tunadaiwa shilingi bilioni 22 ambazo Hayati Dkt. John Joseph Magufuli alizifuta. Hii ni kwa sababu *ZECO* walifika mahali wakawa wanalipa *current bill* tu lakini hawalipi *VAT* mwisho wa siku *TANESCO* wanaandika *VAT* pembedni, hapa tunarudi kulekule. *ZECO* wanasema tunalipa shilingi 130, *TANESCO* wanasema shilingi 160.4 baada ya miezi sita na miaka miwili mbele *TANESCO* watasema wanaidai *ZECO* shilingi bilioni 54 na *ZECO* watasema sisi tunadaiwa shilingi bilioni 12. Hili sio jambo zuri na uwezo wa kulitatua Waziri wa Nishati wa Tanzania Bara Mheshimiwa Dkt. Benard Kalemani anao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine zuri ambalo namuamini Waziri, miradi mikubwa na mizuri ya kimkakati ambayo tunaendelea kuisimamia sisi kama wanakamatilakini kwa miongozo yake mambo yanaenda vizuri nashangaa jambo hili dogo linachukua muda mrefu. Kuna Bodi nzuri ya Mzee Kyaruzi sisi tunamuamini kwa uzoefu na maadili aliyokuwa nayo na uwezo aliokuwa nao kiasi cha kuaminiwa zaidi ya vipindi viwili maana yake hili si jambo la kuchukua zaidi ya miezi miwili, mitatu. Hata hivyo, namuamini Waziri na naamini atakapo-*windup* anaweza akatuletea jibu moja zuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kwa sababu nilisema nina jambo moja mahsus, mimi katika Jimbo la Msalala nina *interest* zangu pale lakini nataka niwaambie watu wa *REA* mpaka leo vijiji 32 tu ndiyo vimepata umeme na vijiji 63 havijapata umeme. Jambo hili linatupa shida na sijui kwa nini wakati uwezo wa kupeleka umeme pale upo. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba nisichukue muda wako. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Usi Pondeza. Tunaendelea na Mheshimiwa Maimuna Pathan atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Mohamed Abdallah.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii nyeti sana ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutoa shukrani zangu za dhati na pungezi nyingi sana kwa Kamati ya Nishati na Madini kwa kazi yao nzuri ambayo wameifanya kupitia kwa Mwenyekiti wake na wajumbe wote kwa kuishauri vizuri Wizara hii ya Nishati na mpaka inaendelea kufanya vizuri kwa sasa. Pia napenda kumpa pungezi nyingi sana Mheshimiwa Kalemani, Msaidizi wake na Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kalemani kwa kweli ni mtu ambaye ni msikivu, anajitahidi sana kutusikiliza. Mimi nimemsumbuu mara nyingi sana lakini namshukuru Mungu kila napomuendea kwa suala linalohusu *TANESCO*na mambo mengine ya Wizara yake, huwa ananjali na huwa tunampigia simu Meneja wa *TANESCO* na matatizo yote tunayaongelea vizuri. Kwa kweli, Mungu akubariki Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati kwenye eneo la umeme ni Wizara nyeti sana. Umeme ni kitu cha msingi sana kwenye maendeleo kwenye nchi yoyote. Tunashukuru mmeweka umeme wa *REA* sehemu nyingi sana kwenye vijiji vyetu. Ombi langu ambalo bado liko kwenu umeme wa Mkoa wa Lindi haueleweki au hauaminiki kwani unakatika sana mara kwa mara. Ndani ya dakika 20 au 10 umeme lazima ukatike, hauwezi ukununua vitu ukaweka kwenye friji vikakaa salama, itakuwa ni uongo vile vitu vinaharibika. Kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa mmesema kukuza ushiriki wa sekta binafsi kwenye maendeleo ya kiuchumi kwa kweli tunatakiwa tujitahidi kwa sababu kuna watu wengi wamejajiri kupitia kazi hizi za umeme lakini wanashindwa kufanya kazi zao vizuri kwa kuwa umeme huu hauko *stable*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Kalemani amesaidia sana kwenye Mkoo wa Lindi hususani Wilaya ya Liwale, Nachingwea na Ruangwa. Inaonekana kweli kuna mafanikio lakini naomba uongeze nguvu kwa sababu ile kasi ya kuzimika sana imepungua lakini bado unaendelea kuzimikazimika. Naomba Waziri atusaidie ili wananchi wale waweze kufaidi huduma hii ya umeme na wao wajisikie vizuri waone kama vile walivyo watu wa Dodoma wanavyofaidi umeme wao. Sisi wananchi wa Lindi tungefurahi sana tupate umeme kama huu wa Dodoma ili tuweze kujisikia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulichangia kwenye Wizara ya Nishati ni kuhusu gesi asilia. Gesi asilia ni muhimu sana kwa sisi wananchi wa Tanzania hasa wenye kipato cha chini ili iweze kutusaidia. Tunaomba sana hili gesi asilia ingeanza kutumika vizuri na pia isambazwe sehemu zote vizuri sana ili iweze kusaidia. Matumizi ya gesi asilia ukiangalia gharama zake ni nafuu sana kuliko vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna magari yanayotumia gesi asilia sasa hivi, matumizi ya yale magari nimejaribu kuongea na wale wataalam yako chini sana karibu nusu ya gharama ya mafuta ya petroli tunayotumia sasa hivi. Kilo moja ya gesi asilia ni Sh.1500 ambayo inaweza kutumika kwa zaidi ya kilomita, samahani kidogo nimesahau lakini gharama yake ni chini zaidi ukilunganisha na petroli lita moja. Tunaomba Wizara hii ya Nishati ijithahidi sana kusambaza hizo gesi asilia na pia iweze kutoa elimu kuhusu matumizi ya gesi asilia ili Watanzania tuweze kufaidika na gesi yetu ambayo iko katika nchi yetu ya Tanzania zaidi Mikoa ya Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa karibuni kulitokea tatizo la LUKU kwenye ununuzi wa umeme. Tunashukuru Waziri wetu alifanya jitihada na tuliona juhudhi alizokuwa amefanya hali ikarejea. Hata hivyo, siku mbili, tatu za juzi mpaka jana ile hali imerudi tena kwa Mkoo wa Dodoma. Watu wengi wamejaribu kununua umeme wameshindwa lakini sasa hivi

kuna watu nimewasiliana nao wanasema sasa hivi ile hali imeanza kurudi umeme umeanza kupatikana lakini kulikuwa na kama siku mbili tatizo lilitrudia tena. Tunaomba Waziri wetu ambaye anajituma sana Mheshimiwa Kalemani ajaribu kuliangalia tena tatizo hili ili wananchi wako tuweze kuva vizuri. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Pathan. Nilishakutaja Mheshimiwa Hamidu Mohamed Abdallah na utafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nianze kwa kufanya marekebisho ya jina langu mimi ni Hamida Mohamed Abdallah, ukisema Hamidu ni mwanaume na sio mwanamke. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya marekebisho hayo, nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Waziri wa Nishati pamoja na timu yake ya Wizara kwa kazi ambayo wanaifanya na wamefanya kazi nzuri sana kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Bahati njema nilikuwa kwenye Kamati hiyo ya Nishati na Madini najua nini kilichokuwa kinaendelea katika utekelezaji wa masuala mazima ya maendeleo na kuleta mapinduzi makubwa ya umeme nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kipaumbele, kama ambavyo taarifa imeelezea katika kasi ya kuongeza uzalishaji wa umeme lakini pia utekelezaji wa mradi mkubwa wa LNG ambaao tunategemea tutakwenda kuutekeleza. Nipongeze sana ndugu zetu wa TANESCO kwa kazi nzuri ambayo

wanaifanya ya kuendelea kutupatia huduma ya umeme katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana katika maeneo yetu ya Lindi Manispaa hatukuguswa na mradi wa *REA*. Kwa hiyo, bado tuna changamoto kubwa katika maeneo mbalimbali kutofikiwa na umeme. Ndugu zetu wa *TANESCO* hawana uwezo mkubwa wa kuweka miundombinu katika maeneo yote ya Mji wetu wa Lindi Manispaa, kwa hiyo, bado tuna changamoto.

Mheshimiwa Spika, tunajua tuko kwenye mpango wa Mradi wa *Peri-Urban*, lakini kwa namna ambavyo mradi huu unatekelezwa unaenda taratibu mno na sisi tuna hamu kubwa ya maeneo yetu yote kufikiwa na umeme kwa sababu tunajua kwamba uwekezaji wowote unahitaji uwepo wa umeme. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuhakikisha kwamba Mradi huu wa *Peri-Urban* kwa namna yoyote unakwenda kwa kasi kubwa na sisi wana Lindi tunahitaji kupata mradi huu.

Mheshimiwa Spika, sisi Lindi Manispaa tuna Majimbo mawili na Majimbo haya yana changamoto kubwa kwa sababu tuna maeneo ya pembezoni mwa mji na maeneo hayo sasa kuna uwekezaji mkubwa wa kilimo. Pia tunajua kwamba sasa wananchi wanakwenda kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji ambacho kinahitaji uwepo wa umeme. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuhakikisha kwamba mradi wa *Peri-Urban* unaharakishwa ili sisi wananchi wa Lindi tuweze kufaidika na mradi huu ambao utakuwa na gharama nafuu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bado ndugu zetu wa *TANESCO* wamekuwa na changamoto kubwa sana kwa sababu wananchi wanahitaji umeme lakini gharama za ulipaji wa umeme wa *TANESCO* ni shilingi 300,000. Hizi ni gharama kubwa sana mwananchi wa kawaida hawezi kumudu kulipa shilingi 300,000 ili apate umeme, kwa hiyo, kuna changamoto hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Iakini wanasema hawawezi kutekeleza kwa kulipa shilingi 27,000 kwa sababu hawana waraka wowote kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Dkt. Kalemani nilikuwa na wewe kipindi kirefu na kila unapokwenda kwenye eneo la mukutano ulikutana na hoja hii na uliweka wazi kwamba kila mwananchi atapata umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 bila kulipia nguzo. Hata hivyo, suala hili bado linaendelea na wananchi wetu wanashindwa kumudu kuweka umeme.

Mheshimiwa Spika, pia *TANESCO*wana changamoto ya nguzo kwa sababu wananchi wengi sana wamelipia ili waweze kufungiwa umeme pale Lindi Mjini Iakini *TANESCO* hawana nguzo hivyo wananchi wanashindwa kupata umeme. Hili ni suala la kushangaza watu wako katikati ya mji wanakosaje umeme?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la kutokuwepo kwa nguzo ni changamoto kubwa, tunaomba Serikali isimamie suala hili kuhakikisha kwamba changamoto hii inaondoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunao mradi wa matumizi ya gesi majumbani pamoja na magari. Bahati njema sana mwaka uliopita tumezindua mradi huu katika Kata ya Mnazi Mmoja eneo la Lindi Mjini. Tumefarijika sana na wananchi wana hamu kubwa ya kuona umeme huu sasa wanaendelea kufungiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa *offer* kwa wananchi wa Lindi nyumba 300 kufungiwa umeme kupitia mradi huu wa matumizi ya gesi majumbani. Hata hivyo, tangia mradi huu umezinduliwa mpaka leo hakuna chochote kinachoendelea. Tunahitaji Mheshimiwa Dkt. Kalemani utuambie ni lini sasa mradi huu unakwenda kutekelezwa.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge Viti Maalum Mkoala wa Lindi.

**WABUNGE FULANI:** Wa Jimbo.

**SPIKA:** Ooh ni wa Jimbo Mheshimiwa?

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ni Mbunge wa Jimbo na siyo Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi/ Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa itabidi baadaye tuonane ofisini ili tufahamiane vizuri zaidi maana nimekosea jina na *title*. Nakuomba radhi sana Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini, ahsante. (*Makofi/ Kicheko*)

Naomba nichukue nafasi hii kumkaribisha tena Bungeni Mheshimiwa Mushashu, karibu sana. Alifiwa na binti yake Upendo Kemirembe Karitas Mushashu. Pole sana kwa msiba mkubwa sana wa binti yako na karibu tena Bungeni ujiunge na sisi wenzako karibu sana. (*Makofi*)

Basi tunaendelea na mchango na sasa ni zamu ya Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa muda ulionipatia ili niweze kuzungumzia changamoto ambazo zinawakumba wananchi wa Nkasi Kaskazini. Kutokana na umuhimu wa Wizara hii nitachangia mambo machache kwa kuwa mengi yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kuhusiana na namna ambavyo Waziri pamoja na Naibu wake na *Cabinet* yote wanavyowajibika kwenye nafasi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri ambayo mnayafanya hasa kuititia miradi ya *REA* bado kuna changamoto kadhaa. Changamoto ya kwanza, kutokana na ukubwa wa hii miradi ambapo imesambaa maeneo mbalimbali *TANESCO* wanakabiliwa na changamoto ya usafiri. Kama tunavyoona kuna mambo mazuri mmeyafanya lakini bado kuna changamoto kwenye uzuri wake wa jambo hilo la usafiri. Kwa hiyo, kwa sababu Serikali ina nia njema kuwafikishia wananchi huduma ya umeme, basi tuone namna bora ambayo tunaweza tukaifanya ili hawa *TANESCO* waweza kuwajibika inapotokea changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la *REA*, naungana na Wabunge wote ambao tumekwenda kufanya *research* ya kutosha na Mheshimiwa Waziri anajua tumekwenda Manyara, Singida na maeneo mengine, wakisema wamepeleka umeme kijiji fulani utakuta watu wachache tu ndiyo wamepata lakini lengo la Serikali ilikuwa wananchi wote sio wachache. Kwa maana hiyo turudi kwenye lile lengo la kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini katika tafiti chache ambazo nilizifanya kwenye Kamati yetu ya *PAC* tulivyozunguka si kwamba wananchi hawataki kupata huduma ya umeme au hawataki umeme majumbani mwao, kuna watu ambao hata hiyo Sh.27,000 ni changamoto. Sasa kama lengo ilikuwa ni hilo na tumeingiza fedha za kutosha ili kupeleka miradi, kwa nini Serikali isibebe jukumu hilo la kuchukua hiyo Sh.27,000 wananchi wakapelekewa huduma na wakaanza kukatwa taratibu taratibu kulingana na huduma ambazo wanazipata? Naamini wananchi wengi watafurahia jambo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hizo, katika Jimbo langu lenye vijiji 49 vijiji 9 havina huduma ya umeme kabisa. Vijiji hivyo ni Itindi, Sentamapufi, Lyele, Matine, Miende, Mpenge, Kalila pamoja na Mkombe. Natambua kwamba kuna maeneo ambayo jiografia yake ni ngumu kama Jimbo langu, kuna vijiji ambavyo unavuka ziwa ndio unakwenda pembeni unawakuta wananchi na wale

wananchi wanajishughulisha na uvuvi na leo tunasema kwamba waende kwenye viwanda lakini umeme haujafika. Kwa hiyo, bado wanaendelea na uvuvi uleule kama tunavyosoma historia ya Yesu walivyokuwa wanavua ukishapita muda fulani hawajauza samaki wale wanaharibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kwa kuwa lengo ni jema pia tuangalie yale maeneo ambayo yana umuhimu zaidi. Natambua kwamba wote wanafanya kazi na wanahitaji kupewa umeme, kuna wengine wanatumia kwa ajili ya mwanga peke yake lakini tunatazama miradi hii ya *REA* namna ambayyo itasaidia pato la Taifa kwa wananchi kuweza kuendelea na majukumu yao kuitia suala la umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kukatika kwa umeme na hili ndilo limenifanya nisimame hapa. Wilaya ya Nkasi na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla umeme unakatika isivyo kawaida. Imefikia mahali kwa sababu watu walishahau vibatari na taa lakini wanaona ni bora walikuwa wakiweka mafuta kwenye taa anajua haya mafuta niliyoweka yatanitosha mpaka kesho nitaweza kununua mafuta mengine lakini leo umeme umekuwa haueleweki yaani unaweza ukakatika zaidi ya mara saba. Mheshimiwa Waziri na sisi watu Nkasi ni Watanzania; kuna wafanyabiashara, kuna wamama kule wameamua kutengeneza juisi na vitu vingine, tungependa kujua tatizo ni nini. Pamoja na kwamba umeme unapokatika wenye wajibu wa kutoa taarifa ni *TANESCO* kwamba kwa nini umeme umekatika na utarudi baada ya muda gani lakini mambo haya hayafanyiki na ni mazoea tu ambayo yanaendelea. Sasa hawa wananchi kwa sababu hii ni huduma tunahitaji basi kuwajibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye jambo hili naomba pia Kitengo cha *Emergency*, kama neno lenyewe *emergency* bado kuna changamoto hakuna *emergency* tena sasa hivi. Ni vizuri tukaboresha kitengo hicho kiwe *emergency* kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa navyozungumza Kata za Kalando na Itete toka jana mchana mpaka leo wako gizani. Sisi tupo mpakani mwa Congo na Burundi amani ya nchi yetu inakuwaje kama watu wako gizani? Ni lazima tuwape kipaumbele watu wa mipakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijasimama hapa kuchangia nimeongea na Meneja wa *TANESCO* anasema ni tatizo la nguzo kuungua toka jana, ni vizuri tukaboresha kitengo hiki. Kama lengo la kupeleka *REA* ni kuwashudumia wananchi basi tuboreshe na hivyo vitengo maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida Khenani. Mheshimiwa Waziri nafikiri hilo la kukatikakatika umeme itabidi jioni uliguseguse kidogo katika majibu yako maana yake imekuwa kero kwelikweli. Linanikumbusha enzi hizo, nikiwa nasoma nchi moja huko Ulaya, zamani hizo nikiwa mwanafunzi tulikuwa tunaandaa maonyesho fulani kwenye ukumbi kama huu, sasa akawa anakuja mtoto wa Mfalme wa nchi hiyo kama mgeni rasmi usiku wakati wa maonyesho hayo. Nilikuwa kwenye Kamati ya Maandalizi nikawauliza baadhi ya waandaaji, hivi nimezunguka hili jengo lakini sijaona jenereta, *incase* mtoto wa Mfalme akaja hapa na umeme ukazimika itakuwaje? Yule kijana akaniangalia akaniuliza unadhani mimi nina umri gani? Nilikuwa nafanya *degree* ya pili na yeze tuko naye darasa moja nikasema nadhani una miaka kama 35 hivi, akaniambia umepatia / *am around there*, sijawahi kuona umeme unakatika katika maisha yangu, umeme huwa unakatikaje? (*Kicheko*)

Mnaweza mkaelewa tabu niliyopata maana sitaki nchi yangu ionekane kwamba kuna shida, nikaanza kubadilisha *topic* pale na nini ananiambia nieleze umeme unakatikaje? Kuanzia hapo tukikaa darasani na mahali pengine anasema huyu bwana huyu ana mawazo ya ajabu sana, yaani yeze badala ya kufikiri mambo ya maana anafikiri vitu ambavyo havipo. Jana aliniambia habari ya umeme

kukatika, hivi umeme huwa unakatikaje? Nilipata tabu sana na swali hilo. (*Kicheko*)

Sasa hiyo ni miaka sijui 20 au 30 iliyopita sisi bado umeme unakatika mara 20 kwa siku moja. *We have to move from there kwa kweli, something has been done.* Lazima tuambiwe shida nini ili tuweze kuelewa. Tunajua Mheshimiwa Waziri unajitahidi lakini basi kutuambia tu tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ulenge*.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti hii ya Waziri wa Nishati. Kusema kweli na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo imeendelea kufanyika toka aliposhika Wizara hii. Hii inonesha kabisa kwamba katika kipindi kifupi kwa maana baada ya mwaka mmoja nchi nzima ya Tanzania itakuwa imepata umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nijielekeze tu kwenye Jimbo langu la Musoma. Mheshimiwa Waziri anafahamu, bahati nzuri nilimwalika na alikuja Musoma na tukawasha umeme kwenye Mtaa wa Bukoba. Baada ya kuwa tumewasha umeme Mtaa wa Bukoba pale pale akatoa agizo kwamba kuanzia sasa kwenye maeneo yote ya pembezoni yatapata umeme. Naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri toka alivyotoka, lile eneo la pale Bukoba hawajapata umeme zaidi ya ule aliowasha. Mitaa ya Nyabisale, Songambele, Kwangwa A, Kwangwa B, Mugalanjabo, Zanzibar, Bukanga hivi ninavyozungumza hawajapata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Waziri amechukua hatua za kuzungumza na Meneja wa *TANESCO* na akamuagiza, bahati mbaya tu sasa hivi hayupo Mwenyezi Mungu amrehemu lakini hilo tatizo kwangu ni kubwa. Nadhani mwezi uliopita Naibu Waziri Mheshimiwa Byabato alikuja Musoma aliweza kushuhudia alikaa mpaka na Wenyevitii wa

Mitaa wanamweleza hali ya umeme ulivyo wa shida pale Musoma Mjini.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* tunapowauliza wao wanasema hivi, ni mita 30 toka pale nguzo ilipo kulia na kushoto zaidi ya hapo hawatoi umeme. Kikubwa zaidi *TANESCO* kila tunapowauliza wanasema hawana bajeti sasa Mheshimiwa Waziri leo ataniambia nini kwa sababu kwenye vitabu hata kwenye ile miradi ya *Peri-Urban* sisi Musoma hatumo, sasa endapo Musoma hatumo na *TANESCO* wanasema hawana bajeti yetu tunafanyaje? Waziri ametangaza hapa kwamba hakuna mwananchi kulipia nguzo sijui wale watu wa Musoma watafanyaje. Naomba baada ya Bunge hili tukubaliane kwamba tukishaahirisha twende wote akawaambie kwamba ndugu zangu ile ahadi aliyotoa kwamba watu wa Musoma watapata umeme wa Sh.27,000 haipo badala yake walipie tu zile gharama za kawaida za shilingi laki tatu na kitu tofauti na hapo tutaendelea kuonekana sisi wengine ni waongo.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri labda atoe maelekezo ili fedha ziweze kupatikana kwenye maeneo kama haya ya *Peri-Urban* kama ambavyo imetokea kwenye mikoa mingine na ameweza kuonesha ili na sisi watu wa Musoma tuweze kupata umeme. Faida za umeme kila mmoja anazifahamu na kwa sababu watu wetu sasa walishajua kwamba umeme wa Sh.27,000 unakuja kila siku inaonekana mimi Mbunge ndiye ninayewakwamisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri aangalie fedha zile zinazokwenda kwenye mfuko wa *REA* ziweze kwenda kwa Mameneja wa *TANESCO* wa Mikoa ili zile ahadi ambazo Serikali inazitoa basi iweze kuzitekeleza. Kusema kweli pamoja na kazi kubwa na nzuri ambayo imeendelea kuonekana lakini kwetu sisi wengine hali si shwari kabisa. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba atakapokuwa anajibu basi suala la Musoma asiweze kulisahau.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu ya muda naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella M. Manyanya.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na niwapongeze sana Mawaziri na Naibu wake kwa utekelezaji mzuri wa majukumbu yao. Vilevile nimshukuru na kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati kwa wasilisho zuri ambalo limetupa *guidance* ya kutosha kuweza kuchangia hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tunaona nchi zetu mbili na Marais wetu; Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Uganda wakitia saini ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima mpaka Chongoleani Jijini Tanga. Kwa mujibu wa maelezo ya mradi huu unatajwa kwamba takriban ajira 6,000 – 10,000 zinaweza kutokea na kuna fursa nyingi sana za kibiashara zinaweza kutokea kwa watu ambaa mradi huo utapita. Naomba kuishauri sana Wizara i-manage *expectations* za wananchi wetu katika maeneo ambayo mradi huu unapita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni nini? Tusije tukawaahidi wananchi wetu kwamba kutakuwa na fursa nyingi sana za kibiashara mwisho wa siku ikawa kinyume chake. Tunaiomba Serikali na kuishauri ituletee tathmini walioyofanya katika ujenzi wa *TANZAM* wakati wanajenga bomba ya mafuta kutoka Tanzania mpaka Zambia fursa gani zilipatikana na za aina gani na wananchi waweze kujianaa. Vilevile tulipojenga bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam watuletee tathmini ya ajira na fursa za kibiashara ambazo wananchi waliweza kufaidika ili watu wetu waweze ku-manage matarajio yao ili mradi ule ukafanyike vizuri bila kusabbisha *chaos* wakati wa utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba sana kuishauri Serikali *i-coordinate* na Wizara nyingine ambazo zitarahisisha utekelezaji wa mradi huu. Tunafahamu kwamba wakati wa ujenzi huu kutakuwa na huduma za *consultation* kati ya wataalam wa mradi na ninyi wataalam wa Serikali, ina maana kwamba kutakuwa na safari nyingi sana kati ya Tanga na Dodoma, kati ya Tanga na Uganda kwa ajili ya *consultation* za utekelezaji wa mradi huu. Hata hivyo, inashangaza ninyi Wizara ya Nishati mmekaa kimya, Kiwanja cha Ndege cha Tanga hakijajengwa mpaka sasa, mna mpango gani na wataalam wa mradi huu hamuoni kama mtawasababishia *difficulties* katika utekelezaji wa kazi zao? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mnafikiri Hayati wetu alipotoa ahadi ya kutekeleza ujenzi wa kiwanja kile pale Chongoleani wakati anazindua mradi huu maana yake ilikuwa ni nini? Maana yake ni kutaka ku-*facilitate* utekelezaji wa mradi huu kwa haraka. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwa maana ya Wizara ya Nishati ya Madini ika-*coordinate* vyema na Wizara ya Ujenzi ili Kiwanja cha Ndege cha Tanga kijengwe haraka iwezekanavyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mradi huu tunafahamu kwamba gesi itachimbiwa ardhini kwa maana ya lile bomba lakini tunafahamu kwamba lazima kuwe na *facilities* kama za zima moto katika maeneo yote ambayo bomba hili litapita. Wizara hii inapaswa ku-*coordinate* na Wizara ya Maji kuhakikisha maeneo yote yale ambayo mradi huu unakwenda kupita kunakuwa na maji ya kutosha *incase* kama bomba linakwenda kuvujisha lazima tuwe na tahadhari za kutosha kuhakikisha wananchi wetu wanaendelea kuishi salama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa upande wa Chongoleani kaka yetu Mheshimiwa Aweso maji yamekwenda lakini maji yale hayatoshi. Ni lazima tujenge *water high drinks* za kutosha katika maeneo yale ili wananchi wetu waweze kuishi salama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mhandisi Mwanaisha Ulenge. Sasa anaafuatia Mhandisi Stella Manyanya, simuoni.

**WABUNGE FULANI:** Yupo.

**SPIKA:** Yupo Enheee. Bado hajasimama. (*Kicheko*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ngoja nisimame uweze kuniona. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella amesimama sasa. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Pia nimpongeze sana injinia mwenzangu Mheshimiwa Ulenge kwa mchango wake mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianzie kuipongeza sana Wizara hii lakini kuwapongeza watanzania wote kwa jitihada za pamoja tulizofanya kuhakikisha kwamba Shirika la Umeme la Taifa (*TANESCO*) halipelekwi kuwa ni shirika la mtu binafsi limebakia kuwa ni shirika la Tanzania kwa ajili ya kuchochaea maendeleo ya Watanzania. Kazi nyingi zinazofanywa na shirika hili kwa kweli ni za kuchochaea maendeleo na siyo faida kama faida ilivyo. Ndiyo maana kwa muda mrefu limekuwa halizalishi faida kwa ajili ya kuangalia wananchi wote wenye uwezo na wasio na uwezo. Tunafurahi hali inavyokwenda sasa *TANESCO* wanaanza kutengeneza faida. Kwa hiyo, natoa pongezi sana kwa Wizara pamoja na shirika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na suala la kwamba mpaka sasa tumeshindwa kufikia malengo tuliyojiwekea ya kupata *megawatts* 5,000. Niseme tu kwamba mimi naona tumekwenda vizuri nikiwa kama mjambe wa Kamati hii ni kwamba kwa miaka takriban 60 ya toka Uhuru wetu tulikuwa tukiongeza wastani wa *megawatts* 26.7 tu katika *grid* yetu

kwa maana kwamba tulikuwa na *megawatts* 1,605 tulizonazo sasa lakini hizo zimefikiwa baada ya miaka 60 sasa, umri wa mtu kustaafu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa kupitia hii mikakati tuliyojiwekea ya kuanza kuzalisha umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na maeneo mengine tayari mwaka 2022 tunaongeza *megawatts* 2,115 kwenye Grid ya Taifa. Jambo hili ni kubwa sana, unaweza ukawa na malengo lakini kuyafikia unayafikia kwa kiasi gani. Malengo haya yanatufikisha sisi kwa lengo tulilojipangia kwa asilimia 74 siyo kitu kidogo, ni kitu kikubwa lazima tujipongeze kwa kile ambacho tumeweza kukifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwaombe *TANESCO* watu vijiji sasa hivi maendeleo yao yamejiwekeza sana kwenye umeme, haitoshi tu kupitisha laini halafu wananchi hawapati umeme lazima sasa lipatikane fungu la kutosha kwa ajili ya kuweka umeme wa laini ndogo yaani *LV lines*. Hilo ndilo eneo ambalo sasa hivi kwa kweli halipati fedha za kutosha. Wanakijiji hawapendi tu kuona kwamba *line* imepita hapa wanataka kutumia umeme. Kwa hiyo, kwa fedha hii inayotengwa lazima fedha za kutosha zipelekwe kwa ajili ya kuongeza *wire* hizi ndogo yaani *LV lines*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine naomba niwasaidie ndugu zangu jana nilimsikia Mheshimiwa Mbunge Joseph wa Ukerewe akizungumzia juu ya vile visiwa vinavyopata umeme kwa bei kubwa sana takriban Sh.2000. Kwa muda mrefu shirika letu lilikuwa ndio shirika pekee linalosambaza umeme mijini na vijiji sasa sehemu moja wanapokuwa wanapata umeme kwa bei kubwa sana nimejiuliza kwa nini? Kumbe ni kwa sababu wale wana-*independent power producer* yaani wanapata umeme kupitia *solar*, ni mtu binafsi amewekeza, kwa hiyo, lazima umeme utakuwa ghali. Sasa niwaombe *TANESCO* kwa sababu wao wana umeme ambao unapatikana kutoka kwenye maji na vyanzo vingine na umeme huo waupe *either* ruzuku au waununue wao halafu wananchi wauziwe umeme kwa bei sana na watu wa maeneo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, sheria ya *EWURA* irekebishwe iweze na yenyewe kuwa na vituo vya mafuta vijijini. Tumechoka kuona chupa za *petrol* kule vijijini halafu zitakuja kuleta madhara tutakuja kuulizana hapa. Watumie *formula* hii hii kwa sababu tuna Shirika letu la Kusambaza Mafuta Vijijini ili sasa nao waweze kuwa na vituo vidogo vidogo huko vijijini tuondokane na mafuta ya kwenye chupa kwa sababu pikipiki na fursa nyingi ziko huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Tuwapate wawili wa mwisho Mheshimiwa Godwin Kunambi na Mhehimiwa Zahor Haji.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa lakini nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii ya Nishati. Waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Naogopa kusema hapa mimi binafsi au labda kwa sababu ndugu yetu huyu ni Msukuma tabia ya unyenyekevu hii kwake yaani ni ya ajabu kwangu ana unyenyekevu uliopitiliza. Wapo waliosema hapa lakini mimi binafsi nasema tu kwamba katika Mawaziri ambao wanaofanya kazi vizuri, kaka yangu Mheshimiwa Kalemani Mungu akubariki sana, umejitoa na unafanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitagusa kidogo kwa habari ya *TPDC*. Shirika hili la Maendeleo ya Petrolini nchini lilianzishwa mwaka 1969 kwa Amri ya Rais chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (*Public Corporation Act*). *TANESCO* wamefanya kazi vizuri sana na wanaendelea kufanya kazi vizuri lakini *TPDC* nilikuwa najaribu kufanya hesabu hapa huyu mtu aliyezaliwa mwaka 1969 sasa ana miaka 52. Pamoja na mambo mengine inayofanya *TPDC* hoja yangu ya msingi mpaka leo tunaendelea kufanya tafiti za mafuta miaka 52.

Mheshimiwa Spika, Adolf Hitler mwaka 1945 wakati anakwenda kupigana Vita ya Pili ya Dunia German-Austria

pale Linz aliwaita wahandisi akasimama na kusema; nakwenda kupigana vita jangwani nahitaji kupata mashine inayotumia *air cooling system* akawapa siku saba. Ilikuwa wachague moja, ama awapige bastola ndani ya siku saba wakishindwa kazi hiyo au wagundue mashine ambayo itatutumia *air cooling system*. Ndani ya siku saba wahandisi wale wa Ujerumani walikuja na majibu ya *air cooling system*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, akili ya mwanadamu ilivyo ukiacha iwe huru inazubaa. Mwanadamu siku zote anataka kusumbuliwa. Ukimtia upepo kidogo anashtuka ndiyo maana hata wakati ule sisi tunasoma darasa la saba ukipigwa fimbo kesho hiyo *table* unaishika vizuri sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri moto ule ule aliotumia TANESCO aupeleke *TPDC*. Waziri aende *TPDC* akawaeleze...

## TAARIFA

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Chifu Kunambi kwamba kwa vigezo na uzoefu wa kutafuta mafuta *TPDC* hajjawezeshwa na haiko kwenye viwango vya kutafuta. Ndiyo maana jana nikawaambia kwamba Uganda 2002 - 2015 walikuwa wamechimba visima 11 ambayo ni *confirmatory test* ya kutafuta mafuta ilhali Tanzania *TPDC* wanatuambia wamechimba visima vitatu pale juu, sio namna hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunambi, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, naipokea Taarifa hiyo lakini bado niendelee kusisitiza tu kwamba Mheshimiwa Waziri sisi Wabunge nadhani kila mmoja hana mashaka na wewe na tunakuombea Mungu

aendelee kukubariki na Mheshimiwa Rais aendelee kukuona hivyo hivyo na sisi uendelee kutuhudumia kama Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine namuomba Waziri atusaidie kuhusu gharama za umeme hasa kwa sisi wananchi tunaoishi vijijini. Ni kweli tumekupongeza, unafanya kazi nzuri lakini hii gharama ya Sh.27,000 tafsiri yake kidogo hebu itazame Mheshimiwa Waziri ni pale ambapo kuna nguzo ya umeme na kuleta umeme kwangu au ni pale ambapo unatakiwa kuvuta nguzo nne au sita? Hili kidogo liwekwe sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwananchi wa kawaida kabisa wa kijijini ukimwambia alipie hizo nguzo sita mpaka kwenye nyumba yake ni vigumu sana. Jana mimi nilipata meseji tatu za wananchi wangu wanaomba niwachangie laki moja moja nao walau wapate umeme. Kama Mbunge sijui utachangia wangapi wananchi zaidi ya 100,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie ufanuzi anapokuja kuhitimisha hotuba yake jioni ya leo atueleze kuhusiana na suala hili. Watanzania hasa wananchi wa Jimbo la Mlimba wangependa kufahamu gharama hii ya Sh.27,000 inazungumzwa vipi? Ni kuvuta umeme kutoka kwenye nguzo au kuongeza nguzo? Mimi nyumba yangu inahitaji nguzo sita, saba au nane bei hiyo inahusika pia? Kama hoja itakuwa tofauti na hiyo Mheshimiwa Waziri mtusaidie namna gani mnakwenda kama Wizara sasa kufikiri na kutafakari juu ya kupunguza gharama hizi ili kumpunguzia mzigo Mtanzania huyu hasa wa kipato cha chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nimemshukuru kwa dhati kabisa na mimi kwangu bahati nzuri tuna mradi ule wa umeme pale Kihansi na tulikuwa tunashuhudia tu umeme unapita unakwenda Dar es Salaam na maeneo mengine leo hii Mheshimiwa Waziri amekwenda kukamilisha pale Mlimba vijiji 11 viliviyobaki, nakushukuru na nakupongeza sana. Hoja inayobaki kwa wananchi wa Jimbo la Mlimba

pamoja na kwamba tunakwenda kukamilisha vijiji hivi 11 je, umeme huu utafika kwenye maeneo muhimu kama vile shule, vituo vya afya na zahanati? Haya ni maeneo muhimu sana kwa sababu utaona umeme unapita kwenye njia tu lakini taasisi muhimu kama hizi hazina umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba niunge mkono hoja na Mungu aibariki Wizara hii muhimu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Kunambi nakushukuru. Mheshimiwa Zahoro Haji.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nishukuru kitu chako kwa ufupi. Pili, naomba niseme kwamba ninashikiri au niko kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Nimekuwa nikijaribu kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge hapa kwa muda mrefu toka tumeanza Bunge kuna jambo linaendelea kujitokeza sana. Sasa naomba hasa wenzetu wa Serikali hili walitafakari tena kwa kina na hatua za dharura zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunapata mafunzo au tunachukua hatua tunapoona matokeo yanazidi kukithiri. Siku chache zilizopita tuliskia tatizo dogo kutoka kutoka *TRA* kwamba mifumo kila siku iko chini lakini baadaye tukasikia tatizo la *TANESCO* kwamba watu hawawezi kununua *LUKU* lakini hapa kiongozi amerudia tena kuongelea suala hili inaonekana limerudiarudia. Ombi langu kwa *TANESCO*, tuko kwenye *cyber war*, kuna kitu tunaita *cyber warna* kitu tunaita *cyber-crime*, umeme ndiyo unaotumika kupeleka athari zote kwenye mifumo yetu. Naomba sana na hili *TANESCO* mliangalie sana, vinavyotokea havitoeki kwa bahati mbaya, ni mambo yanayopangwa na yanapangwa yatokee ili siku moja tu-*collapse*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie wenzetu kwamba *TANESCO* tumewapa kuongoza Serikali kwa sababu leo maji tunalipia kwa *internet*, umeme tunalipia kwa *internet* maana yake ni kwamba hata benki zetu zinatumia *internet*

kufanya mambo yake maana yake ndiko kelele ziliko. Hata hivyo, *internet* leo inawezeshwa kuitia kwenye umeme, ombi langu kwa *TANESCO* haya mambo hayaji kwa bahati mbaya iko siku sote tuta-*faint* kwa sababu tunaelekeea kwenye *cashless economy* ni kwamba ni mitandao ndiyo inayotuwezesha kufanya mambo yote maana yake tumewapa kuendesha Serikali kwa kutumia umeme. Tunawaomba sana muwe makini na suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mkiangalia *attemptzinazofanywa BoT*, iko siku tutawaomba hapa waje watuambie *attempt* za mara ngapi zinafanywa kwenye benki zetu kwa kutumia *internet* ambazo zinapitia kwenye umeme. Tunawaomba sana tumewapa shirika hili au taasisi hii muweze kutulindia nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu alitukumbusha kwenye *backup* maana yake tuweze kujilinda lazima tuwe na *plan B* na *plan C* kwenye kujilinda ili tusifikie siku tukawa hatuwezi au kila kitu kime-*paralyze* kwa sababu ya *internet* kumbe siyo *internet* ni kwa sababu ya umeme. Kwa hiyo, nawaomba sana mtililie maanani suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hili naomba uendelee kutusaidia wataalam wetu walikumbuke kwamba umeme ndiyo unaotumika kuitisha kila kitu. Juzi Marekani nadhani mmeona wataalam, Serikali ya Marekani illiazimika kuwalipa wataalam wa *IT* ambao huku tunawaita *hackers*, si kwa sababu walipenda kwa sababu *system* zao za mafuta zilingiliwa na *hackers*, waliwalipa! Pamoja na *policy* zao kwamba hatuzungumzi na watu ambao hawahusiki na *system* zetu lakini waliwalipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba shirika letu au Wizara yetu ilisimamie suala hili ili kuhakikisha kwamba hatufiki mahali tukashindwa kufanya mambo yetu kwa sababu tumeshindwa huko. Lazima tuwe na wataalam wetu wa ndani ambao watalinda mifumo yetu ili tusishindwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ushauri mzuri sana Mheshimiwa Zahor Haji. Nawashukuru sana kwa michango yenu, kwa kweli imekuwa mizuri sana inayoisaidia Wizara. Michango mingi kabisa yenye mchanganuo mpana kabisa. Naamini na wanafunzi wetu wa vyuo vikuu walioko kwenye *gallery* zetu wameweza kufuatilia kwa umakini. Moja ya mafunzo ya chuo kikuu kwa mwanafunzi ukiacha ile taaluma anayosomea anafundishwa kufanya kazi *under pressure/duress, homework* haijaisha, natakiwa kukusanya hiki, kuna mtihani kesho, kuna *quizhapa*, kuna hiki pale yaani ile *pressure*. Kama sasa hivi saa saba unaambiwa saa tisa kuna mtihani na hujakaa vizuri, saa kumi kamili usipokusanya kitu fulani kwa mwalimu hapokei tena, kwa hiyo, lazima uanze kukimbia, sasa ile *duress/pressure* ile ndiyo inakufundisha utakapotoka chuo kikuu ukikutana na mambo ya kawaida haya yaani unakwenda bila tatizo. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa niwatangazie kwamba Taasisi yetu ya Dar es Salaam *Institute of Technology (DIT)* wako katika viwanja vya Bunge kule nyuma ya Msekwa kwa ajili ya kuonesha teknolojia ya gari linalotumia gesi. Kwa hiyo, mkitaka kuona Waheshimiwa Wabunge mfike pale nyuma ya Msekwa na wale wa Ngorongoro pia bado wapo kwa hisani ya Wizara ya Maliasili na Utalii. (*Makofii*)

Ninao wageni 121 wa Mheshimiwa Elibariki KIngu ambaao ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kutoka Mkoa wa Dodoma ambaao pia ni Mabalozi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) katika kuhamasisha wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu kujiwekea akiba *NSSF* kwa ajili ya kesho yao. Wanafunzi hao wameambatana na Meneja wa Usimamizi wa sekta hiyo isiyo rasmi Ndgi. John Mwalisu pamoja na wafanyakazi wenzake kutoka *NSSF*. Wale wanafunzi 121 na *NSSF* pia naomba msimame pale mlipo. Tunawakaribisha sana hapa Bungeni. Yupo Mbunge kijana mmoja anaitwa Ng'wasi, hebu simama bwana, aliwahi kuzungumzia sana jambo hili ambalo mnalisimamia, mnajaribu kuli-*practice* kwa kuona jinsi gani wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu mnaweza mkaji-*integrate* katika kufanya mambo haya ambayo sasa ninyi mnaanza

kuwa ni mfano katika kijiwekeea akiba na katika kuangalia kesho yenu. Muhimu sana hili, ahsante sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna wageni waliotembelea Bunge ambao ni wanafunzi 61 wa Chuo Cha Mipango kutoka Jijini Dodoma. Mipango wako wapi? Oh, ahsanteni sana. Karibuni sana watoto wetu kutoka Mipango. Nilikuwa nawaambia kama utani tu watu wa Wizara ya Fedha kwamba hiki chuo kinatakiwa kibadilishwe jina badala ya kuitwa Chuo Cha Mipango Vijiji sasa kitiwe tu Chuo Cha Mipango basi kwa sababu vijiji vimebakvi vichache sana labda kule Usukumani kuna vijiji sisi hapa Dodoma karibu kila mahali ni mji na hasa baada ya Mheshimiwa Kalemani kuleta umeme yaani kila mahali ni mji. Tunataka mipango miji na Waziri wa Ardhi, Waziri wa Nishati, Maji na kadhalika yaani tunataka kimjimji habari ya vijiji tunazidi kuachana nayo. Sasa ninyi mkisoma habari ya vijiji, vijiji inaisha sasa ni mijini tu, kuna miji mikubwa, majiji, manispaa na miji midogo, vijiji hamna. Vijiji vimebakvi Unyamwezini na Usukumani basi maana wamechelewa sana hawa jamaa. Ahsanteni sana watoto wetu, mnaweza mkakaa. (*Kicheko/Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji wala sina haja ya kutaja majina, nawaomba tu wale ambao mko kwenye orodha muwahi kufika, atakayefika mapema tutam-*note* na atachangia mapema kuliko mwenzake. Muda wetu ukituishia itakuwa basi tena ndiyo imekuwa bahati mbaya. Naomba tu muwahi kufika, nitakuwa na jicho kabisa la kuona yule yupo, yule yupo haraka haraka basi mtachangia kwa kuanzia halafu tuone muda gani tunabakiza kwa ajili ya Waziri ili aweze pia kutujibu kwa sababu mambo ni mengi ambayo mmeyaongea.

Kwa jinsi hiyo basi, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi leo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.16 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na tutaanza na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Mimi kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, ye ye na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa Jimbo langu la Maswa Mashariki na Maswa nzima kwa ujumla kwa kweli tatizo la kukatika umeme limekuwa sugu. Kila siku tunasikia mipango mizuri na nini lakini hatuoni juhudhi ya kuondokana na kero hii ya kukatikakatika kwa umeme. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri mfanye basi jitihada za ziada ili kuweza kuondokana na kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna vijiji vyangu vingi ambavyo havina umeme. Tumeona mradi wa REA umefanya kazi vizuri sana lakini wamefanikiwa kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Kata, tunakubaliana na hilo, hata hivyo, vijiji vya pemberi mwa kata hizo havina umeme. Kwa hiyo, katika records zetu zinaonesha kama vile kata zote Wilaya ya Maswa zimepata umeme lakini ukiangalia vijiji vya pemberi mwa kata hizo hakuna umeme.

Kwa hiyo, tunaomba sana msifikishe tu umeme kwenye kata basi mpeleke na vijijini, maeneo ya pembezoni mwa kata hizo. Kwa mfano pale Maswa kuna Kijiji cha Jilago, Mwabadini, Mbugamita, Mbalagane, Chugambuli,

Mwabalogi, Mlimani, Mwabalatulu, Mwamashindike, Ikungulyankoma, kote huko tunaomba umeme ufile jamani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Yaani majina hayo, sijui urudie tena ili Waziri aandike? Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie; Jilago, Mwabadini, Mbugamita, Buhangija, Chugambuli, Mwabalogi, Mlimani, Mwafumbuka, Mwabalatulu, Ifungilo, Mwamashindike na Ikungulyankoma. Mheshimiwa Kalemani atakuwa amenielewa vizuri sana, tunaomba umeme ufile tumetoa ahadi siku nyingi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nichukue tena fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe na Mheshimiwa Waziri kwa uamuza wenu mliouamua wa kupeleka ile huduma ya vinasaba kwenda *TBS*. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Spika umeshaamua na Wabunge tumeshaamua kwamba tubadilishe sheria, lakini kuna *data fulani* napenda Watanzania waielewe; tunapopeleka huduma ya vinasaba *TBS* kuna *advantage* kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimezunguka kuna watu wengine mpaka wakawa wananiuliza tena wengine mpaka Wabunge wanakuuliza, hivi vinasaba ni nini? Vinasaba kwa lugha nyepesi ni rangi ya kutia kwenye mafuta na uamuza huu tuliuamua mwaka 2010. Mafuta yanapotoka bandarini kuyatofautisha na mafuta yanayokwenda nchi za jirani ilibidi mafuta yetu tuyatie rangi, ni uamuza mzuri sana ili kuepuhuna na yale mafuta yanayokwenda nje ya nchi kushushwa njiani. Hata hivyo, kitendo kinachofanyika kwa kweli kilikuwa kinafedhehesha sana kwa sababu bado mafuta yalikuwa yanashushwa njiani na kwa sababu vinasaba vilikuwa vinamilikiwa na mtu binafsi ilikuwa rahisi kuwauzia watu wengine kisha wanaenda kutia ile rangi kwenye mafuta ambayo yako *on transit*. Tunawashukuruni sana kwa uamuza huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa harakaharaka hii Kampuni ya *Global Fluid International (GFI)* tunakubaliana walikuwa wanalipa kodi lakini naomba nikutaarifu kodi waliyolipa mwaka 2020, *corporate tax*, ilikuwa ni shilingi bilioni 1.86 tu na VAT walikuwa wanalipa wastani wa milioni 650 kila mwezi. Mafuta yanayopita kwa siku tuna wastani wa lita milioni tisa, wana-charge shilingi 14 kwa lita, ukichukua milioni 9 mara shilingi 14 mara siku 365 za mwaka walikuwa wanachuma Sh.45,990,000,000 halafu wanalipa *corporate tax* bilioni 1.86 na VAT wastani wa milioni 650 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, tukiwapa *TBS* kwa bei hiyo hiyo ya shilingi 14 mara lita milioni 9 kwa siku mara siku 365 wanapata hiyo bilioni 45.9 gharama zao ni bilioni 33. Vilevile watatoa fedha kwa ajili ya *development* bilioni 2.5 na bilioni 9 itakwenda kwenye *Government Consolidated Fund*, tutapata bilioni 9. Hii ni fedha nyingi. (*Makofî*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhan, Singida Kaskazini.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na kunipatia fursa hii angalau na mimi niwasemee wananchi wenzangu wa Jimbo la Singida Kaskazini kuhusiana na suala hili muhimu sana la nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara na hasa Waziri Kalemani kwa usikivu wake mwingi sana tunapokuwa tuna mahitaji kwake, tukiwa na shida mbalimbali kwa kweli, amekuwa msikivu na anatusikia. Namuomba

aendelee kuwa mnyenyeketu na asipandishe mabega.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mambo machache matatu makubwa, umeme wa *REA*, umeme wa upepo Mkoani Singida na ule umeme mkubwa unaotoka Namanga – Arusha – Singida. Kwa upande wa *REA*, kata zangu tano hadi sasa hazijaguswa kabisa na umeme hata nyumba moja zinakaa gizani, lakini unakuta kata imezungukwa, wamegusagusa kwenye *centres* za kata lakini maeneo ya jirani yameachwa.

Mheshimiwa Spika, mathalani Kata ya Ughandi yenye Vijiji vya Senenemfuru, Laghane, Damisinko, hajaguswa hata kidogo. Upande wa huku Msisi angalau wameguswaguswa upande wa Mashariki Ntinko, kuna baadhi ya maeneo yameguswa, lakini kata iko katikati kwa nini hata vijiji vya jirani visipate umeme?

Mheshimiwa Spika, Kata ya Itaja ambayo iko barabara kuu, *Arusha Road*, vijiji vyake hata kimoja havijapata umeme, lakini kuna vijiji vya jirani ambavyo vina umeme. Kwa nini sasa wasingekuwa wanaunganisha vijiji kulingana na jiografia?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe Vijiji vya Ngimu, Bohama, Mbwighanji, Lamba, Kinyagigi, Makuro, Mkenge, Matumbo, Poku, Ghalunyangu, Mwalala, Migugu, Minyenye, Ikiu, Mwarufyu, Mdhae, Mwasauya, Sefunga, Ndwamoghanga, Unyampanda vipatiwe umeme. Nashukuru kwamba tumepatiwa huyu mkandarasi *at least* tunapata matumaini na wananchi wetu wanapata moyo, wamefurahi sana; nimewajulisha kwamba, tumepata mkandarasi sasa mtulie umeme unakuja utekelezaji basi uwe ni ule ambao tunautarajia. Naomba hawa wakandarasi wawasikilize viongozi wanapowaelekeza anzieni hapa, wawe wasikivu sio wawe miungu watu, watusikie tunapowaomba *at least* yale maeneo ya vipaumbele wayafanyie kazi. Naomba haya malalamiko sasa yasirudierudie tena kwa sababu umeme ndio maisha ya Watanzania, umeme ni uchumi. Tunataka

twende kwenye uchumi wa viwanda, utawezekanaje bila umeme? Vijana wetu wana shughuli mbalimbali zinazohitaji umeme, kuchomelea, kunyoa, watafanyaje hizi shughuli bila umeme? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye umeme wa upemo Mkoani Singida, mradi huu una miaka zaidi ya sita hivi sasa na mkandarasi alishaweka kila kitu chake pale *field* lakini hadi sasa ameshindwa kupewa *go ahead* ya kuendelea kutekeleza mradi huu na unapita katika *vijiji* nane vya jimbo langu. Niombe sasa Waziri atakapokuja hapa *ku-wind up* atupe *commitment* ya kuanza kwa mradi huu ili angalau wananchi wa *vijiji* vile nane wapate matumaini ya kupata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huu umeme mkubwa unaotoka Namanga – Arusha – Singida, una *Kilowatt* 2000 ni umeme mkubwa ambao ungeweza kuondoa kabisa tatizo la umeme nchini lakini hadi sasa hatujajua muendelezo wake unakuwaje. Kwa hiyo, niombe pia Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa atupe *commitment* kuhusu eneo hili ili tupate umeme kwa uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nimuombe Mheshimiwa Waziri, mimi ninayeongea hapa Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini nakaa gizani umeme hamna nyumbani kwangu, Waziri haoni aibu? Nimeshamueleza mara kadhaa, nimeshamueleza hata *DG* wa *REA*, Meneja wa Kanda hata wa mkoa wameshindwa kunisikiliza. Jamani, sasa kama Mbunge hasikilizwi mwananchi wa *kijiji* kule atawenza kusikilizwa? Naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani. Mheshimiwa Edwin Enos Swalle atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kuungana na Wabunge wenzangu kutoa pongezi nyngi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na timu nzima ya Wizara hii. Hata mimi ni shuhuda ambaye nimekuwa nikiongea na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wamekuwa ni wasikivu sana.

Mheshimiwa Spika, Sera yetu ya Umeme inasema Umeme kila Kijiji. Hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaeleza idadi ya vijiji ambavyo bado kupata umeme lakini sisi katika Jimbo la Lupembe bado tupo kwenye shida ya kupata umeme kwenye ngazi ya kata. Zipo kata ambazo hazina umeme hata katika *level* ya kata, achilia mbali vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kata kama za Ukalawa, Ikondo, Mfiriga na Idamba, hakuna umeme. Maeneo haya palikuwa na mtu binafsi alikuwa na umeme unaitwa umeme wa Sefa ambapo watu wa Wizara waliwapa nafasi ya kutoa umeme kwa baadhi ya vijiji. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa sana ule umeme ambao ni wa Sefa kwanza ni wa bei ghali sana kwa sababu ni wa mtu binafsi, lakini pili umekuwa na changamoto nyngine, ule umeme hauna uwezo wa kuendesha hata mashine ya kukobo na kusaga.

Mheshimiwa Spika, viko baadhi ya vijiji kwa mfano sehemu za Image, ikifika jioni saa 02.00 wananchi wamerudi mashambani wakiwasha *TV* zao haziwezi ku-*operate* kabisa kwa sababu umeme hauna nguvu, hata redio za kawaida, *TBC* au redio ndani ya mkoa umeme huu hauna uwezo wa kuziendesha. Kilichobaki sasa wananchi hawa wanaendesha hizi mashine na redio kwenye sehemu za starehe kwa kutumia mafuta. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali katika karne hii ya 21 kwa muda ambapo tupo katika Sera ya Viwanda kuwa na jimbo ambalo hata umeme kwenye kata haujafika, hatutendi haki kwa wananchi hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Lupembe lina fursa nyngi za utajiri kwa ajili ya viwanda; Lupembe tunalima sana zao la chai kuna viwanda zaidi ya viwili vinahitaji umeme, Lupembe inalima sana matunda, hasa nanasi, wako watu

wengi wana nia ya kuwekeza kwenye nanasi maeneo ya Madeke lakini kwa sababu hakuna nishati ya umeme wanashindwa kuweka viwanda ambavyo vingetoa ajira nyingi sana kwa vijana wetu. Pia kulikuwa na fursa nzuri ya kuweka viwanda vya parachichi kwenye jimbo hili lakini kwa sababu ya changamoto ya umeme wawekezaji wengi hawaji tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naishauri sana Wizara ya Nishati pia kwenye maeneo ambayo kuna umeme wa *REA* kiasi kuna shida kubwa na mara kadhaa nimeongea na Naibu Waziri, Mheshimiwa Byabato kwamba umeme ambao upo umekuwa na wenyewe ni kero kuliko hata usingekuwepo. Wananchi wana mashine zao mfano, mteja amekuja kusaga unga kabla hujamaliza kusaga umeme umekatika. Kwa hiyo, mwananchi anashindwa kwenda kufanya kazi nyingine anasubirila mpaka umeme urudi na hajui unarudi saa ngapi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna wananchi wa mashine ndogo au viwanda vidogo vya kuranda mbao. Kuna msiba, inabidi watu warande mbao kwa ajili ya shughuli ya msiba, umeme unakatika. Kwa hiyo, tatizo la kukatika umeme kwa nchi nzima ni kubwa na namuomba sana Waziri kama walivyoongea Wabunge wengi humu ndani, hii ni shida kubwa ukiachilia mbali kupeleka umeme kwenye kila kijiji, lakini kuwa na umeme ambao hauna uhakika pia ni kero kubwa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wako wananchi wamepata hasara sana, wameunguza redio, kuna mwananchi wangu mmoja mpaka nyumba yake imeungua kwa sababu ya kero ya umeme kukatika. Kwa hiyo, nimuombe Waziri pamoja na sifa nyingi ambazo tumetoa kwenye Wizara yake lakini tatizo la umeme kukatika, kutotabirika, kutokuwa na nguvu, Wizara hii itoe kipaumbele wasiweke tu kipaumbele kupeleka umeme kwenye kila kijiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Enos Swalle. Sasa ni Mheshimiwa Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini na Mheshimiwa Daimu Mpakate ajlandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kupata fursa hii ndogo, tuko wengi tunagombania muda huu. Mimi nitajikita kwanza kutoa shukrani kwa Wizara hii na Serikali yetu lakini pia malalamiko kidogo kwenye jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano na ya Sita kwa mradi huu mkubwa wa *REA* na hasa hasa kueneza umeme nchi nzima. Vilevile kujandaa kuwa na umeme wa kutosha kwa kuleta miradi mingi ya kuzalisha umeme na baba yao ni Mradi mkubwa wa Mwalimu Julius Nyerere kule Rufiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara hii si kwamba ameivaa Mheshimiwa Kalemani, Mheshimiwa Kalemani ameivaliwa na Wizara hii. Mheshimiwa Kalemani Wizara hii anaichukua kama familia yake. Mimi kwangu tulipoanza uongozi hapa mwaka 2015 hapakuwa hata na kijiji kimoja chenye umeme jimboni kwangu. Kwa kujua hilo, huyu Waziri amekuja jimboni kwangu mara nane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tuna wilaya saba Mkoani Tabora. Kote mradi ulikuwa unaenda vizuri lakini Jimbo la Tabora Kaskazini halikuwa hata na kijiji kimoja chenye umeme, leo tuna vijiji 32 vina umeme. Alikuwa anasikiliza maoni ya wananchi wangu anatoka machozi, hili si jambo la kawaida kwa Waziri kuumia kama vile wale ni familia yake yeye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwaambieni alipita jimboni kwangu kuzindua umeme *REA* III sehemu ya pili siku saba kabla ya kumpoteza Mheshimiwa Rais aliyetangulia mbele za haki. Hii ni kuonyesha kiasi gani alikuwa na uchungu wa kufanya kazi akijua kwamba ana matatizo ya familia yake, lakini akaweka familia ya Watanzania wote mbele. Huyu ndio Waziri Kalemani nayetaka kumtaja leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, matokeo yake vijiji 12,000 vimepata umeme kutoka vijiji vichache vilivyokuwepo mwaka 2015 bado vijiji 1,900 na kitu basi nchi nzima iwe ya umeme. Ameitoa nchi hii kule chini kwa umeme leo ni nchi ya kwanza katika Afrika kuwa na umeme. Huyu ndiyo Waziri ninayesema Wizara imemvaa naye kaivaa Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu tuna vijiji 96 Jimbo zima, 32 vina umeme na 64 havina umeme. Hata hivyo, kwa imani kubwa niliyonayo kwa Mheshimiwa Waziri ameshakuja na kuzindua *REA III round II* pale kijijini kwetu Kanyenye na kutoa ahadi kwamba vijiji vyote vilivyobakia vimo katika *REA III round II* na wilaya yote ya Uyui imepewa vijiji 100 vitakavyopatiwa umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, licha ya hivyo tulikuwa tumbabakiwa na vijiji vitatu kujumuisha vijiji vyote vya Wilaya ya Uyui. Alipokuja tumeongea naye na wakandarasi wote tumekubaliana vijiji vile vitano vilivyobakia vimo pia katika mpango huu wa *REA III round II*. Kwa hiyo, mimi nina imani kwamba baada ya mwaka 2022 kama tunavyosema miezi 18 Jimbo langu na Wilaya yote ya Uyui itakuwa na umeme. Hili si jambo dogo, nimesimama hapa kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano na Awamu ya Sita kwa kazi nzuri inayofanya. Tusingoje mtu fulani afariki ndipo tumpongeze tunampongeza Mheshimiwa Kalemani yuko hai na anatusikia amefanya kazi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la usalama wa mitambo inayoitwa *Business Continuity Planning*. Mitambo hii inafanya kazi kila siku lakini lazima kuwe na mbadala wake. Tumepata tatizo sana la LUKU wiki tatu zilizopita ilipoanguka awamu moja walijonayo ya kuendesha mitambo hawakuwa na awamu ya pili jambo hilo limeleta mushkeli. Naomba waangalia kuwa na mitambo mbadala.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Almas Maige. Mheshimiwa Jumanne Sagini atafuatiwa na Mheshimiwa

Daimu Mpakate na Mheshimiwa Minza Simon Mjika ajiandae.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwenye sekta hii ya nishati. Nami niungane na wote waliompongeza Waziri, Naibu na timu yake kwa juhudini na kazi nzuri wanazozifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nitaomba kwa kweli niache yale ya kitaifa niende kwenye Jimbo la Butiama. Butiama ndiko alikozaliwa Baba wa Taifa na tunasema tunamuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kazi nzuri aliyowafanya Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Sisi tunaishukuru Serikali hususan Serikali ya Awamu ya Tano na Sita kwa kujitahidi kuona kwamba vijiji vyote vinafikiwa na umeme. Ninavyo vijiji 59 na kwa kweli vyote kwa tafsiri ya *access*, kufikiwa vimefikiwa. Changamoto tuliyonayo ni huko kufikiwa walikokuona wananchi na wote wanatamani wapate umeme. Wakati fulani mtani wangu mmoja aliwahi kuongea hapa kadri tunavyopanua huduma ndivyo watu wanavyotamani na ni kweli kwamba kila mtu sasa anataka apate umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pale Butiama pamoja na kuwa na vijiji 59, vyenye vitongoji 370 ni vitongoji 147 vilivyo fikiwa sawa na asilimia 40; vitongoji 223 havijafikiwa sawa na asilimia 60. Hata kwenye hivyo vijiji na vitongoji vyake unakuta wamegusa *center*. Kwa mfano, ninayo Kata moja maarufu ya Nyamimange, Tarafa ya Kiagata kuna vitongoji 10 lakini vitongoji vyenye umeme ni vitatu tu; Kiagata Madukani, Kewancha na Serengeti ndiyo vyenye umeme lakini vitongoji saba vifuatavyo Isangura, Kebwasi, Nyamihuru, Sania, Mtakuja, Masongo, Mamititu havina umeme na hali iko hivyo karibu kwenye vijiji vingine vyote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa hali kama hii haiwardhishi wananchi wanaona kama wameachwa lakini hali inakuwa mbaya zaidi pale taasisi za umma zinazohudumiwa wananchi wengi hazifikishiwi umeme kama hospitali, vituo vya afya,

zahanati na shule. Ni vizuri tukatambua tunapokwenda kwenye *REA* / / round / / wajue kwamba bado wana kazi kubwa sana huko Butiama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru juzi tumepeewa orodha ya majina ya wakandarasi watakaohudumia majimbo na wilaya zetu. Kwa Butiama sijui ni bahati mbaya au nini tumepeewa mkandarasi anaitwa *Giza Cable Industries*. Sasa nimemtafuta tangu juzi simu yake inasema haipatikani jina lenyewe walilochagua wala halitii matumaini. Bora angeita Nuru au Mwanga yeye kaita Giza na hapatikani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wengine wanalipia umeme lakini hawaunganishiwi, hili nalo ni tatizo mwenzangu amelisema asubuhi. Ninaye mwananchi hapa Mama Omari wa Kitongoji cha Kohoko kule Nyamikoma amelipia nguzo mbili Sh.551,147.32 tangu tarehe 10/04 lakini hawajasogeza nguzo wala hawajachimba mashimo na hakuna kinachoendelea wakiulizwa wanasema tatizo ni mita. Sasa kama tatizo ni mita walikuwa na sababu gani ya kumtaka mwananchi huyu alipie.

Mheshimiwa Spika, lipo hili tatizo la kukatikakatika umeme hili limesemwa na Wabunge wengi. Kule majimboni wameweka *ma-group* ya *WhatsApp* haya watu wanazungumza umeme unavyokatika mpaka wanatumia maneno yanayofedhehesha Shirika letu. Nakumbuka wakati fulani nikiwa pale Simiyu na hata Butiama naona yanaendelea mambo ya kukatika kwa umeme, wanasema umeme wa *TANESCO* unavyokatika utafikiri mwanamuziki Fally Ipupa.

Sasa nikajiuliza Fally Ipupa ni nani nilikuwa sijamjua, kwamba umeme unavyokatikakatika ni kama Fally Ipupa au wengine wana-*comment* yamekata umeme yaani badala ya wamekata wanasema yamekata umeme, yamerudisha, yamekata tena yaani namna umeme unavyokatika unakera wananchi mpaka wanasema utafiriki kuna mtoto anajifunza namna ya kuwasha na kuzima. Mheshimiwa Kalemani

tunajua unafanya kazi kubwa sana lakini tuombe wataalamu walioko mikoani na kwenye wilaya pengine hawatusaidii vya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naona nimepigiwa kengele basi mimi nishukuru kwa nafasi hii, naunga mkono hoja nikiamini kwamba haya niliyoyasea yatafanyiwa kazi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Sagini kwa mchango wako mzuri. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri itabidi kwenye maelezo yako uje ueleze watu wa Butiama umepeleka Kampuni inaitwa M/S Giza, sasa hii ipo au haipo. Mheshimiwa Kalemani ana kazi leo. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Mwanyika atafuatiwa na Mheshimiwa Boniface Butondo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akifanya.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri tunaambiwa sasa ni vijiji karibu 1,952 ndiyo bado havijapata umeme na katika *REA III round II*ndiyo vitapata umeme. Kwa Jimbo letu la Njombe tuna tatizo na nilishaonana na Mheshimiwa Waziri kumueleza matatizo ambayo tunayo. Njombe ni vijiji vinne tu ndiyo ambavyo vimeingia katika mradi wa *REA III round II*. Mheshimiwa Waziri alinihakikishia kwamba kulikuwa na makosa na kwamba vitajumuishwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri ametushauri hapa kwamba tuwasiliane na wakandarasi ili tuweze kujua *scope* ya kazi yao na wanafanya nini. Nimewasiliana na wakandarasi kama Waziri alivyosema lakini cha kusikitisha ni kwamba wakandarasi mpaka sasa *scope* yao ya kazi inafahamu hivyo vijiji vinne tu.

Mheshimiwa Spika, naelewa pengine kuna mchakato wa kubadilisha hiyo *scope* lakini nimuombe Waziri kwa niaba

ya wananchi wa Njombe awahakikishie kwamba vijiji vile 20 vyote vitaingizwa katika mpango huu.

Tunaomba sana asitupeleke kwenye *Peri-Urban Project* maana vijiji hivi ni vijijini kabisa siyo maeneo ya mijini kwa vile Jimbo la Njombe linaitwa Njombe Mjini. Vijiji hivyo ni kama vifuatavyo; Makoo, Ngelamo, Mamongolo, Lugenge, Kisilo, Kiyaula, Idihani, Utengule, Ngalanga, Uliwa, Igoma na kijiji ninachokaa mimi vilevile kina matatizo cha Makanjaula nacho hakina umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana Waziri atuangalie kwa jicho la huruma. Njombe *program* nzima ya REA I, II, III zote hizi kwa kiasi kikubwa sana zimekuwa *propelled* na Mkoa wa Njombe kwa sababu sisi ndiyo *supplier* wakubwa wa nguzo karibu zote ambazo zinakwenda katika *project* hizi zote. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuona Mheshimiwa Waziri na sisi anatuangalia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya pekee nimuombe Waziri, tuna Shule ya Sekondari Yakobi, *REA III round / uli-target* taasisi mbalimbali za afya na za elimu lakini kwa bahati mbaya sana shule hii ambayo ina watoto karibu 600 mpaka leo wako gizani. Tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kuiingiza shule hii nayo ili iweze kupata umeme katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la nishati jadidifu. Sekta madhubuti ya nishati ni ile ambayo ina mchanganyiko wa vyanzo mbalimbali nya umeme. Kwetu hapa tunaona kabisa kwamba kwa kiasi kikubwa umeme wa maji na umeme wa gesi ndiyo unachukua sehemu kubwa lakini tuna *potential* kubwa ya kuwa na umeme tofauti na huo au wa kuongezea kama umeme wa upepo au *solar*. Wawekezaji siyo kama hawapo lakini majadiliano na wawekezaji hawa yanachukua muda mrefu sana. Njombe tuna *potential* ya kuzalisha mpaka *megawatt* 150 kwa umeme wa upepo kama vile wenzetu wa Singida. Mheshimiwa Waziri ametuambia wanakwenda kufanya majadiliano na ni kweli wawekezaji tunajua wameshaitwa

kwa majadiliano lakini majadiliano haya yafike mwisho basi ili na umeme wa upepo nao uingie katika mpango wetu wa umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama muda utaniruhusu niongelee kidogo kuhusu mradi wa kusindika umeme wa gesi. Kwenye vitalu Na.1, 2 na 4 ndipo ambapo tunategemea kwamba mradi huu mkubwa wa *LNG* utajengwa au utapata *resource* yake ya umeme. Tuseme wazi Tanzania ina bahati kuwa na *endowment* kubwa sana ya gesi 57 *tcf* ni umeme mkubwa, ukiu-put kwenye *context* ni umeme ambao unaweza uka-power nchi ya UK kwa miaka 20 bila wasiwasi, kwa hiyo, ni umeme mwingi mno. Hata hivyo, suala siyo kuwa na *resource* ni namna gani *resource* hii sasa tunakwenda kuifanya ifanye kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kimoja katika *global scale* bado Tanzania hatupo hata katika *top twenty* wenye *resource* kubwa ya gesi. Kwa hiyo, wawekezaji ambao tunao kwenye sekta hii ni vizuri tukakamilisha mazungumzo hayo. Tunafahamu siyo kitu cha kukimbilia au cha kufanya haraka lakini tuseme kama alivyosema Mbunge mmoja hapa kwamba kwa kweli hatuna muda mwingi wa kupoteza.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Mwanyika. Mheshimiwa Boniface Butondo atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate.

**MHE. BONIFACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Kalemani pamoja na Naibu Waziri wake, niwapongeze pia na watendaji wote katika Wizara hii. Sababu kubwa kwa nini nampongeza Mheshimiwa Kalemani ni kwa namna ambavyo amekuwa mfano wa

kuigwa kwa Mawaziri na hasa katika jambo kubwa la kutusikiliza sisi lakini pia kufika kwa wakati katika majimbo yetu na kuona changamoto na matatizo yallyopo katika maeneo yetu. Kweli wewe ni kiongozi wa kuigwa na Mawaziri wengine ningependa waige mfano na mwenendo wa Kalemani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kishapu ina jumla ya vijiji ya 127 lakini vijiji 75 vina umeme na vijiji 52 bado vina tatizo kubwa la umeme. Hivi navyozungumza kata tano hazina kabisa umeme kati ya kata 29 hata Kata nakotoka ya Lagana. Kata hizo ni Lagana, Bunambiu, Mwasubi, Itilima na Masanga, hizi kata hazina kabisa umeme hata katika kijiji kimoja. Kwa hiyo, hili bado ni tatizo kubwa sana katika eneo langu. Naomba sana Wizara katika hii *REA III* Awamu ya Pili vijiji hivi vyote viweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri mwaka 2017 alijeza kufika katika Jimbo la langu katika Kata za Ukenyenge, Mwamashelle na bahati nzuri aliahidi kwamba maeneo hayo yatapatiwa umeme. Kata ya Mwamashelle nguzo zimefika lakini mpaka sasa hatujapata umeme, kwa hiyo, bado wananchi wanasubiri umeme. Mimi ninahakika kwa jinsi ambavyo Waziri ameahidi atakwenda kutekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto kubwa ya kukatika umeme katika Mji wa Munze ambao ni Makao Makuu ya Wilaya yangu ya Kishapu, liko tatizo kubwa na kwa kweli jambo hili linasikitisha. Pengine wakati una-*wind up* naomba ueleze tatizo ni nini kwa sababu maelezo yako mengi. Kwa kutwa nzima umeme unapatikana kwa wastani wa asilimia 30 ama 40 asilimia 60 unakatika; kwa siku unaweza ukakatika mara tatu, mara nne ni tatizo kubwa sana. Tunaomba kujua tatizo ni ni linalosababisha kukatika kwa umeme katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni masuala mazima ya watumishi. Wilaya ya Kishapu tuna watumishi 12 peke yake na Mheshimiwa Waziri

anafahamu watumishi katika sekta hii muhimu ni kubwa. Pale inapotokea *emergency*, kwanza katika *emergency gang* inatakiwa watumishi 12 waende haraka kwa ajili ya kutatua tatizo sasa unapokuwa na watumishi wilaya nzima 12 panapotokea *emergency* unafanya nini pia kuna maeneo yanayotakiwa kutolewa huduma za kila wakati, kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie suala zima la wakandarasi. Nchi nzima wakandarasi wametolewa katika kila wilaya, Wilaya ya yangu ya Kishapu haijapata mkandarasi, hili ni tatizo sijajua sababu ni nini. Wakati Mheshimiwa Waziri ana-*wind up* aeleze nini tatizo. Nimeendelea kufuatilia mchana huu Mkoa mzima wa Shinyanga hatujapata wakandarasi. Kwa hiyo, hili bado ni tatizo na pengine nataka nipate majibu tatizo ni nini. Juzi Waziri alisema atakapowaita hao wakandarasi pamoja na mameneja wa *TANESCO* kutoka katika kila wilaya atawapa maelekezo wawasiliane na Waheshimiwa Wabunge ili waweze kuona maeneo gani ambayo yana changamoto na ya kufanya kazi kwa haraka, kwa hiyo, kwangu hili ni tatizo kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie pale panapotokea matatizo ya moto. Mwezi Machi palitokea tatizo la kuungua nyumba tatu katika Kata ya Mwaweja Wilayani kwangu Kishapu kutokana na *short* za umeme. Tumepata tatizo kubwa sana kuzima moto katika nyumba zile lakini pia hata *TANESCO* wenyewe kuwahi kufika ilikuwa ni tatizo kubwa. Tatizo hili limechangiwa pakubwa sana kutokana na kutokuwa na magari na watumishi wa kutosha. Kwa hiyo, naomba sana mjaribu kuitizama Kishapu na watusaidie ili tuondokane na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu. Sasa ni Mheshimiwa Daimu Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi nichangie kwenye Wizara hii ya Nishati. Naungana na wenzangu waliowapongeza Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaongelea *point* mbili ambazo ni muhimu kwa Wilaya ya Tunduru na Jimbo la Kusini kwa ujumla. Moja, nashukuru kwa kuletewa mkandarasi, Wilaya ya Tunduru ina vijiji 157 lakini kati ya hivyo 83 havina umeme. Kwa kuwa mkandarasi amekuja basi tunaomba ajitahidi kazi hii ianze mapema, maana ilitakiwa ianze mwezi wa tatu huu ni mwezi wa sita naamini ndani ya mwezi ujao ataanza kazi ili kukamilisha hivyo vijiji 83 ambavyo havina umeme kabisa.

Mheshimiwa Spika, katika hivyo vijiji 83 Jimbo la Tunduru Kusini kuna Kata 10 ambazo hazina umeme kabisa, ziko gizani. Kuna Kata ya Nalasi Mashariki na Magharibi, Mchoteka, Marumba, Mbati, Mtina, Mchesi, Lukumbule na Masakata pamoja na Misechela. Kata hizo zote hazina kabisa umeme, kwa hiyo tunaomba mkandarasi afanye chini juu aweze kuwahi kufanya kazi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili nitazungumzia suala la kukatika kwa umeme Wilaya ya Tunduru. Sisi tuna majibu, kwa hiyo, namuomba Waziri ayafanyie kazi majibu ambayo tumeyaona. Tunashukuru Serikali imeleta umeme Gridi ya Taifa lakini umeme ule kutoka Songea mpaka Tunduru ni kilometra 265 Kv 33, kwa hiyo, umeshindwa kuhimili vishindo. Umeme huo huo unaenda mpaka Mang'aka, Masasi mpaka Nachingwea kilometra 600 Kv 33. Kwa hiyo, majibu tuliyoyapata ni kwamba tunatakiwa tuweke *substation* pale Tunduru na Masasi ili ku-*boost* umeme uweze kufika kwa kiwango kili ambacho kinatakiwa, lakini bado mnatakiwa muongeze ile nguvu kwa maana kutoka Kv 33 mpaka kufika Kv 132. Jambo hili limekuwa ni kero kubwa sana Tunduru, umeme unakatika kila siku na kila wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tunduru inapita Namtumbo, Namtumbo ina barabara mbili; ina barabara

inayopita Namtumbo Mjini na ina barabara inayopita Lusewa ambako nako umeme umekwenda basi ikiwezekana mfanye utaratibu wa kuweka *line* mbili za kupeleka umeme Tunduru ambao unaenda moja kwa moja mpaka Masasi na Nachingwea. Mkatumia *line* ya Lusewa, Nalasi, Mbesa mpaka Tunduru Mjini ili iweze kufanya kazi ile ambayo imekusudiwa. Kwa hiyo, naomba sana suala hili mliangalie, mtuwekee *extention* nyingine ya *line* ambayo itaenda Tunduru kuititia Nalasi ili ihakikishe kwamba inaleta umeme ule na usumbufu unapungua kwa asilimia kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala la gesi. Kwa kweli kwa taarifa ya Wizara magari 700 yanayotumia gesi ndani ya miaka mitatu ni madogo sana. Naomba tuweke mkakati mahsus, hasa sisi Wabunge walete wale wataalam watufungie yale matanki ya gesi ili magari yetu yatumie gesi kwa sababu ni gharama nafuu sana.

Nawashauri *TPDC* waweke kituo cha gesi hapa kwa ajili ya kujanza kwenye magari ya Wabunge pamoja na wananchi waliopo Dodoma ili kupunguza adha hii ya kutumia mafuta ya *diesel* na *petrol*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii itatusaidia moja, kuongeza mauzo ya gesi na pili itawapunguzia watumiaji gharama ya kutumia mafuta ya *petrol* pamoja na *diesel*, haya yatusaidia sana. Wenzetu Dangote kama ulivyozungumza wale wana magari 600, mpaka sasa magari 250 tu tena maroli ndio yanatumia gesi. Hili ni jambo nzuri sana na ni funzo kwa Serikali kutumia magari yanayotumia gesi ili kuhakikisha tunatumia gesi kwa uadilifu zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda tuliangalie ni suala la *LNG* pale Lindi. Kwa kweli suala la *LNG* ni kizungumkuti na ni la muda mrefu, naomba sasa mhakikishe ila kazi inaanza kwa maendeleo ya watu wa Kusini ili watu wa Mtwarara na Lindi waone kwamba gesi yao inathaminiwa na ule mradi unaanza kwa sababu

utatupatia fedha nyingi sana kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mbunge wa watu wa Tunduru.

Nina wawakilishi wawili wa Balozi Norway ambaao wako kwenye *gallery* ya Spika pale, kwanza Ndg. Neema Shayo, Mshauri wa Masuala ya Nishati. Neema ahsante na karibu sana. Wa pili ni Ndg. Børge Romsloe, yeye anashughulika na Masuala ya Nishati ndani wa Ubalozi wa Norway hapa nchini. Karibuni sana. (*Makofii*)

Nilimtaja Mheshimiwa Maimuna Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix. (*Makofii*)

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Nishari.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nitoe pongezi nyingi kwa Waziri mwenye dhamana ya Nishati pamoja na watendaji wake wote. Pia niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuasisi suala la mradi wa umeme vijiji ni kwani umepunguza kwa kiasi kikubwa sana kero ya umeme ambayo ilikuwa inavikumba vijiji vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Jimbo la Newala Vijiji. Wote tunajua kwamba umeme ni ajira, biashara, ulinzi lakini pia ni afya. Jimbo la Newala Vijiji lina jumla ya vijiji 107, kati ya vijiji hivyo ni 54 tu ndiyo vyenye umeme, vijiji 53 havina umeme sawa na asilimia 49.53. Kuna Kata sita katika hivyo vijiji 53 ikiwemo Kata ya Chitekete ambayo Mbunge mimi natoka haina umeme niko gizani. Kata nyingine ni Nakahako, Mpwapwa, Nandwahi, Mkoma 2 na Nambali, kata hizi hazina kabisa umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ujazilizi wa vijiji vile ambavyo mradi wa *REA* umepita. Mheshimiwa Waziri una kazi kubwa ya kufanya kwa sababu kama walivyotangulia kusema katika vijiji ambavyo umeme umepita vingi wanauona umeme umekaa kama kamba ya kuanikia nguo, haujashuka kwenye nyumba za wananchi. Ukienda Kata ya Mdimba inahesabika kwamba ina umeme lakini Mdimba pale ambapo ndipo Makao Makuu ya Kata umeme haujashuka kabisa na ni kero kubwa wanasumbua kila siku. Tunashukuru tumepeata mkandarasi, niombe sana Mheshimiwa Waziri msimamie kwa karibu kwa sababu hali iliyopo inahitaji usimamizi *otherwise* ile miaka miwili ambayo tumejjipangia kwamba vijiji vyote vitakuwa vimepata umeme kwa hali iliyopo Newala Vijiji tunaweza tusifanikiwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunamshukuru Mwenyezi Mungu Mtwara sasa ameshusha neema ya madini. Tumesikia kuna *graphite* kule Chiwata ambayo na mimi pia inanigusa kwa namna moja au nyingine. Ili mradi ule uweze kufanyiwa kazi vizuri tunahitaji umeme wa uhakika. Kulikuwa na mpango ule wa kujenga *power station* ya *megawatt* 300 pale Mtwara, tunaomba wakati unakuja kuhitimisha hoja yako utuambie mpango hule umefikia wapi kwa sababu kupitia mpango ule tutakuwa na uhakika kwamba umeme wa kutosha utapatikana na miradi mingine mikubwa ya maendeleo kama viwanda pamoja na machimbo vitaendeshwa bila bugudha yoyote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia na mimi niongelee suala la kukatikakatika kwa umeme, hali ilikuwa mbaya sana kwa Mkoa wa Mtwara lakini niishukuru Serikali illifanya juhudu kubwa sasa hivi umeme unakatika lakini nafuu hipo. Watu wa *TANESCO* Makao Makuu, watu wa Kanda, *TANESCO* Wilaya waliweka kambi kuhakikisha kwamba tatizo la kukatika kwa umeme katika Mkoa wa Mtwara linapata ufumbuzi.

Kwa hiyo, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba tulikwambia suala hilo na wewe ukalifanya kazi na tunashukuru ulikuja ukaona ile hali ukatuma hiyo timu ikaja kuhakikisha kwamba suala la kukatikakatika kwa umeme basi

linaisha Mkoani Mtwara. Niendelee kukuomba juhudziendelee kufanyika ili kukomesha kabisa suala la ukatikaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini. Nilishakutaja Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix na tafuatiwa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Felix hayupo.

**SPIKA:** Basi Mheshimiwa Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Msalala naomba nichangie hotuba ya bajeti hii ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja nianze kwa kumpongeza Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika Taifa letu hili la Tanzania. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Mheshimiwa Waziri Kalemani kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika nchi hii ya Tanzania na *Deputy* wake kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Nitakuwa mchoyo wa fadhila bila kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kuchangia katika maeneo matatu. Nianze kuchangia katika suala nzima la *REA*. Mheshimiwa Waziri nikuombe suala la *REA* hili katka Jimbo langu la Msalala na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu leo yule wa Zanzibar ametutania hapa kwamba mradi wa *REA* katika Jimbo langu la Msalala Mheshimiwa Waziri bado na wewe mwenyewe ni shahidi. Pia sijui ni kwa nini Jimbo

langu la Msalala na Mkoa mzima wa Shinyanga tumekuwa na bahati mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mbunge mwenzangu hapa tuna vijiji 92 katika Jimbo la Msalala lakini vijiji 63 bado havijapatiwa umeme. Siyo hilo tu hata mradi wa umeme jazilishi kwa maana ya *desentification* katika baadhi ya maeneo bado haujasambaa kwa uhakika. Nimuombe Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili tuweze kuambatana kwenda katika Jimbo la Msalala tuweze kuzindua miradi mbalimbali inayoendelea, lakini pia tufike katika maeneo yenye changamoto za umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu na maeneo mengine ya Mkoa wetu wa Shinyanga ukosekanaji wa umeme unapelekea kuhatarisha ndoa za kina mama. Akina mama wanajitahidi sana kupika wali na kuhakikisha umenyooka lakini unakuwa ni bokoboko kwa sababu wanatumia mbinu ya kutwanga badala ya mashine za kisasa za umeme ambazo zitachambua mchele vizuri na kuwapelekea kupika wali ambao utapelekea kudumisha mapenzi ndani ya ndoa. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri chondechonde fika Jimbo la Msalala tuone namna gani tunaenda kuanzisha umeme katika Kata za Jana, Mwalugulu, Mwakata na kata zingine zote zilizoko katika Jimbo la Msalala. Kwa kufanya hivi utanusuru ndoa za kina mama. Nikuombe baada hapa twende tukanusuru ndoa hizo za kina mama wa Jimbo la Msalala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie changamoto ya umeme katika uwekezaji. Katika Jimbo la Msalala wengi wetu ni wawekezaji katika sekta ya madini, tunategemea umeme ili shughuli hizi za uchimbaji ziweze kufanikiwa. Waziri alitoa maelekezo kwamba katika Kata ya Lunguya, Kijiji cha Nyangarata maeneo yote yenye machimbo wapeleke umeme. Nashukuru Mheshimiwa Waziri tayari umeme unaelekeea katika Kijiji cha Nyangarata, lakini bado Ntambarare umeme haujafika. Haya maelekezo unayatoa huku Mheshimiwa Waziri watendaji wako hebu jaribu kuyafatilia wanayapuuza, ulisema utakapotoka waanze

kupeleka umeme mara moja katika Kijiji cha Ntambarare Segese katika Kata ya Segese. Mheshimiwa Waziri hebu tusaidie kwa sababu ukuaji wa sekta ya madini katika Jimbo langu la Msalala tunategemea nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kumekuwa na changamoto ya gharama. Wawekezaji wengi wanalia kwa sababu ya changamoto ya gharama na gharama hiyo ni *KVA charges* kama *penalty*. Unapoenda kuwekeza hao wateja wakubwa kuna gharama ambayo huwa inatozwa kama *penalty* kwa wawekezaji hawa na gharama hiyo inapelekea kuleta changamoto kubwa katika uwekezaji. Leo hii mtu analipa gharama ya umeme mathalani shilingi milioni 40, lakini hapo anapigwa *penalty* kwa ajili ya matumizi ya umeme wa ziada ambao yeye hautumii. Niilombe Wizara hebu jaribuni kuona ni namna gani sasa mnaenda kutupunguzia *charges* hizi na ikiwezekana mziondoe ili ilete unafuu kwa wawekezaji wetu katika maeneo hayo ya migodi na viwanda vikubwa katika Jimbo la Msalala. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni namna gani mnawenza kuimarisha ugawaji wa *transformer* katika maeneo mbalimbali katika Jimbo langu la Msalala lakini pia katika maeneo mengi nchini kote. Nimekuletea *concern* za wafanyabiashara wengi ambao mpaka sasa viwanda vimesimama kwa sababu ya ukosefu wa *transformer*. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri bajeti hii itakapoenda kupita uone namna gani unaenda kuimarisha suala zima la usambazaji wa *transformer* kwa wafanyabishara wetu hawa katika maeneo yale ili na wao waweze kuendeleza viwanda vyao hivyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi hii, ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, poleni sana kwa ndoa hizi kupata matatizo lakini unaweza ukamuita Mchungaji Gwajima aende akaone nini cha kufanya huko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Kavejuru nimekuona, utafuatiwa na Mheshimiwa Kasaka Masache.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kumpongeza Waziri wa Nishati na Naibu wake na viongozi wote wanaoshirikiana kwa utumishi wao uliotukuka, Mungu awabariki sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikushukuru wewe binafsi kwa kuniona lile la vinasaba kurudi kwenye *TBS* na Wabunge wote wakaamua litungiwe sheria. Hili ni jambo jema na la ukombozi kwa uchumi wa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mchache, naomba niende moja kwa moja kwenye changamoto za umeme katika Mkoa wa Kigoma. Umeme ndiyo ufunguo wa maendeleo ya viwanda na ni uhai wa maendeleo ya jamii. Mkoa wetu mpaka sasa haujaungwa na Gridi ya Taifa na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati amesema hapa kwamba ifikapo 2023, Mkoa wetu utakuwa umeungwa na Gridi ya Taifa na hilo limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu. Kuna vituo viwili vya kupozea umeme, Kituo cha Nguruka na Kidahwe. Nilikuwa nawasiliana mchana huu, je, ile *site* ambayo ilipendekezwa kijengwe kituo cha kupozea umeme kuna shughuli yoyote inayofanyika, jawabu ni kwamba hakuna chochote kinachoendelea na muda unaendelea kusonga mbele. Watu wa Kigoma tumekaa kwenye giza kwa muda mrefu, watu wa Kigoma wanaasili ya kufanya kazi sana, tuna mazao ya kimkakati ya michikichi ambapo mwaka kesho tunahitaji tuwe na viwanda, tunaomba tuungwe kwenye Gridi ya Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Jimbo langu la Buhingwe, namshukuru Waziri na mkandarasi ambaye alitupa amesonga mbele, lakini naomba kasi iendelee kwa kuweka umeme kwenye Vijiji vya Janda, Murungu, Changwe, Kilelema na vingine vyote viliviyobaki ili na sisi pale pafunguke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri ustawi wa Taifa lolote ule utategemea maendeleo yaliyopo lakini ukiwa unaongezwa na kukuzwa na tafiti. Nimshauri Waziri wa Nishati awekeze kwenye utafiti kwa kuwa kule Uganda pamekwishagunduliwa mafuta kwenye Ziwa Albert na wataalam wa miamba wanasesma kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu ambapo sisi Tanzania ni matajiri yawezekana tuna hazina kubwa ya mafuta na gesi basi utafiti uendelezwe na kuwepo mtaji wa kuweka kwenye tafiti ili tafiti ziendelee na tuendelee kubaini utajiri amba Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Huyo ni Mbunge mpya wa Buhigwe Mwalimu Kavejuru Eliadory Felix akishusha mambo yake hapa ndani ya Mjengo. Karibu sana Mheshimiwa Kavejuru na umeanza vizuri, umewakilisha jimbo hasa. (*Makofii*)

Sasa Mheshimiwa Njelu Masache subiri kidogo, tusiondoke Kigoma haraka, hebu Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda kwanza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kunikumbuka na kuniona na hasa baada ya kuzungumza ndugu yangu Mheshimiwa Kavejuru.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme wa Gridi ya Taifa katika Mkoa wa Kigoma ni ajenda ya mkoa, ni ajenda ya Wabunge wote hata wengine amba ni Mawaziri hawawezi kusema lakini ni ajenda yetu. Hii ni kwa sababu kama mnavyojua Kigoma ni mionganini mwa mikoa ya pembezoni na ambayo imechelewa sana katika maendeleo na moja ya jambo lilituchelewa ni kukosa umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo tunapozungumzia changamoto za umeme tunazungumzia mafanikio makubwa yaliyofanyika kutohana na kazi iliyofanywa na Wizara hii. Kwa hiyo, nimpongeze sana Waziri, Naibu Waziri pamoja na

watumishi wote wa Wizara hii na mashirika kama *TANESCO* na watu wa *REA*, kwa kweli tunazungumza changamoto zinatokana na mafanikio. Sisi zamani huko Kigoma ilikuwa umeme ukiwaka maana unaweza ukawaka hata mara moja kwa wiki ukiwaka unasikia watu wote eee, utafikiri labda Timu ya Wananchi imeingiza goli kwenye nyavu za Simba. Yaani wala hili sikudanganyi... (*Makofi/Kicheko*)

**MBUGE FULANI:** Rudia

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, yaani ukisikia kelele wakati ule ilikuwa sababu ni mbili; ni Yanga kafunga goli kwenye lango la Simba au umeme umewashwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kumshauri Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwamba pale Kigoma mmeingia mkataba na wale wawekezaji wa *solar* ili wazalishwa umeme wa *megawatt* 4.8 mpaka sasa wanazalisha *megawatt* 2. Tatizo la wale wawekezaji ni kwamba ule mradi wao ulichelewa kuanza ukakumbana na misukosuko mingi hata mlipokuja kukubaliana na kuingia mkataba baadhi ya vifaa vilikuwa vimeibiwa. Kubwa kuliko yote hizo *megawatt* 2 zinapatikana mchana tu ikishaingia saa moja jioni ni zero, umeme haapatikani kabisa kutoka kwa watu wale wa *solar*. Kwa maana hiyo wanachosaidia pekee ni kupumzisha mashine za *TANESCO* mchana ili ziweze kuwaka usiku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la pale inaonekana vifaa vyote; *panel, inventor, step-up transformer* viro sawasawa lakini hawana zile betri kubwa za *ku-store energy*, kwa hiyo, inapofika usiku hawezi kuzalisha chochote. Kwa sababu mmeingia mkataba na mnawalipa naomba wapeni hata *government guarantee* wakope benki waweze kuweka mradi wa vizuri. Sisi tukipata ile *megawatt* 4.8 tatizo letu sisi Wilaya ya Buhigwe na maeneo mengine linakwisha kabisa kabisa. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri muone jinsi ya kusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hebu chukueni utaratibu kama wanaouchukuwa TAMISEMI au Wizara ya Afya, wanapofika mahali wakaamua kuna hospitali ya shirika la dini wanaitumia kama Hospitali ya Wilaya basi hupeleka madaktari wa Serikali kusaidia *supervision* na kutoa huduma. Hebu kwenye kituo hiki kwa vile mmeingia mkataba na wale watu peleka mainjinia wako wa *TANESCO* wasaidiane na wale watu pale kuhakikisha kwamba kazi inakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizingumza ni kwenye nishati ya mafuta, tofauti ya bei kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine. Leo hii asubuhi nimefuatilia Dar es Salaam lita moja ya *petrol* shilingi 2,249, lita ya *diesel* ni shilingi 2,073 lakini Kigoma leo hii lita ya *diesel* ni shilingi 2,481 tofauti ya shilingi 232 na Dar es Salaam sasa hapa ukinunua lita 1,000 tu kuna tofauti ya shillingi 232,000, gharama za uzalishaji lazima zitakuwa kubwa kwa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtu ambaye namuamini sana Mheshimiwa Waziri, hebu ajaribu kuangalia hivi hatuwezi kuwa na bei moja ya *petrol* na *diesel* kwa nchi nzima. Ni jambo ambalo linawezekana, mkaona wapi pakufidia tukawa na bei moja, ukienda Kigoma, Mbeya au sehemu nyingine kila sehemu iwe moja.

Mheshimiwa Spika, la mwisho limezungumzwa suala la vinasaba hapa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati mbaya muda hauko upande wako.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana lakini kwenye vinasaba nilitaka tu kumsaidia ndugu yangu pale aliyekuwa anaomba ulinzi kwamba mimi nimeshamuandalia ulinzi kule Kigoma asiwe na wasiwasi. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, umechokoza mwenyewe kwenye mchango wako, ningekuongezea dakika moja lakini sasa umeharibu mwenyewe uliposema kuhusu ushangiliaji wa Kigoma. Sasa nimtaarifu tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwamba kule Mwanza Ruvu wamepigwa tatu bila. Sasa hivi ni mwendo wa tatu-tatu kuelekea tarehe 3 Julai, yaani ni tatu, tatu. (*Makof/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mashache Njelu Kasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu sana inayogusa wananchi wengi. Kwanza niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri lakini kwa mipango mizuri sana illyokuwepo kwenye Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia tushukuru kwa namna ambavyo tumepata namba za wakandarasi ambao wanaenda kujenga umeme wa *REA III* na sisi wananchi wa Chunya kwa namna yake kwenye kata zote 20 tunaenda kupata umeme katika kata zote. Umeme huu utaenda kufika kwenye Vijiji cha Lupa Market, Kambi Katoto, Sipa, Lualage, Mwigi, Liheselo, Bitimanyanga, Mazimbo, Kalangali, Magunga pamoja na Shoga. Sasa hapa Chunya tutaenda kuwa tumewaka vizuri. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaenda kufanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri anayofanya Waziri bado kwa Wilaya ya Chunya tuna changamoto ya umeme mdogo ambao unafika ndani ya wilaya yetu. Kwa kuwa tunaenda kupeleke umeme mwangi kwenye vijiji vyetu changamoto hii Wizara iweze kuichukua na kuitatua kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya ya Chunya kama tunavyofahamu uchumi wetu mkubwa tunategemea uchimbaji kwa hiyo tuna viwanda vingi vidogovidogo

ambavyo vinachenjua dhahabu maarufu kama *co-elution*. Viwanda hii vinazidi kujengwa kila siku umeme ambao wanautumia ni umeme mkubwa, sasa inafikia hatua watu wengine wanashindwa kutumia umeme huo inabidi wawashe majenereta ili kuweza kukidhi mahitaji ya umeme ambayo yanahitajika. Naomba tuone namna ambayo ni nzuri zaidi kuweza kuongeza umeme wa msongo mkubwa uweze kufika kwenye Wilaya yetu ya Chunya ili mahitaji haya yaweze kuwafikia wananchi wetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia umeme huu ambao unatoka kwenye kituo cha Mbeya unafika Chunya lakini pia unaenda wilaya jirani ya Songwe ambapo kule kuna mgodi mkubwa sana wa Shanta. Mgodi huu na wenyewe bado wanatumia umeme ambao unapita Wilaya ya Chunya, kwa hiyo, inafikia hatua umeme huu haukidhi mahitaji ya wananchi wa Wilaya ya Chunya. Kwa hiyo, naomba kama ikiwapendeza na bajeti ikiwepo tuweze kujenga *power station plant* pale kwenye Mji wa Makongorosi ili sasa umeme huu uweze kugawiwa vizuri kwenye Miji ya Chunya, Mkwajuni, Lupa mpaka Kambi Katoto ili sasa kuweza kukidhi mahitaji vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na vijiji hivi kupata umeme lakini pia tatizo kubwa tunalo kwenye *REA* awamu II, vijiji kadhaa viliweza kupata umeme lakini umeme ambao uliweza kufika ilikuwa takribani kilometra moja au moja na nusu, kwa hiyo, wananchi hawa walikuwa wanaonjeshwa tu ule umeme. Unakuta kwenye kijiji kuna nyumba 20 mpaka 25 ndizo zilizopata umeme, wananchi wengi wameomba na wamelipia lakini mpaka sasa hivi bado hawajaweza kupata umeme. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana naomba tuone namna bora xaidi kushughulikia suala hili. Pamoja na mambo mazuri yanayoendelea tuweke bajeti ya kutosha ili vile vijiji ambavyo vilikuwa havijaweza kufikiwa kwa maana kuongeza kwenye mitaa umeme huo ziweze kufikiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna vijiji ambavyo vilikuwa kwenye mradi wa *TANESCO* havikuwa kwenye mradi wa *REA* kama Igundi, Sangambi, Godima pamoja Itumbi.

Mradi huu ulianza zaidi ya miaka mitatu na nusu iliyopita toka 2018/2019 nguzo zimefika kwenye vijiji hivi lakini mpaka leo umeme haujaweza kuwaka. Kwa hiyo, tulombe Wizara kuona namna ambavyo tunaweza tukapata vifaa kwa maana ya *transformer* pamoja na mita ili sasa wananchi wale waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, vijiji nilivyovitaja hapa ni vikubwa lakini umeme haujaweza kuwaka na kuna baadhi ya vitongoji vimepata lakini vijiji havijapata. Kwa hiyo, malalamiko ya wananchi yamekuwa makubwa na wanaanza kuona kama Serikali hii haiwajali. Kwa hiyo, niombe sana wakati Mheshimiwa Waziri ana *wind-up* aone namna iliyokuwa bora zaidi na hivi vijiji pia viingizwe kwenye mpango ikiwezekana kwenye hii *REA* !!! ili na wao waweze kunufaika na umeme huu na baadaye waweze kuona matunda mazuri zaidi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.  
(*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka. Nilikutaja Mheshimiwa Jafari Chege na utafuatiwa na Mheshimiwa Self Gulamali.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi. Kabla sijasahau kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya.

Mheshimiwa Spika, nami niendelee kusisitiza kwamba *Giza Cable Industry* huyu mkandarasi ambaye amepewa kazi katika Wilaya nne za Tarime, Serengeti, Butiama pamoja na Rarya, mkandarasi huyu kama alivyo sema Mheshimiwa Sagini hapatikani kwenye simu. Sisi kama wakazi wa Mkoa wa Mara kwenye hizi wilaya nne tunapata wasiwasi kwa sababu kama wakandarasi wengine wamekwishaanza kufanya *survey* lakini ye ye mpaka sasa hapatikani. Leo asubuhi nilikuwa naogea na Injini wa Wilaya yangu Rarya anasema hajaona

mkandarasi yeote maeneno yale. Kwa hiyo, kama Bwana Giza ananisikia popote alipo basi ni vema tukafanya mawasiliano ili angalau atuondoe kwenye adha hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nishauri mambo mawili ambayo yako ndani ya jimbo langu. La kwanza ni kushukuru kwa kazi kubwa illyofanyika katika Jimbo langu la Rarya, ndani ya vijiji 87 vijiji 73 vyote tayari vina umeme wa *REA*. Ni imani yangu kwa Viji 14 vilivyobaki vya Kanyamsana, Kabache, Nyamusi, Masike, Nyabikondo, Burere, Wamaya, Nyabihwe, Nyihara, Bugendi, Busanga, Ulio, Tai pamoja na Lalanya navyo vitapata umeme. Ni imani yangu utekelezaji wa *REA* awamu hii vijiji vyote vitakuwa vimepata umeme.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu Mheshimiwa Waziri atatusaldia pia kutatua kero kwenye maeneo ambayo tayari ndani ya vijiji 73 hivi ambavyo umeme umefika ili angalau maeneo mengine waweze kupata umeme. Kwa sababu hiyo Mheshimiwa Waziri nishauari maeneo mawili, ni kweli umeme umefika kwenye vijiji 73, lakini kwenye kijiji kuna kaya au wakazi wako 20 kwenye *center* ya Kijiji, unaweza ukaona kwamba kama wako watu 20 ni nyumba tano tu ndizo zinazopata umeme lakini nyumba 15 hazina umeme. Sasa kwa *status* ya Rarya jinsi ilivyo katika hizo 15 bado unakuta watu 10 tayari wamelipia umeme zaidi ya mwaka mmoja lakini hawajaunganishiwa umeme. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba wananchi wengi pamoja na kwamba tunawaambiwa ndani ya kijiji chenu wana umeme hawaoni tija ya umeme ule.

Mheshimiwa Spika, atakuambia tu Mheshimiwa Mbunge ninachoona ni nguzo mimi nimelipia nina miaka miwili au mwaka mmoja sijapata huo umeme. Zile kaya tano zilizosalia wanashindwa kulipia kwa sababu wanaona wenzao mpaka sasa hawajatatuliwa tatizo lolote la umeme. Nikuombe Mheshimiwa Waziri kipindi unakimbizana na namna ya kutatua changamoto ya vijiji vilivyosalia nchi nzima tupeleke fedha *TANESCO* ili wakimbizane kumalizi hivi vijiji vilivyosalia ili hawa watu 15 waliosalia na waweze kupata

umeme katikati ya kijiji kwenye maeneo ya *centre*. Kwa kufanya hivyo utakuwa umetatua tatizo zima la eneo lile.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nizungumzie kuhusu kukatikakatika kwa umeme. Mimi kwangu ni changamoto kubwa sana, naweza nikawa naongoza kwenye Mkao wa Mara kwa Jimbo la Rorya kukatika umeme. Changamoto kubwa ni ukubwa wa kilometa za mraba ambazo *TANESCO Halmashauri* ya Wilaya ya Rorya wanazohudumia. Watu hawa wanahudumia zaidi ya kilometa 344, kutokea Nyamongo mpaka ndani ya jimbo zima ni zaidi ya kilometa 344.

Mheshimiwa Spika, lakini ukifuatilia historia ya umeme ule nguzo zina zaidi ya miaka 40 kwa hiyo zimechoka na kuchakaa. Pamoja na kwamba utakuja kutoa majumuisho na kutoa mwelekeo wa nchi nzima ni kwa nini umeme unakatikatika lakini *solution* kubwa ni kupeleka fedha za kuboresha miundombinu kwenye maeneo haya. Hizi nguzo za umeme zina miaka 40 sasa kwenye maeneo ambayo kuna chemchem zinaoza halafu zinadondoka ndiyo maana mpaka leo ninavyozungumza kuna maeneo ndani ya jimbo langu watu wana siku tatu hawana umeme. Hivi ninavyozungumza kuna Kijiji cha Chabakenye toka jana mchana hakuna umeme wowote lakini ukifuatilia unakuta miundombinu hii imechakaa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna yoyote hata kama Mheshimiwa Waziri atafanya marekebisho ya watendaji mimi niseme kwamba inawezekana hawana wakawa hawana kosa. Kikubwa ambacho anaweza kufanya ni kupeleka fedha ya miundombinu hasa fedha *maintenance* kwenye maeneo haya ambayo umeme unakatika mara kwa mara. Pamoja na kwamba atakuja na suluhisho lingine lakini aamini nachosema umeme huu kwa maeneo haya nguzo zina muda mrefu sana toka zimeoteshwa. Akitatua hilo pamoja na mengine atakayokuja nao naamini kwenye halmashauri hizi ambazo ziko pembezoni atakuwa amewaokoa kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege. Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Januari Makamba ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Binafsi niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa waliyoifanya kwenye sekta hii ya umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme kwenye nchi yetu ndani ya vijiji vya Tanzania kumeifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza Afrika kusambaza umeme vijijini. Tanzania tumesambaza umeme kwa zaidi ya asilimia 90, kwa Afrika tumeshika nafasi ya kwanza kwa kuweka umeme kwenye vijiji vyetu. Ni jambo zuri, la kupongezwa na kwa kweli Mawaziri hawa wanastahili pongezi na pongezi hizi ni haki yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto zilizopo za kukatika kwa umeme karibu nchi nzima. Tumuombe tu Waziri na timu yao wajipange kwa sababu tatizo la ukatikaji wa umeme lipo karibu katika kila eneo hata Igunga na sehemu nyingine. Kwa hiyo, pamoja na kupeleka umeme kwenye vijiji karibu vyote nchi nzima lakini uimara au *stability* ya umeme imekuwa ni tatizo.

Kwa hiyo, tuwaombe waliangalie suala hili kwa umakini mkubwa ili kuondoa tatizo la ukatikaji wa umeme katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, Igunga maeneo mengi ni majoruba, nguzo zile zinawekwa kwenye majoruba kila siku ni *service*. Kwa hiyo, kwa sababu Serikali iko kwenye *project* ya kutengeneza nguzo za zege, naomba zipelekwe kwenye maeneo ambako kuna majoruba kwani hizi nguzo za mbao hazina uhimilivu. Kwa hiyo, niwaombe walifanyie kazi suala hili kwa umakini zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka nichangie ni la vinasaba. Kwanza niipongeze Serikali kwa kulichukua suala hili na kulipeleka Serikalini na kuliondoa kwa wakandarasi ambao walikuwa wamejipa kazi hii. Hizi zilikuwa ni kampuni mbili za tajiri mmoja; mmoja anauza *materia*/kwa kampuni nydingine na kampuni nydingine inaiuzia Serikali au inafanya kazi ya kuweka *marking* kwenye mafuta. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini vinasaba? Tulikuwa tunaweka vinasaba kwenye mafuta yetu kwa sababu sisi ndiyo *port* tunapokea mafuta ya ndani ya nchi yetu na nchi jirani. Kwa hiyo, mafuta haya yanapoingia unashindwa kujua ya kwetu ni yapi na ya nchi jirani ni yapi. Kwa hiyo, ili kuondoa ukwepaji wa kodi ndiyo vinasaba vikatumika kuwekwa kwenye mafuta tunayotumia ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kulikuwa kuna ujanja mwiningi ukifanyika katika suala hili la uwekaji wa vinasaba. Mafuta mengine ambayo yalikuwa yakienda *transit* yalikuwa yanatumika ndani ya nchi na wanaweka vinasaba na maisha yanaendelea na wafanyabiashara wanapata pesa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala hili limepelekwa ndani ya Serikali, umakini na uzalendo mkubwa sana unahitajika ili kuondoa ubadhirifu na ujanjaujanja utakaokuja kutokea kwa watumishi wa Serikali ili kuondoa ukwepaji wa kodi kwa wafanyabiashara kwenye sekta hii ya mafuta. Niombi sana Waziri wa Viwanda, *EWURA* isimamie na isishirikiane na watumishi ambao siyo waadilifu. Ni lazima hapa tukubaliane, pamoja na kuiondoa kwa wakandarasi tumerudisha Serikalini, uzalendo unahitajika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri tumechukua watumishi wale tumewaingiza Serikalini kwa ajili ya kutuongezea ujuzi lakini pia ndio waliokuwa wanafanya kazi hii. Ni lazima tuwafuatilie kwa ukaribu Zaidi, tusiliache jambo hili hivi hivi. Pamoja na wao kufanya tusiache liende tu ni lazima tuwafuatilie ili kudhibiti mianya ya upotevu wa kodi ya Serikali.

## TAARIFA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nakuruhusu, taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba asubuhi ya leo nimekwenda kuweka mafuta hapa Dodoma yameongezeka kwa Sh.80 kutoka Dar es Salaam kuja hapa, yaani siku hizi ni kila siku mafuta yanaongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukitaka kutazama suala hili na mimi naliangalia mara mbilimbili; duniani kote mafuta hayatumiki kwa sababu ya Corona maeneo mengi biashara hazifanyiki, mafuta mengi sasa hivi yamekwama kule yanakuja huku ndani lakini Tanzania mafuta yanaongezeka bei, nadhani kwa sababu ya vinasaba, mimi nina mashaka nalo hili. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, anachokisema Mheshimiwa Getere ni kweli; kuna ongezeko la haraka na kubwa sana la bei ya mafuta hivi sasa. Labda Mheshimiwa Waziri atatuambia baadaye kidogo tatizo ni nini. (*Makofii*)

Endelea Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa naipokea lakini kwa uelewa ni kwamba kila tarehe za mwanzo za mwezi mpya *EWURA* wanapanga bei mpya kulingana na bei ya soko la dunia. Ila nachoomba ni kwamba waangalie bei hizi zisije zikaathiri mzunguko wa uchumi wa nchi yetu. Kwa mfano, bei iliyopanda juzi kwa Dodoma hapa ilikuwa ni Sh.1,800, ime-shoot mpaka Sh.2,300. Kwa hiyo, ni kiwango kikubwa sana cha upandaji wa bei. Niziombe Wizara hizi kwa sababu najua bei zinapangwa na watu wa *EWURA* na *EWURA* iko Wizara ya Maji...

## TAARIFA

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, endelea hapo ulipo.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpe taarifa Makamu Mwenyekiti wa Kamati inayohusika kwamba mfumo huu wa kuagiza mafuta wa Tanzania umerejewa kwenye bei za dunia na bei zetu ni mwezi tuliomo toa mwezi uliotangulia.

Kwa hiyo, kadri bei za dunia zitakavyopanda, sisi ni *price taker*, hatuna ujanja lazima tufuate kanuni bei ipande au ishuke. Hata hivyo, bei hupanda na bosi wangu wa zamani anajua, kuna *contango* na *backwardation*. Kwa hiyo, sisi *price taker* hatuna ujanja.

**SPIKA:** Japo hatuna ujanja lakini ile *trend* ni ya ghafla na ni kubwa mno, ndio maana kwa binadamu wa kawaida atahitaji maelezo fulani tu. Mkiangalia hivi karibuni bei imepanda sana, tukiambiwa ni *World Market* nalo ni jibu pia lakini ni vizuri kujua kuna nini kwa sababu zimepanda sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Gulamali, malizia.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, mwisho katika mchango wangu, naomba kuzungumzia usimamizi wa *flowmeter* yetu. Naomba ikiwezekana pale tujenge ukuta kama wa Mererani, tuweke ukuta na kufuli kubwa na funguo wapewe Waziri na Katibu Mkuu ili kulinda wizi na uchezeaji wa *flowmeter* pale bandarini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi, nawasilisha mchango huo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa ushauri wako. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, aliye kuwa anaongea ni Mheshimiwa Seif Gulamali, Meneja wa Timu ya *Bunge Sports Club*. (*Makofi*)

Kesho kutwa *Bunge Sports Club* itacheza na *TBC*, mechi ambayo itakuwa *live*, kwa maana kwamba itatangazwa. Niwaonye *TBC* kwamba siku hiyo ya Jumamosi wajia ndae kwa tatu bila. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Sebastian Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa January Makamba.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nianze kwa neno la shukrani kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake. Ni kweli Mheshimiwa Waziri ni mtu rahimu. Mimi niseme hadharani kwa zaidi ya mara mbili nillipokuwa na udhuru na yeye alipotembelea jumbo langu, alifikia hatua ya kupiga simu akaniunganisha na wananchi wangu. Huyu ni mtu muungwana, namshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba shukrani nyingine ziende kwako wewe. Bunge liliopita uliunda Kamati Teule ya Bunge ya kukushauri kuhusu suala la gesi na mimi nilikuwa mmoja kati ya Wajumbe uliowachagua. Rai yangu ni nini? Naomba Serikali iendelee kufanya rejea kwenye taarifa ile kubwa na kuona ni mambo gani tulioishauri Serikali. Nashauri sana katika hilo. Katika masuala yote ya gesi ujumbe mzima uko pale, kwa hiyo Serikali iendelee kufanya rejea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho Waziri alikuwa Uganda wakati Rais wetu na Rais wa Uganda walipokuwa wakitia saini moja ya mikataba. Nilijifunza mambo kama matatu na mambo hayo yalinifanya nipate vivu lakini vivu ambaao ni chanya. Rais Museveni alisema mafuta ni jambo la kupita tu, linaweza likawa jambo la muda, lakini utajiri huo uwasa idie kwenda kufanya sekta nyingine kama kilimo, utalii na mambo mengine ya namna hiyo. Pia aliwasimamisha vijana akasema ugunduzi ule umefanywa na Waganda wenyewe, vijana ambaao waliwapeleka shule wakasoma.

Akasema pia eneo ambalo limechimbwa ni asilimia 40 bado asilimia 60. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi suala hili limenitia vivu wa maendeleo. Watananza tunajifunza nini kutoka hapa? Je, tuna mpango gani wa makusudi wa kuhakikisha vijana wetu ama kupitia shule au na mambo mengine kwa sababu wao watakuwa na uzalendo kufanya kazi hizi? Mtu mwengine anaweza akaenda kufanya utafiti hapa na akakuta labda kuna mafuta na kwa sababu ya masuala ya kiuchumi asikupe taarifa sahihi lakini kwa wale ambao ni wazalendo, kama walivyofanya wale vijana wa Uganda hawatafanya hivyo. Naomba tuendelee kujifunza kutoka kwa wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua kuna maeneo kama Eyasi, Wembele ambapo Jitihada zinaendelea lakini twende mbali zaidi. Sisi kule Tanganyika, kwa maana ya Mkoa wangu wa Katavi, utafiti umekuwa ukiendelea katika bonde lile. Ni vizuri basi tukaongeza kasi ya kuendelea kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo nirudi tena kwa Mheshimiwa Waziri. Pamoja na sifa nilizokupa za kutembelea maeneo yangu, changamoto ambayo naipata mimi katika eneo langu, nasomeka niko Manispaa lakini umbali wa kijiji cha mwisho watu wa TANESCO wanasema wao ndiyo watashiriki na siyo suala la REA wakati huo wale watu wanasonic wako kijijini. Kwa mfano, ukienda Kata ya Mwamkulu, japo inasomeka mitaa lakini ni vijijini; maeneo kama Mkwajuni, Kabwaga, Mkokwa, Nguvumali na Seso. Ninayo pia Kata ya Kasokola maeneo ya Kasolwa, Ivungwe na Isungamilia.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninalo eneo la Kakese, kuna eneo linaitwa Kamakuka. Mheshimiwa Waziri, ni shahidi, mara ya mwisho alikuja pale na akatusaidia kuhakikisha umeme unafika hata kwa maeneo yale yanayowagusa wachimbaji. Katika hilo mimi nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo napenda kulizungumzia tuliambiwa ongezeko la mapato liliwa ni pamoa na suala la LUKU. LUKU ilivyokuwa ikitumika vizuri ilifanya TANESCO wafanye vizuri. Tuliambiwa mara ya mwisho kulikuwa na shilingi bilioni 72 katika mwaka 2016 kwa mwezi, lakini mwaka 2021 ilikuwa shilingi bilioni 160 kwa mwezi na hii yote ilikuwa asilimia 102. Sasa kama LUKU ilisababisha TANESCO wakapata matokeo mazuri na kipato kikapanda, hii juzi tumeona LUKU ikichezewa; wanataka kuleta ujumbe gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nakushukuru kwa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa January Makamba.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii. Nami nitumie nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya. Sisi kwetu katika Jimbo la Bumbuli tuna changamoto za vijiji vingi ambavyo havina umeme, lakini nimeongea na viongozi wa REA na Wizara na wametoa ahadi kwamba maeneo yote ambayo hayana umeme yatafikiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya leo kwenye Wizara hii ni suala la nishati ya kupikia. Nishati ya msingi kuliko zote ni nishati ya kupikia. Kila nyumba kunapikwa na kila siku kunapikwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mahitaji ya nishati hapa nchini unaweza usiwe na umeme wa kupigia pasi au wa kuwashaa taa au wa kupooza vinywaji lakini lazima utafute nishati ya kupikia. Kwa hiyo, tunapozungumza suala la nishati kama wawakilishi wa wananchi hatuwezi hata siku moja kuacha kuweka mkazo na msisitizo wa nishati ya kupikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania asilimia 92 ya Watanzania wanatumia nishati inaitwa tungomotaka (*biomass*), yaani kuni na mkaa kupikia. Naomba nirudie; asilimia 92 ya Watanzania wanatumia kuni na mkaa kupikia.

Ukichukua matumizi yote ya nishati katika shughuli zote hapa nchini iwe mafuta, gesi, *hydro* bado nishati ya tungomotaka (*biomass*) kwa maana ya kuni, mkaa, pumba na kadhalika ni asilimia 80, inashinda hata mafuta yote kwenye magari na mitambo na inashinda *hydro* zote. Naomba nirudie; ukichukua *total primary energy consumption* hapa nchini, *energy* zote tulizoweka kama mitambo na kadhalika bado *energy* ya tungomotaka ndiyo inaongoza. Ushauri wangu kwa Wizara, nafahamu iko Sera ya Nishati, lakini kutokana na ukubwa na umuhimu wa *biomass* (tungomotaka) yaani kuni na mkaa, lazima kuwe na sera tofauti ya kutusaidia kama Taifa kuendesha eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, thamani ya mnyororo wa biashara ya mkaa hapa nchini ni kubwa kuliko thamani ya *export* za mazao yetu yote; ni kubwa kuliko kahawa, chai au korosho. Thamani ya mnyororo wa mkaa, *value chain* ni karibu dola bilioni moja, siyo biashara ndogo. *Revenue* ya mkaa Dar es Salaam peke yake mwaka jana ilikuwa ni karibu shilingi bilioni 800; hii ni sekta kubwa mno ambayo kama Serikali na kama Wizara hatuwezi kuipuuza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuna hoja kwamba tunasambaza umeme vijijini ili tunusuru misitu ili umeme utumike kupika. Mji unaoongoza kwa usambazaji wa umeme hapa nchini ni Jiji la Dar es Salaam, asilimia karibu 96 ya Jiji la Dar es Salaam lina umeme. Hata hivyo, mji unaoongoza kwa matumizi ya mkaa hapa nchini ni Dar es Salaam ambapo asilimia 70 ya mkaa wote unaotumika Tanzania unatumika jiji moja. Kwa hiyo, kwa hoja hiyo, itachukua muda mrefu sana kwamba huu umeme tunaousambaza ndiyo utuokoe kutoka kwenye matumizi ya mkaa na kuni. Kwa hiyo, zinahitajika jitihada za makusudi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inasemekana mkaa ni nishati ya wanyonge. Ni kweli lakini si kweli; humu Wabunge wengi na viongozi na watu wenye uwezo mzuri wa fedha wanunua mkaa, lakini wanunua kwa gunia, wanyonge wanunua kwa kopo. Kwa hiyo, ukipiga hesabu, chakula ambacho nimetumia mimi kwa mkaa wa 70,000, mnyonge anakuwa

ametumia kwa 180,000 kwa sababu ananunua kwa kopo.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa suala la kuni na mkaa na nishati ya kupikia limekaa maeneo mengi. Biashara ya mkaa inadhibitiwa na *TFS* (Wakala wa Misitu Tanzania) ambaao ipo Wizara ya Maliasili na Utalii; Sera ya Nishati ya Nishati ambayo inahusika na mambo ya nishati ya kupikia iko Wizara ya Nishati; masuala ya hifadhi na mazingira yapo Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa hiyo, naamini kwamba huu mkanganyiko na mtapakao wa udhibiti wa jambo hili muhimu ukifanyiwa kazi vizuri, basi tunaweza kupata manufaa.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama viongozi wa wananchi katika jambo ambalo tunaweza kuwatendea haki Watanzania ni kuhakikisha kwamba tunaondoa umaskini wa nishati, unaitwa *energy poverty*.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa January Makamba kwa hoja yako nzuri na muhimu. *(Makofi)*

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbushia baadhi ya Kata katika Wilaya ya Ludewa ambazo hazina umeme, kama Kata ya Ibumi, vijiji 28 Wilaya ya Ludewa havina umeme. Kata ya Milo, Ibumi, Kilondo, Ludende, Lumbila, Mkongobaki na

Munford Wilaya ya Ludewa hakuna umeme. Tarafa ya Mangali Ludewa kwa baadhi ya maeneo hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ilione hili, ituletee umeme Ludewa maeneo yote. Wilaya ya Ludewa Kata ya Lugarawa vijiji 20 havina umeme; na Kata ya Mawengi vijiji vinane havina umeme. Tunaomba umeme.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchangia kuhusiana na gesi ya Mtwara, Baada kuanza kwa mradi wa kuchimba gesi Mkoani Mtwara ni matumaini ya watu wa mikoa ya Mtwara na Lindi wawe wa kwanza kunufaika na mradi huu, lakini sasa ni kinyume chake. Mfano, mradi wa gesi majumbani unaanza kutekelezwa Mkoani Dar es Salaam na Pwani na kuiacha mikoa ya kusini Lindi na Mtwara inakotoka gesi. Jambo hili siyo jema hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kata ambazo hazina umeme kabisa katika Wilaya ya Liwale ni pamoja na Kata za Mpigamiti, Mlembwe, Lilombe, Ngongowele, Mkutano, Kimambi, Mbaya, Barikiwa, Miriwi na Nahoro. Ningetamani kwa awamu hii Kata ya Mpigamiti ingekuwa ya kwanza, Kata anakotoka Mbunge kuko kiza, ni aibu isiyovumilika.

Mheshimiwa Spika, naanza mchango kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya kusimamia majukumu ya Wizara hii hasa kwenye Mradi wa *REA*. Hata hivyo, hakuna mafanikio pasipo na changamoto. Ziko changamo kadhaa katika utekelezaji wa mradi huu wa *REA*.

Mheshimiwa Spika, mfano katika Jimbo langu la Liwale bado umeme huo haujafika katika vijiji vingi. Wilaya ya Liwale yenye Kata 20 na Vijiji 76 kuna Vijiji 34 tu vilivyofikiwa. Tatizo kubwa ni Wakandarasi, wamekuwa wakitoa visingizio vya kushindwa kufikisha vifaa kutokana na ubovu wa barabara. Jambo ambalo halina ukweli, kwani ziko taasisi

nyingi zinafanya kila siku na kupeleka bidhaa mbalimbali. Hapa naomba Mheshimiwa Waziri atembelee Liwale kuona uhalisia wa miradi ya *REA* katika Jimbo langu, bado mahitaji ni makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, umbali wa kutoka Nachingwea hadi Liwale ni zaidi ya kilometra 230. Hivyo basi, *line* ya umeme imekuwa na changamoto nyingi sana kama vile nguzo kuanguka na kuungua moto. Pia kutohana na umbali uliopo, unahitaji pia *substation* kwa ajili ya kuongeza nguvu ya umeme. Kwani umeme unaofika Liwale tayari unaonekana kuwa na nguvu ndogo.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuwapatia Watanzania umeme takriban nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo letu la Mchinga, tuna maeneo kadhaa ambayo hayajafikiwa na umeme. Maeneo hayo ni Kijiji cha Ruvu (Kata ya Mchinga), Kijiji cha Dimba(Kata ya kilolambwani), Kijiji cha Matapwa(Kata ya Mipingo), Kijiji cha Mnyangara (Kata ya Mipingo), Kijiji cha Lihimilo (Kata ya Mipingo)na Kijiji cha Namkongo (Kataya Mipingo).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza sana Waziri wa Nishati na Naibu wake pamoja na jopo la wataalamu wa Wizara kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye kuipeleka nchi yetu kwenye Tanzania ya Wiwanda kwa mchango wao mkubwa kwenye sekta ya umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudu kubwa zinazofanywa na Serikali, bado wananchi wengi wa Jimbo la Moshi Vijijini hawajapatiwa nishati ya umeme kupitia mradi wa umeme vijijini (*REA*).

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 inaelekeza kwamba kufikia 2025, vijiji vyote Tanzania vitakuwa vimeunganishiwa umeme. Upatikanaji wa umeme vijiji utachochea kuboreka kwa maisha, ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira kama zile za kuchomelea vyuma, gereji, maduka, *salon* za kunyoa na kutengeneza nywele na mabanda ya kuonyesha mpira.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na ahadi hii, ninaiomba Wizara ya Nishati isaidie kutatua changamoto za nishati ya umeme katika Jimbo langu la Moshi Vijiji. Kukosekana kwa umeme katika baadhi ya vijiji na vitongoji jimboni kwangu kunawafanya wananchi kuingia gharama kubwa ya kununua mafuta ya taa kila siku ili waweze kupata mwanga nyakati za usiku.

Mheshimiwa Spika, maeneo yenyе changamoto ya umeme Jimbo la Moshi Vijiji ni katika Kata ya Kindi, Kijiji cha Chekereni Weruweru, Vitongoji vya Miembeni, na Kisiwani havina umeme kabisa. Mbunge ametokea Kata ya Kibosho Kirima. Katika Kijiji cha Boro kwenye Vitongoji vya Boro Katni Boro Juu (anakotokea Mbunge), *voltage* za umeme ni ndogo sana na hupelekea kushindwa kuendesha vifaa vya ndani kama friji na vyombo mbalimbali vya ndani. Mashine za Welding (kwenye vitongoji hivi) na pump ya kuvuta Maji Masoka Sekondari hushindwa kufanya kazi kutokana na umeme mdogo. Shule hii ina wanafunzi zaidi ya 800.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali wameshindwa kuweka mashine za kusaga unga, mashine za kutengeneza matofali na miradi mingine midogo inayohitaji umeme wa uhakika. Wanafunzi wa bweni wa Sekondari ya Masoka hushindwa kupata huduma ya umeme ili wajisomee usiku kutokana na umeme mdogo. Umeme huwaka kuanzia saa 5.00 usiku. Naomba Wizara isaidie kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Okaoni, Vijiji vya Sisamaro, Omarini na Mkomilo vinahitaji kuanganishwa japo baadhi ya maeneo nguzo zimepita ila bado kuanganishwa. Kata ya Kibosho Mashariki inahitaji huduma. Katika Kijiji cha

Sungum Vitongoji vya Kyareni na Nkoitiko havijaunganishwa. Katika Kijiji cha Singa, Kitongoji cha Singa Juu hakijaunganishwa. Katika Kijiji cha Mweka, Kitongoji cha Mweka Juu na Omi havijaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kibosho Kati, baadhi ya maeneo ya Kijiji cha Uri hakijaunganishwa. Kwa ujumla, katika vijiji vya Otaruni na Uri, kuna changamoto ya ukosefu wa umeme kwenye baadhi ya Vitongoji. Pia kuna tatizo la umeme kidogo (*low voltage*) kwenye vijiji hivyo. Tunaiomba Serikali iweke Transfoma za kutosha ili kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Uru Mashariki, Kijiji cha Materuni, Kitongoji cha Wondo hakijaunganishwa. Walichimba mashimo kwenye baadhi ya maeneo na kuleta nguzo tokea mwezi wa Tisa mwaka 2020 na hawajarudi tena. Katika Kata ya Mbokomu, Kitongoji cha Mmbede Kyaroni, Tema na Masanga na baadhi ya maeneo ya Korini Kati havijaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mabogini sehemu ambazo hazijapata umeme hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

(1) Vitongoji vya Sanya “*Line A*” na Mjohoroni vilivyopo katika Kijiji cha Mabogini.

(2) Kitongoji cha Uru, katika Kijiji cha Muungano;

(3) Katika Kijiji cha Maendeleo, Vitongoji vya Mshikamano na Uarushani;

(4) Mgungani katika Kijiji cha Mtakuja;

(5) Katika Kijiji cha Mserekia, hakuna umeme katika Vitongoji vya Mbeya kubwa, Mbeya ndogo, Remit, Mkwajuni na Mafuriko. Vilevile Kijiji cha Mji mpya, Kitongoji cha Utamaduni hakijaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mabogini wapo wananchi waliofanya *wiring* lakini *surveyor* hawaji kukagua ili waruhusiwe kulipia; pilii, wapo wananchi ambao wamesharudisha *form* na hawajaitwa kwenda kulipa ili wawashiwe umeme. Tunaiomba Wizara ifuatilie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Old Moshi Magharibi Kitongoji cha Salingo katika Kijiji cha Mandaka mnono hakina umeme kabisa. Kata ya Kimochi Kitongoji cha cha Kiwalaa kilichopo Kijiji cha Sango, Kitongoji cha Iryaroho kilichopo katika Kijiji cha Mowo na Kitongoji cha Maryaseli katika Kijiji cha Lyakombila havina umeme.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo niliyotaja hapo juu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha umeme wa kutosha unapatikana katika maeneo yote ya Jimbo la Moshi Vijiji. Hili litafanikiwa ikiwa Wakandarasi watalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vilevile, naishauri Serikali iwe na programu ya kuwaelimisha wajasiriamali wa vijiji kuhusu fursa zilizopo vijiji, na ni kwa namna gani wanakijiji wanaweza kutumia nishati hii kujajiri na kuongeza thamani ya bidhaa zao?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanywa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera bado una vijiji vingi ambavyo havina umeme. Je, ni lini Miradi ya REA III, Mradi wa ujazilizi na wa *Peri-urban* takamilishwa au kuanzwa lini Mkoani Kagera?

Mheshimiwa Spika, Wilaya nyingi hazikuunganishwa kwenye *grid* ya Taifa. Tunatumia umeme wa Uganda. Umeme

huu umekuwa kero kwa wananchi kwani unakatika katika kila mara. Je, ni lini Serikali itarekebisha hayo matatizo ili wana Kagera wapate umeme wa uhakika?

Mheshimiwa Spika, Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano, akiwa kwenye mkutano wa hadhara pale Bukoba Manispaa, alisema anampatia jukumu Naibu Waziri wa Nishati ahahakikishe matatizo ya umeme yanaisha kabisa Mkoani Kagera. Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Me Spika, hoja yangu ni kuhakikisha tunajumuisha umeme wa jua ili kuongeza nguvu kwa *TANESCO*. Kule Iringa kuna mwekezaji ameshaainisha eneo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Jimbo la Kalenga, Kijiji cha Kilambo. Naishauri Serikali iweze kuharakisha katika kuidhinisha mradi huu uanze, kwani utasaidia siyo tu kutoa ajira, bali kuharakisha maendeleo. Ahsante.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya. Pia niendeleee kuwapongeza kwa kuwaagiza Wakandarasi wawe wanawasiliana na Waheshimiwa Wabunge. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Lushoto lina Kata 15 na baadhi ya Kata, umeme umepita maeneo ya barabaranii tu. Kwa hiyo, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Lushoto. Hata hivyo, namshukuru Waziri kwa kutoa maagizo yake ya kuhakikisha vijiji vyote vya Jimbo la Lushoto vipatiwe umeme. Wasiwasi ni Wakandarasi: Je, watafanya hivyo kweli? Kama hivyo ndivyo, naomba niorodheshe vijiji vyangu vyote ambavyo havina umeme kabisa, pamoja na vitongoji vilivyo rukwa.

Mheshimiwa Spika, hivi ndiyo vijiji ambavyo havina umeme kabisa. Gare, Yamba, Kongei, Masange, Boheloi, Kwemashai, Ngulu, Miegeo, Handei, Milungui, Kireti,

Kwemakame, Mazumbai, Ntambwe, Kigumbe, Bombokamgobolo, Kilole, Mbelei, Mavului, Mazashai, Kigulunde, Mdando, Kweulasi, Bwaya, Kwetango, Bombo na Ngulwi Chumbageni.

Mheshimiwa Spika, hivi ndiyo vijiji ambavyo havina umeme kabisa. Pamoja na hayo, kuna Vitongoji zaidi ya 27 navyo vimerukwa. Kwa hiyo, naomba Serikali ivipatie Vitongoji hivyo vilivyorukwa na umeme ili kuepuka malalamiko ya wananchi waliokosa umeme na wakati huo huo wanauona umeme unawaka kwa jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, wananchi wa Lushoto wana uwezo mkubwa wa kuweka umeme, lakini wanakwamishwa na watu wa *TANESCO*, kwa kuwaambia umeme bado ni shilingi 177,000. Hili suala linawakatisha tamaa wananchi wa Lushoto. Kama hivyo, basi nalomba Serikali toe waraka wa kutoa bei elekezi kwa wananchi ili kuepuka usumbufu kwa wananchi wanaoupata kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi, Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, kiuchumi, kidiplomasia na kisiasa. Kama Taifa tuendelee kusema ahsante sana Mungu wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hasan, Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania kwa kupokea uongozi wa Taifa letu kwa amani na utilivu. Ninamwombea baraka, ulinzi na mafanikio makubwa kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawaombea watendaji na wateule wote wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mwenyezi Mungu

awajalie mafanikio mema katika utume wao Taifa letu lipate kufikia malengo makuu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania kuendelea kuwaombea Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano na Watanzania wote waliotangulia mbele ya haki kwa Mwenyezi Mungu awapokee katika Ufalme wake usio na mwisho. Kwa kweli kama Taifa mchango wake utakumbukwa daima. Kwa vielelezo hivi, Bwawa la umeme, *SGR*, *Busisi Bridge*, Bomba la Mafuta na mengine mengi sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kuitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii ya Nishati. Kwanza Wizara kuitia Mpango wa *REA* /// unaoendelea, ije na mkakati wa kuwatambua walengwa kwa kuwa wako wateja wengi sana waliofanya uwekaji wa waya katika makazi yao lakini umeme haujaunganisha.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ugumu wa utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri katika Jimbo langu la Mbulu Mjini kuitia ziara zake mbalimbali katika Jimbo letu. Kwa kauli ya watendaji wa *TANESCO* na *REA* kuwa hawana fedha, mifano hiyo iko katika Kata za Murray 2016, 2018, Gunyoda, Nahasey 2018 hadi sasa umeme haujaenda, hali iliyotupa wakati mgumu kuomba kura za CCM wakati wa Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2020.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maeneo mengi ya vijijini kuwa na uhitaji mkubwa wa nguzo na nyaya za umeme, Serikali iangalie uwezekano wa kufanya uhakiki wa maeneo hayo ili kupeleka kifaa cha utayari (UMETA) wakati majengo yakiendelea kuongezeka. Hivyo basi, naomba kauli ya Serikali kuhusu hali hii umeme kwamba utaenda lini?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya, lakini zaidi usikivu wenu. Binafsi kila nilipoomba kuonana na Mawaziri au Watendaji kuanzia Katibu Mkuu, *DG* wa *REA* na *TANESCO* kwa kweli nimepata nafasi na nimesikilizwa na shida za wananchi wa Mafinga zimepata walau suluhisho,

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nina ushauri na mambo kadhaa kwa Wizara. Hoja yangu ya siku zote ni kuhusu kuona uwezekano wa kuwa na Wilaya mbili za Kitanesco katika Wilaya ya Mufindi kutokana na umuhimu wake, hasa katika dhana nzima ya uchumi wa viwanda.

Ushauri wangu ni kwamba tuwe na ofisi kwa ajili ya Mafinga ambako kuna viwanda vingi vya mazao ya misitu na tuwe na Ofisi Mufindi ambako kuna viwanda vingi vya chai pamoja na Kiwanda cha Karatasi Mgololo. Ninaamini hata mapato, Mufindi inazidi baadhi ya mikoa. Hivyo kusogea huduma hii haitakuwa mara ya kwanza. Kwa mfano, llala ina zaidi ya Wilaya moja ya Kitanesco.

Mheshimiwa Spika, transforma zinazofungwa Mafinga za KV 50 ni ndogo ukilinganisha na uhitaji hasa wa viwanda vya mazao ya misitu. Maombi yangu; umeme ni huduma na ni biashara/mapato, ni kwa ajili ya uzalishaji, hivyo kuwekeza nguvu kwenye maeneo kama Mafinga itasaldia kuongeza mapato ambayo yatatumika kusambaza umeme maeneo ambayo umeme ni kwa ajili ya huduma zaidi. Kwa hiyo, iwe ni ujazilizi au *REA* / / awamu ya pili, ipo kila sababu maeneo kama Mafinga kuyaangalia kwa macho mawili na kwa jicho la uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu taa za barabarani. Tayari Halmashauri ya Mafinga Mji, imeshawasilisha andiko kadri ambavyo *DG* wa *REA* alituelekeza. Hivyo kwa umuhimu ule ule ambao Serikali ilikubali mazao ya biashara ikiwa ni pamoja na nguzo za umeme kusafirishwa masaa 24, tunaomba taa za barabarani katika maeneo ambayo ni *junction* za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, lingine ni Luku. Sina utaaliam wa masuala ya *IT*, lakini nashauri kwamba kama teknolojia inaruhusu, basi mtu anaponunua umeme asilazimike tena kwenda kwenye mita kuingiza *token*. Iwe kama ving'amuzi ambapo ukinunua tu inaji-*update*. Naomba kuwasilisha.

**MHE. OTHUMAN HIJA JUMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukuwa fursa hii kutoa shukurani zangu kwako kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hii ni mionganini mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimae kuiwasilisha katika Bunge lako Tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo. Kwanza ni kuhusu sekta ndogo ya umeme na hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Napenda kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyofanya jitihada kubwa ya kutafuta vyanzo vya umeme vya kila aina. Vyanzo vyote ni muhimu sana na vitasaidia katika upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi unaonesha kuwa umeme wa gesi ni rahisi sana ukilinganisha na vyanzo vingine. Hivyo, ushauri wangu kwa Serikali katika suala hili ni kuharakisha matumizi ya chanzo hiki ili kuwarahisishia maisha wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mradi wa kuzalisha umeme wa Ruhudji. Mradi huu ni mkubwa sana ambao unazalisha MW 358 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji. Mradi utajengewa laini yenye urefu wa kilometra 170 yenye mkondo wa 400kv. Urefu wa kilometra 170 ni mrefu ambao bila ya shaka laini itapita kwenye vijiji kadha katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba wapitie shirika letu la *TANESCO* na kuweka vituo vya kupoza umeme (*substations*) katika maeneo yatakayopitiwa na *line* hii ili wananchi wa maeneo hayo yaweze kufaidika na umeme huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA BAKARI YUSSUF:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Kalemani kwa kazi kubwa na ngumu anayoifanya katika Wizara hii ye ye pamoja na watendaji wake wote katika Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii ni pekee ambayo asilimia 98.9 ya bajeti yake yote ni kwa ajili ya utekelezaji wa mirdi ya maendeleo, hivyo basi, nashauri Serikali kutoa fedha kwa wakati ili kutekeleza kwa ufanisi mirdi yote ya maendeleo na ya kimkakati iliyo chini ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, mradi wa bwawa la umeme wa maji la Julius Nyerere Mkoa wa Pwani Rufiji unatekelezwa na Serikali kupitia *TANESCO* na unategemewa kuzalisha umeme wa maji wenye uwezo wa kuzalisha MW 2,115 na *Unit* bilioni 6.307 za umeme kwa mwaka. Pia kitu cha kufurahisha zaidi ni kwamba mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani kwa asilimia mia moja; na mkandarasi hadai hata shilingi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuwa, mradi huu utengenezewe mazingira mazuri ili kuwa kivutio cha utalii na kuongeza pato la Taifa, ukizingatia mradi huu umo ndani ya hifadhi ya mbuga ya Selous. Mradi huu wa bwawa la umeme wa maji la Julius Nyerere, una faida nyingi kwa Watanzania, kwani wasimamizi wa mradi huu ni Watanzania wenyewe. Pia mradi huu utaongeza ujuzi na uwezo kwa vijana wetu nchini na kuongeza fursa za ajira.

Mheshimiwa Spika, itasaidia kukuza pato la Serikali na Shirika la *TANESCO* kwa kuuza *unit* nyingi za umeme (*kwh*)

zipatazo shilingi bilioni 6.307 kwa mwaka. Pia itapelekea kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na mkaa kwa kupata umeme wa gharama nafuu na wa uhakika. Hivyo basi, ili miradi ikamilike kwa wakati, lazima Serikali iwasimamie vizuri Wakandarasi waliopewa miradi hiyo, wafanye kazi ipasavyo ili kupata ufanisi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nalishauri Bunge lako Tukufu kuwa kuna haja ya kuandaa ziara ya kwenda kuona mradi wa bwawa la umeme wa maji la Julius Nyerere Rufiji ili Wabunge wakaone jinsi Serikali inavyofanya kazi nzuri nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya Awamu ya Tano illyoongozwa na Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudzi zinazoendelea kufanyika za kusambaza umeme kwa nchi nzima. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati umeandaliwa vizuri. Pia nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri mambo yafuatayo. Naishauri Serikali kuendelea kusimamia na kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika na kuondoa changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara. Pia nashauri Serikali iedelee kusambaza umeme katika Vijiji na Vitongoji ambavyo bado havijafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iendelee kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Umeme wa Mwalimu Nyerere ili kupata umeme wa uhakika. Pia napendekeza Serikali kuendelea kufanya utafiti wa mafuta, gesi na vyanzo vingine vyta kuzalisha nishati ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia Serikali iendelee kuanzisha vituo vya usimamizi katika ngazi ya Taraifa ili kusaidia kutatua changamoto za kiufundi zitakazojitokeza. Vile vile iendelee kusambaza umeme. Kuna changamoto ya uhaba wa upatikanaji wa Transfoma hivyo kuchelewesha usambazaji wa umeme. Hivyo, Serikali isimamie uzalishaji wa Transfoma za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iendelee kusimamia usambazaji wa nishati ya gesi kwa matumizi ya majumbani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza na upande wa Mawaziri, sasa naomba niwatambue wageni wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Wauguzi Itigi, *St. Gaspar*, kutoka Mkoani Singida wakiongozwa na Ndg. Nyenze Ernest. Wanafunzi wa *St. Gaspar Nursing*, hongera sana na karibu sana Bungeni Dodoma. Mmetukuta tunaendelea na bajeti ya Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Waziri wenu wa Afya sijui kama mmemuona, yuko kwenye kona huku amenyamaza kimya. Haya anawapungia, ahsante sana. (*Makofii*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Edward Olelekaita kutoka Shule ya Sekondari ya *St. Maria Goreti*, Moshi, wakiongozwa na Ndg. Conina Lore na Bi. Nina Edward. *St. Maria Goreti*, shule maarufu sana hii. (*Makofii*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa Assa Makanika ambao ni wanafunzi nane wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) wanaotokea Jimboni Kigoma Kaskazini wakiongozwa na Ndg. Yamungu Kasogota. Karibu sana. (*Makofii*)

Sasa Waheshimiwa Mawaziri, tunaanza na Naibu Waziri wa Ardhi, dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na Wabunge wote ni mashahidi wameweza kuwapongeza. Nami nawapongeza kwa kazi kubwa waliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo na uchangiaji wa Wabunge, kuna maeneo mawili mazuri na ni maeneo ya kimkakati kwa Taifa letu lakini Wabunge wengi hawakuyazungumzia sana, wamezungumzia masuala ya REA pamoja na vinasaba. Nataka nizungumzie maeneo mawili ya bomba la mafuta kutoka Hoima mpaka Chongoleani pamoja na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, nianze na Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kama unavyotambua, maeneo mengi tunapokuwa na miradi ya kimkakati usipofanya maandalizi ya awali migogoro ya ardhi inakuwa ni mingi. Napenda nilithibitishie Bunge hili kwamba katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, pamoja na kazi zinazoendelea, Wizara pia imehakikisha inafanya kile inachotakiwa kufanya ili kuhakikisha kwamba tunalinda maeneo yale ya vyanzo vyaya maji, misitu na maeneo oevu.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika pale ni kuwaondoa wale waliokuwepo, kulikuwa na mahotel kama matatu; *Serena Luxury, Amara Camp* pamoja na *Retreat Safari Ltd.* Hoteli hizi zimelipwa zaidi ya Sh.3,754,000,000 ili kupisha maeneo yale. Kazi inayoendelea pale ni kupanga matumizi kwenye Mji wa Mloka pamoja na Mji wa Kisasi.

Katika Mji wa Mloka urasimishaji utafanyika kwenye kaya kama 1,000 na katika ule Mji wa Kisasi michoro 19 yenye viwanja 4,043 imeandaliwa. Kwa maana hiyo tayari tutakuwa tumeweka mazingira mazuri ili mradi unapoendelea basi kusiwepo na changamoto au migogoro ya ardhi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini upande wa bomba la mafuta, tayari eneo la Mkuza kutoka Hoima mpaka Chongoleani utambuzi wa maeneo yale ya Mkuza umeshafanyika na kuweza kujua kama kuna maeneo yanahitaji kulipwa fidia ni maeneo kiasi gani. Tayari maeneo 12 yametambuliwa katika eneo lile ambayo hasa yataanza na masuala mazima ya ujenzi wa kambi zile ambazo zitatumwiwa na wale wajenzi wa bomba la mafuta.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika maeneo ambayo wananchi watakuwepo pale kunapangwa miji ambayo itarahisisha kusogeza huduma za jamii katika maeneo yale kwa sababu bomba lile la mafuta litakapopita ni wazi shughuli za kijamii zitakuwepo. Kwa hiyo, tayari Sh.20,457,965,000 zitalipwa kama fidia katika yale maeneo ambapo *camp* hiso zitajengwa. Katika maeneo hayo watakaonufaika kwa fidia hiyo kwenye ujenzi wapo watu wa Misenyi, Kiteto, Kondoa, Iramba, Nzega, Igunga, Bukombe, Chato, Muheza, Handeni na Kilindi. Tayari utambuzi umefanyika na kinachofuata sasa ni namna ya kuweza kuona ni jinsi gani hatua hiso zitafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua hiyo kama Wizara ili kwanza kuleta usalama kwenye lile bomba la mafuta kwa sababu usipofanya hatua hiso za kupanga matumizi kwenye eneo lile ndiyo mwanzo sasa wa kugombania pale, watu watakuwa wana-*struggle* kutaka kuongezeka pale. Wizara inashirikiana na Wizara ya Nishati kuhakikisha mpango mzuri unawekwa pale ili watu waweze kukaa kwa amani kwa sababu tayari pia ni fursa kwao kwa shughuli za kimaendeleo. Maana ile miji ikipangwa tayari na uwekezaji katika maeneo yale utakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo nilitaka nilithibitishie tu Bunge kwa sababu wengi hawakuchangia maeneo hayo, nikaona basi kama Wizara tuseme kile ambacho Serikali imefanya kuhakikisha hii miradi mikubwa ya kimkakati inalindwa ili kuepusha migogoro na wananchi. Pia usalama wa maeneo yale tunaweka maandalizi kuweza kujua ni jinsi gani ambavyo tunaweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo pia kuna maeneo mengine 12 ya vituo vyatupozea, tayari wafidiwa 392 wametambuliwa. Jumla ya fidia yao ni shilingi 1,600,000,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali tayari imeshafanya maandalizi yake na tunaendelea kuhakikisha kwamba kila kilichopangwa kwenye eneo lile kinafanyika vizuri. Tumefanya hivyo ili bomba linapojengwa basi pasiwepo tena na sintofahamu katika suala zima la umiliki wa maeneo, lakini pia na kuyapanga yaonekane kwamba yamekaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuchangia hilo ili kutoa taarifa kwa Bunge lako nini ambacho kimefanyika katika hii miradi ya kimkakati. Vivyo hivyo hii inafanyika pia kwenye ile miradi ya *SGR*, nako Wizara ya Ardhi tupo kuhakikisha kwamba tunaepusha changamoto zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya ardhi au kwa watumia ardhi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ardhi Dkt. Angeline Mabula. Sasa nimuite Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka, dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kuunga mkono hoja ili lolote likitokea huko mbele basi niwe kwenye *safe side*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa muda huu mfupi ili na mimi niweze kusema kidogo tu wakati huo nikimuachia Mheshimiwa Waziri nafasi ya kueleza na kuweka *commitment* za Serikali kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa shukrani, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai, afya na nimshukuru Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kuniona mimi kijana na akaamua kunipa majukumu haya makubwa. Nimhakikishie tu kwamba kwa niaba ya vijana wenzangu ambao

tunaendelea kutumika katika nafasi hizi hatutamuangusha yeye wala Watanzania katika utekelezaji wa majukumu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini niwashukuru viongozi wa Kitaifa, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Kipekee kabisa nikushukuru wewe kwa jinsi unavyotuongoza na kutujenga sisi Wabunge na hasa sisi Wabunge vijana na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wapo humu kwa ushirikiano mkubwa ambao wanatupatia kama Wabunge, lakini mimi kwa nafasi yangu kama kiongozi kwenye nafasi ya Uwaziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Wizara yetu ya Nishati kwa kuendelea kuwa kiongozi, jemedari shupavu na aliyekakamaa kabisa na kutufikisha hapa ambapo wengi tunaogopa tunadhani hatutafika, lakini kwa maelekezo ya wakubwa wetu na yeye Wizara yetu imeendelea kufanya kazi ambazo Watanzania wanazitegemea. Pia niwashukuru watendaji wengine wote wa Wizara yetu ambao kwa kweli mengi tunayoyasema na kuyafanya hapa ni yale ambayo wao wametushauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipowashukuru wananchi wa Jimbo la Bukoba Mjini walioamua kukichagua Chama cha Mapinduzi kwa kunipa mimi kura za kutosha na kunituma kijana wao kuja kutumikia Taifa katika maeneo haya. Nimshukuru pia mke wangu kwa kuendelea kunivumilia na kunipa nafasi ya kufanya majukumu haya, lakini na familia kwa ujumla na maisha yanaendelea vema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia maeneo matatu tu, kwa haraka haraka, maeneo mawili ni ya ufanuzi mdogo na Mheshimiwa Waziri atakuja kumalizia. Eneo la kwanza Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia kuhusu kumatikia kwa umeme. Sababu za kumatikia kwa umeme zitaelezwa, lakini mimi niseme tumejipanga kupitia bajeti tunayoomba mbele yenu lakini

tumejipanga kufanya yafuatayo kwa uchache wake ili kuhakikisha basi umeme unakuwa haukatiki mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza tutarekebisha miundombinu kama ambavyo tumekuwa tukifanya, tutaendelea kupanua wigo wa kurekebisha miundombinu. Pia tutasogeza vituo vya kupoza umeme karibia na watumiaji ili kupunguza ule wigo wa umeme kupotea na vimetajwa kwenye bajeti yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tutafunga vifaa mbalimbali vya kitaalam vya kuhimili vitishio vya kiasili kama radi, mvua na vitu kama hivyo nitavitaja baadaye kitaalam. Pia tunaweka njia ile ya kupitisha umeme salama kwa kuendelea kufyekea yale maeneo ili yasipate madhara ya miti kuangukia nguzo na nyaya za umeme.

Mheshimiwa Spika, la mwisho siyo kwa umuhimu kuendelea kuwasimamia watumishi tunaofanya nao kazi na hasa wale wachache ambaao ni wazembe, wanaosababisha upotevu wa umeme na kuonekana kwamba umeme unakatika pengine bila sababu za msingi. Hivi juzi mmeona hatua ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu alizichukua pamoja na Mheshimiwa Waziri wetu katika kuhakikisha kwamba watumishi wanakuwa waadilifu na wanatumika vizuri kwa ajili ya kuwaleta maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nataka nizungumzie kidogo tu ni kuhusu miradi ya *REA*. Kwa nini miradi ya *REA* mingine imekuwa ikichelewa kukamilika? Sababu zipo nyingi lakini mimi nitaje kidogo tu, mojawapo ni ile kuongezeka kwa wigo wa kazi ambayo mkandarasi amekuwa amepewa mara ya kwanza. Alipewa vijiji sita lakini tumefika *sitemekuta vijiji* vinavyohitaji umeme zaidi ni kama tisa au kumi kwa vyovoyote vile ule muda wa awali tunajikuta tunatakiwa kuongeza ili kukamilisha yale ambayo yanatakiwa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ambalo ni la kuelezeza ni pale ambapo baadhi ya maeneo yanakuwa

hayafikiki labda ni kwenye mapori, hifadhi au hali ya hewa ya mvua basi hapapitiki kwa sababu ya miundombinu kuchukuliwa na maji tunajikuta tunachelewa katika maeneo hayo. La tatu ambalo pia linatokea ni mkandarasi kujikuta ana kazi nyingi na mwisho wa siku ikawa ni ngumu kuzimaliza kwa wakati aliopewa kwa sababu pengine ya usimamizi kuwa mgumu kidogo na hilo pia tutalizungumza kwamba tumechukua hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kama alivyosema mwenzangu mmoja lakini kama alivyowahi kusema kiongozi wetu mstaafu wa Mkoa wa Kagera Mama yetu Prof. Tibaijuka kwamba kadri unavyopanua zaidi ndivyo watu wanavyokuwa na hamu zaidi. Sasa Serikali ya Awamu ya Tano na ya Sita zimeendelea kupanua wigo wa kupata umeme. Katika kupanua wigo wa kupata umeme wananchi wamekuwa wakiluhitaji sana na matumizi yamekuwa ni makubwa na hiyo sasa inapeleke pengine umeme usionekane wa kutosha lakini jitihada za Serikali ni wazi kabisa mambo yataendelea kuwa mazuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo naomba nilizingumzie, mimi kwa nafasi yangu ya Unaibu Waziri na kwa jinsi tunavyofanya kazi katika michango mbalimbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge nimeona tunayo mambo kama 15 ambayo tunatakiwa kujivunia lakini pia yatakuwa ni chachu ya sisi kuendelea kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha Watanzania wanapata nishati ya umeme katika maeneo yaliyopo na umeme wa uhakika, sahihi, kila wakati na kwa gharama nafuu. Mambo hayo nikiyataja kwa haraka haraka tu, naamini dakika zilizobaki zitanitosha kuyajata hayo mambo 15; la kwanza ni bajeti ya Wizara ya Nishati kuwa na fedha ya maendeleo asilimia 98.9, hii fedha nydingine ni asilimia moja tu. Kwa hiyo, Wizara ya Nishati tumejipanga mkitupitishia kama ambavyo nitaomba mwishoni kufanya kazi kwa fedha tuliyopewa asilimia 98, tunaamini tutafika mbali kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini tumejipanga kuendelea kusimamia bora rasilimaliwatu na rasilimali fedha kama

ambavyo imekuwa ikifanyika. Pia tunahakikisha kwamba tunafikisha ile adhma ya kuwa na umeme unaotosha kwa Watanzania wote. Kwa sasa tunao uwezo wa kuzalisha *megawatt* karibu 1,602, lakini jana usiku ndio tumekuwa na matumizi ya juu *megawatt* 1,201, kwa hiyo bado tuna kama *megawatt* 400. Sasa miundombinu ya kuzifikisha hizo zote kwa Watanzania ndiyo ambayo tunaomba sasa mtusaidie ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoomba kwamba naomba...

**SPIKA:** Bado dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni kuendelea kuzalisha umeme katika miradi mbalimbali mkubwa sana ukiwa wa Mwalimu Nyerere, lakini pia tunayo Rusumo, tumesaini mkataba mwagine wa Malagarasi na tunaamini kwamba tutakuwa katika nafasi nzuri na miradi mingine. Pia tunahakikisha tutapeleka umeme katika vijiji vyote vilivybakia takribani kama 1,500 kabla ya mwezi Disemba 2022. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuboresha miundombinu yetu ya umeme kwa kufunga vifaa mbalimbali nilivyokuwa navisema, tunafunga *surge arrester, combi unit, auto recloser socket breaker, AVR* wameitaja hapa asubuhi na vitu vingine kama *lightning arrester*, tunahakikisha kwamba sasa umeme ukishakuwepo unaweza kuhimili hayo mambo ambayo ni ya kina *naturally* yanayoweza kuja kuzuia umeme wetu usiwe wa uhakika.

Pia tumejitahidi kutoa kazi nyngi kwa wakandarasi kidogo kidogo ili mkandarasi awe na wigo mdogo wa kufanya kazi na kumaliza, lakini tukiwa tunajenga uwezo wa watu wetu wa ndani kuweza kila mmoja kupata kazi na kumaliza kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tunahakikisha kwamba hakuna anayeuziwa nguzo, Mheshimiwa Waziri atakuja kulisitiza na kuliweka vizuri. Pia tunaunganisha wateja kwa gharama ya shilingi 27,000 peke yake, Mheshimiwa Waziri atakuja kulisema.

Mheshimiwa Spika, lakini tutahakikisha kwamba katika hiki kipindi cha kupeleka umeme kwenye awamu ya tatu, mzunguko wa pili, tunafungua madawati ya malipo katika maeneo ya wananchi wenyewe. Mtu asifunge safari kufuata sehemu ya kwenda kulipia kilometa 20, 30; madawati ya wenzetu wa *TANESCO* yatakuwa katika Kijiji au kitongoji ambapo mradi unafanyika. Ilishaelezwa Mheshimiwa Waziri naamini atakumbushia kwamba tutaruhusu hata kulipa kidogo kidogo kwa utaratibu ambao mwananchi atakuwa anaweza ili mwisho wa siku ile shilingi 27,000 iweze kufikia hatua ambayo sasa anaweza kila mmoja akalmudu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunafurahi kwamba *TPDC* imefanya kazi kubwa, asilimia 60 ya umeme tunaouzalisha unatokana na gesi yetu tunayozalisha ambayo inasimamiwa na *TPDC*. Hilo ni jambo la kujivunia sana.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunalo bomba la mafuta limezungumzwa hapa, tunazo fursa kedekede zitakazo kuja. Pia tunafikisha Gridi ya Taifa katika maeneo ambayo hayakuwa na *grid*, Mkoa wa Kagera ikiwemo, imeshafika Nyakanazi, Mkoa wa Kigoma tutakwenda mpaka Katavi na ni katika muda mfupi sana tutakuwa tumekamilisha yote hayo.

Mheshimiwa Spika, mawili ya mwisho, Wizara imehakikisha inaweka utaratibu mzuri kabisa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri kuhakikisha mkandarasi anampata Mbunge na Mbunge anampata mkandarasi. Tunaamini hilo ni sehemu kubwa ambayo itatuwezesha kujadiliana, kushauriana na kusimamiana vizuri kabisa ili muda utakapofika basi yale tunayo yaahidi yaweze kuwa yamefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho japo siyo kwa umuhimu ninashukuru kwamba wakati haya yote ninayoyasema yanatokea, mimi ni Naibu Waziri kwa hiyo nitakuwa na mimi ninajivunia na historia itakuwa imeandikwa kwangu mimi, kwa familia, lakini na kwa Watanzania wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzetu mtupitishie bajeti yetu, siyo ndogo ni kubwa, lakini itaweza kufanya yale ambayo mtatuagiza kuyafanya kwa moyo thabiti kama ambavyo mmetusifia na kutusemea vizuri tangu mnaanza na kwa kuendelea kutumwa bila kuchoka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Watanzania basi wanakipata kile ambacho wanakitarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**WABUNGE FULANI:** Kazi lendelee.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati. Sasa nimuite Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri mwenyewe, karibu hapa mbele, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, una nusu saa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, muda haupo upande wetu, Mheshimiwa Waziri tuendelee. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja. Nianze kukupongeza wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo umeongoza mjadala kwa upeo wa hali ya juu sana, ahsate sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumepata wachangiaji takribani 82 waliochangia kwa maandishi na wengine kwa

kuzungumza na wengine kwa namna mbalimbali. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwanza niwahahakishie kwamba michango yenu yote mliyoitoa kwetu, ushauri na mapendekozo na maoni yenu sisi tunachukulia kama maelekezo ya kwenda kufanya kazi. Tunawashukuru sana kwa michango yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze na kuchangia katika maeneo takribani 12, kwa ujumla jumla na machache sana nitagusia kwa kipekee. Nianze kuzungumzia Mpango wa Serikali wa kufikisha *megawatt* 5000. Tumeeleza kwenye kitabu chetu cha Mpango na Bajeti ya mwaka huu. Tunatekeleza miradi mikubwa mingi lakini mradi ambao kwa kweli Watanzania tungependa wote kujivunia ni Mradi wa Julius Nyerere, tunakwenda vizuri. Tumeeleza kwenye kitabu kwamba tumefikia asilimia 52 lakini ukienda kule *site* unaweza ukadhani tumefikia asilimia 80 na kitu, kazi inakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwahakkishie Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kuitia Bunge hili Tukufu mradi huo unakwenda kukamilika ndani ya wakati. Nilizungumza siyo siku nyingi zilizopita kwamba hivi karibuni Novemba mwaka huu tunaanza kujaza maji bwawa. Ni kweli kuja kufika tarehe 15 Novemba 2021, tunaanza kulijaza maji bwawa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi siku hiyo wachache wetu itakuwa ni siku ya sherehe. Kwenye mabwawa kama hayo huwa kuna hatua kubwa mbili; ya kwanza, siku ya kujaza bwawa na ya pili ya kuchaji umeme unapokwenda kutumika kwa wananchi.

Niwaondoe wasiwasi ndugu zangu wananchi na Waheshimiwa Wabunge tutalijaza mpaka kufikia tarehe 25 Aprili, 2022 bwawa letu litakuwa limeshajaa maji ya kuanza kuzalisha umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kusema kuja kufika tarehe 14 Juni 2022 tunaunganisha kwenye Gridi ya Taifa, tunawasha *transformera* wananchi wanaanza kupata umeme. Ni jambo ambalo nimeona niliweke wazi leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kurudia manufaa ya miradi kama hii, lakini jambo la msingi ambalo Waheshimiwa Wabunge mmechangia ni kuwepo umeme mchanganyiko. Ni kweli tumejipanga vizuri sana kusema ukweli kuanza kutekeleza miradi ya kila aina kuhakikisha tunapata *megawatt* 5,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi huu mkubwa wa Julius Nyerere, lakini tuna mipango ya miradi mingine ya gesi asilia ambapo mwakani kuanzia mwezi Septemba tunaanza kutekeleza mradi wa *megawatt* 300 kule Mtwara ambao utaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa baada ya miezi 18. Kwa kueleza michache tu ni kwamba tumejipanga vizuri na Waheshimiwa Wabunge mnatusaidia kupitisha bajeti leo, sisi kazi yetu kubwa ni kwenda kuhakikisha tunapata *megawatt* 5,000 ndani ya muda mfupi kufika mwaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi *LNG* ni muhimu sana na ni wa kimkakati. Ni lazima tukiri kwamba tumeporteza muda mrefu kidogo, lakini lengo ilikuwa ni kujipanga vizuri ili tusiliwe na wawekezaji. Mnafahamu vizuri sana ni kupitia Bunge hili mlisauri kwamba mikataba yote ya rasilimali ya gesi ichambuliwe na kupitiwa vizuri ili iwe na tija na manufaa kwa Watanzania. Naishukuru sana Serikali imetika wito, imechambua mikataba yote sasa kazi imekamilika na tunaanza majadiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe taarifa mbele yenu Waheshimiwa Wabunge tumeanza majadiliano toka mwezi uliopita na majadiliano yatachukua takribani miezi sita kutoka wakati huo na baada ya hapo utaratibu wa utekelezaji unaendelea. Kwa hiyo, niwape matumaini wananchi wote wa Kusini na Watanzania kwa ujumla mradi wa *LNG* unaanza

sasa kutekelezwa tena kwa *speed* kubwa. Kwa hiyo, niwaondoe wasiwasi ndugu zangu wananchi katika jambo hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la msingi hapa kuna suala la mgawanyo na matumizi ya gesi. Ni kweli tumegundua gesi nyingi sana takribani futi za ujazo trillioni 57.54 lakini kiwango tunachokitumia kwa sasa pamoja na kutumia kwa kiwango kikubwa katika kuzalisha umeme takribani asilimia 67 ya umeme tunaotumia, pamoja na kupeleka majumbani zaidi ya wananchi 1,000, magari 700 na viwanda 58 na kadhalika bado tumetumia chini ya asilimia moja kwa maana ya trillioni tulizonazo, ni 0.57 tu ya gesi tulioitumia, kwa hiyo, bado tuna gesi nyingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mpango wetu ni nini? Kwanza, ni kuhakikisha kwamba mradi huu wa *LNG* ambao utatumia takribani tani milioni 10 kila mwaka, kwa matumizi ya gesi kwenye kiwanda hiki gesi itatumika kwa kiasi kikubwa sana. Hadi kumaliza mpango wa utekelezaji wa mradi huu, tutakuwa tumetumia trillioni 3.9 kwenye rasilimali ya gesi. Hicho ni chanzo cha kwanza kuanza kuitumia gesi kwa kiwango kikubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunaendelea kuzalisha umeme wa gesi, megawati 300 Mtwara, megawati 330 Somangafungu na Kinyerezi I na Kinyerezi II tumetumia gesi, tunakwenda kuanza tena Kinyerezi III megawati 600 tutatumia rasilimali ya gesi. Matumizi yetu yatapanda, kwa sasa tunatumia takribani futi za ujazo milioni 200 kwa siku lakini matarajio yetu zitapanda maradufu katika miaka miwili ijayo. Kwa hiyo, niwaondoe wasiwasi wananchi kuhusu utumiaji wa rasilimali ya gesi.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la msingi tuna miradi mikubwa ya gesi, mradi wa kwanza tuna bomba la Uganda. Tunataka tutumie Mkuza huu wa bomba la kutoa mafuta Hoima kuja Tanga na sisi tutumie sehemu hiyo hiyo kupitisha gesi yetu kuwauzia majirani zetu Uganda. Vilevile, tunatarajia kujenga bomba lingine la kutoka Dar es Salaam kuelekea

Tanga hadi Mombasa litakalotumika kupeleka gesi pia maeneo ya Mombasa nchini Kenya. Kwa hiyo, bado rasilimali yetu itatumika sana katika maeneo yote. Nimeona hili nilifafanue kwamba rasilimali ya gesi haitakaa *idleitaendelea* kutumika kwa ajili ya manufaa ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ni muhimu sana Watanzania kulielewa, katika mafanikio ambayo Awamu ya Tano na Awamu ya Sita imepata ni huu mradi wa treni ya mwendokasi ya kisasa ya kutumia umeme. Haya ni mafanikio makubwa sana. Nilieleza kwenye bajeti yetu kwamba hadi sasa tumeshajenga kilometra 160 kwa asilimia 100 hata ukitaka ulete leo treni ya mwendokasi ya kisasa ya kutumia umeme kama tunataka iishie Morogoro, inaweza ikaanza kukimbia hata wiki ijayo na ikafika mpaka Morogoro kwa sababu tumeshajenga na tumekamilisha kwa asilimia 100. Haya ni mafanikio makubwa sana, naipongeza sana Serikali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *EACOP* wa kusafirisha mafuta kutoka Hoima. Huu ni mradi wenye manufaa makubwa sana. Tumeeleza hivi karibuni takribani mikoa nane, wilaya 24, kata 134, vijiji 257 na vitongoji 527 vinapitiwa na mradi huu. Maana yake nini? Maeneo yote nilyoyataja yanakwenda kukua kiuchumi. Kwa hiyo, hii ni fursa kubwa sana kwa wananchi wetu kuchangamkia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaambia wananchi wote wanaopitiwa na miradi hii, waanze kuijanda kuchukua fursa hizi ambazo kwa asilimia 80 ziko kwa Watanzania. Zaidi ya asilimia 80 ya mradi huu uko Tanzania maana yake ni kwamba sisi ndiyo wenye fursa ya kupata manufaa makubwa kutokana na mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilieleza vituo vingapi vitajengwa, kwa haraka haraka tutajenga takribani vituo nane kwa ajili ya kusukuma mafuta lakini vituo 6 kati ya 8 vyote viko Tanzania na vitakuwa na makambi ya wafanyakazi. Tutakuwa na maeneo ya kufunga *valve* kwenye vituo 79 lakini maeneo 53 yako Tanzania, hizo ni fursa. Tutakuwa na maeneo ambako

tutachemsha mafuta hayo kwa sababu ni ya kuchemsha, kati ya vituo 29 vituo 22 viko Tanzania, hizo ni fursa kwetu. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Watanzania kutumia fursa hizi ili kuleta manufaa kwao. Mradi umeshaanza kutekelezwa, ni matumaini yetu ndani ya miaka mitatu mradi utakamilika na manufaa tutayaona zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi katika Mkoa wetu wa Tanga hasa kule Chongeleani, bandari ya Tanga inakwenda kupanuka sana kwa sababu hapo ndiyo mafuta yatakapokwenda kusimama na kutakuwa na uwekezaji mkubwa zaidi ambapo uwekezaji wa nje tunatarajia kwa Serikali yetu kunufaika kwa asilimia takribani 55. Haya ni manufaa makubwa ambayo Watanzania ni vyema kujivunia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mradi wa *REA*. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda niwahakikishie Watanzania na Waheshimiwa Wabunge mradi huu wa *REA III round II*, tunakwenda kumaliza vijiji vyote na huu siyo utani, hii ni dhamira ya Serikali. Tumedhamiria ni lazima tumalize. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge katika hili kwani wametupa ushirikiano wa kutosha katika kila hatua. Niwaombe, kama kuna Kijiji katika eneo lako kimesahaulika, ama kimerukwa kwa namna yoyote ile tukiwa hapa Bungeni tuletee kabla hatujaondoka ili twende tukakijumlishe na kifanyiwe kazi. Suala la umeme kwa sasa ndugu zangu sio la hiari ni jambo la lazima. Ni lazima tuelewane. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ameeleza Naibu Waziri, tumejipanga vizuri leo tuko wa kwanza Barani Afrika kupeleka umeme vijiji lakini tunataka tusiishie hapo tuwe wa kwanza kupeleka umeme bora na wa uhakika, ndio lengo letu la msingi. Vijiji vilivyobaki tumepeleka wakandarasi, tumebakiza wakandarasi watano ni matumaini yetu kwamba wiki ijayo nao wanaweza kupatikana ili mikoa na maeneo yote wakandarasi wawe wameshafika *site*. Nitumie nafasi hii kutoa

wito kwa wakandarasi, mkandarasi ye yote atakayelegalega hata kabla hajachelewesha mradi tukimbaini njiani, tunamuacha, tunamtelekeza, tunachukua mkandarasi mwingine, hiyo hatua tunayokwenda kuchukua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimeeleza Watanzania Mradi wa Umeme Vijiji haubagui nyumba na hili nisitisite kwa watani wangu wa Dodoma. Zile nyumba zetu za tembe zote ni umeme, hatuchagui nyumba. Najua mmeshatoka huko lakini tunataka Watanzania wote waone hii ni fursa. Nazungumza huu si utani, leo nenda Kongwa kwa Mheshimiwa Spika, Bahi, Singida angalieni barabarani, nyumba za aina hiyo tunataka zikue zifanane na magorofa, wananchi wa -enjoymaisha yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mradi huu tumejipanga vizuri. Katika maeneo ambayo vitongoji vimebaki, tuna mradi wa vitongoji almaarufu *densification*. Huu mradi ni muhimu sana, tumetenga shilingi bilioni 366 kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote, hiyo ndiyo dhamira ya Serikali. Pia tuna maeneo ambayo kimsingi sio vijiji yanaitwa mitaa lakini ukiyatazama kwa hali halisi na wala si mitaa kwenye macho ya Watanzania. Hasa maeneo katika Majiji, Manispaa, Halmashauri za Miji yako mengi, tumeanza kushughulika nao. Kwa sasa tumbaini maeneo 637, maeneo ya Dar es Salaam, yakiwemo ya huko Chanika, Bombambilii, Dondwe, Msongole, Zingiziwa hayo yote tunawapelekea umeme. Hata kule kwa Naibu Spika kule Tonya, Ituhi, Nzoho, tunapeleka umeme kwa bei hiihii. Hata kwako Mheshimiwa Spika ulisema pale Mbande Kati na Mbande Kisimani tunapeleka kwa bei hii hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Majiji ya Mwanza, iwe Nyamanoro, Nyamadoke, Kishiri, Kabaha, Kalemela yote tunapeleka umeme kwa bei hiihii. Arusha, iwe Murieti, Olasiti, Moshono, Terati, bei ni hizi hizi. Dodoma, iwe Ntyuka, Nala, Vikonde tunapeleka kwa bei hiihii. Tumetenga shilingi bilioni 160 kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo haya ambayo yanatuchanganya ni vijiji ama ni mitaa. Sisi kwenye macho ya Serikali tumedhamiria yote

yawe shilingi 27,000. Kwa hiyo, Watanzania wote watapata umeme bila kuchelewa. Kazi hii si ndogo lakini Serikali tumejjipanga, Wabunge mmejjipanga najua leo mnatupitishia bajeti, mkishamaliza kupitisha bajeti sisi mtatuona vijiji hatutakaa ofisini, lengo tupeleke umeme kwenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikandamizie mbele ya Bunge lako Tukufu, umeme iwe kijijini anapeleka *REA* au mjini anapeleka *TANESCO* bei ni shilingi 27,000. Naomba nirudie, bei ya kupeleka umeme ukiondoa *City* pale llala Dar es Salaam ambapo hata kwa sasa hawahitaji wana umeme, maeneo yote nchini ni shilingi 27,000. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan, Oyeee. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Oyeee. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba niwaelekeze *TANESCO*, atakayesuasua kutekeleza agizo hili, hajitaki na atakuwa hana kazi. Hayo ndiyo maelekezo ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuuziwa nguzo, naomba nirudie, Serikali imegharamia nguzo kwa asilimia 100 na nguzo zipo. Mahitaji yetu ya nguzo kwa mwaka ni nguzo milioni 2.8, nguzo tulizonazo ni milioni 4.9, kwa hiyo, nguzo zipo. Naomba nisisitize kwa mara nyingine wakandarasi, Mameneja wa *TANESCO*, wala msijiingize kwenye mtego wa kusema mwananchi anunue nguzo tutakushughulikia mapema usiku na mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jipangeni, haiwezekani Watanzania wote waishi ndani ya mita 30 kutoka kwenye nguzo. Niwaombe sana *TANESCO* na wakandarasi mijipange katika hilo, lazima muwe wabunifu, mfanye kazi kwa kasi na uweledi wenye uaminifu. Sihitaji kurudia katika hilo, nadhani watendaji wetu wameelewa na hili linatekelezeka wala hatuna mashaka nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna suala la kucheleweshwa wananchi kuunganishiwa umeme. Ameeleza Mheshimiwa Naibu Waziri yako maeneo kuna sababu lakini pamoja na sababu nzuri tulizozitoa, tumeanza kuchukua hatua na tunawapima Mameneja wetu kwa vigezo viwili, ili apande cheo ni vigezo viwili vikubwa. La kwanza, kuunganishia umeme wateja kwa kasi, hilo ndilo lengo tunalowapimia. La pili, anavyohudumia wateja, hivyo ni vigezo vikubwa sana tunavyovizingatia. *TANESCO* inafanya biashara, kazi yake kubwa ni kuwajali wateja wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeshaeleza na nimetoa miezi miwili kwa *TANESCO* Mameneja wote ambao wanadaiwa na wananchi wameshalipa pesa yao, hajawaunganishia umeme wakamilishe kufanya zoezi hilo ndani ya miezi miwili vinginevyo tutachukua hatua kwa Mameneja wanaohusika. Tumeanza kuchukua hatua, slo lengo letu kuwaonea, lakini tunataka wafanye kazi kwa umakini, kwa kasi na kwa kweli kwa ubunifu mkubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu kukatikakatika kwa umeme. Tumeeleza kwa kiasi kidogo, naomba nirudie tu kidogo. Yako kweli mazingira, nchi yetu ndugu zangu ni kubwa, unauzungumzia waya unatoka Mtwara mpaka Kagera, unatoka Mtwara katika Mtaa wa Mkunjanguo unakwenda mpaka Kyaka, mazingira haya ni marefu, yako maeneo kwa kweli hali halisi inatokea waya ukakatika, hilo nalo lipo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, lazima tukubali bado tunatumia nguzo za miti kwa kiasi kikubwa, baada ya miaka miwili zinaoza, si kwamba hazina ubora ndiyo *nature* ya miti yetu haiwezi kukaa miaka mingi, hiyo changamoto nyngine. Sababu nyngine ni matumizi yetu sisi wananchi, mtu anaweza akagonga nguzo, akachoma moto na kadhalika. Hata hivyo, tumeweka bajeti tumeeleza hapa, mwaka huu tumetenga bajeti ya ndani ya *TANESCO* shilingi bilioni 85.8 kurekebisha dosari hizo ndogo ili umeme uwe imara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi kabisa tumeleza, baadhi ya maeneo kwa kweli njia ni ndefu, umeme unafika ukiwa kidogo. Tumetenga fedha nyingi sana mwaka huu zaidi ya shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kujenga vituo vya kufua umeme katika maeneo hayo ili kuimarisha upatikanaji wa umeme. Tumefanya hivi Handeni, Kilindi, Simiyu, Ipole, Nguruka, Urambo na maeneo mengine tunaenda kufanya hivyo. Leo tumeanza kutekeleza mpango wa kujenga *substation* Mkuranga ili Mbagala ijitegemee na Mkuranga ipate umeme wake, lengo ni kuboresha njia hizo za umeme. Hatukusudii kuendelea kuwa na umeme unaokatika, tumejipanga vizuri na Wabunge mnatuunga mkono, ni matumaini yetu hili jambo tumelipa muda mfupi mbele ya safari tutakwenda vizuri. Tukikamilisha Mradi wa Julius Nyerere nataka niwaambie Watanzania hii nchi inakwenda kuwa Ulaya ya Afrika, hizi ni dosari za wakati huu tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala la kukatika kwa umeme Serikali inakwenda kupitia upya bei za ankara za umeme kwa Tanzania. Tunakwenda kuangalia bei kulingana na uzalishaji. Tulisema uzalishaji wa mradi huu unachukua mpaka *unit* 1 Sh.36 ukilinganisha na vyanzo vingine. Sitaki kutaja kila chanzo, lakini ndio chanzo cha gharama ya chini kabisa unapozalisha umeme, kwa hiyo, Serikali tutafikiria pia kufanya mapitio ya bei za ankara kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bei za visiwani, wazalishaji wadogo maeneo mengine wanaitwa Wananzengo wanawauzia wananchi umeme kwa bei kubwa Sh.3,500 wakati *unit* 1 kwa bei elekezi ya Serikali ni Sh.100 kwa Watanzania wa kawaida. Tilitoa maelekezo mwaka juzi, tumetoa maelekezo mara nne na leo narudia mara ya tano. Niwaombe na kuwaagiza wazalishaji wote wadogo wadogo, bei elekezi ya Serikali ya kuuza umeme kwa Watanzania ni Sh.100 kwa *unit* na si vinginevyo. Kwa hiyo, wazalishaji walioko visiwani, Mheshimiwa ameeleza hata kule Ukerewe kuna wazalishaji wa namna hiyo, wako Buchosa kule Maisome wanafanya hivyo, wako Nyantakara Biharamulo, wako Mafia, wako Njombe na Makete na maeneo mengine, tulishawapa muda warekebishe dosari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze viongozi wenzetu wanaosimamia usalama wa wananchi kule, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa watusaidie, tulishatoa maelekezo na hata kwenye kanuni na mikataba yao hiyo bei haimo wanafanya hivyo kurejesha faida. Hatuwezi tukakubali arejeshe faida kwa maumivu ya Watanzania, bei inaeleweka.

Kwa hiyo, ni marufuku wazalishaji wengine wowote wale, kuzalisha umeme sio shida, wahudumieni wananchi wetu lakini bei ya umeme lazima iwe linganifu shilingi 100 kwa *unit* na si vinginevyo. Hili narudia leo tusilisikie tena tutachukua hatua kali dhidi ya wazalishaji hao wadogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na gridi Kigoma, Katavi na maeneo mengine. Kwanza niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote wa Kigoma na Katavi mnajitahidi sana kutupa ushirikiano. Nataka niwahakikishie kwa Kigoma peke yake, kuna njia nne zote zinashambulia kupeleka gridi ya umeme Kigoma. Njia ya kwanza ni ile ya dharura ya kutoka Urambo, tunapitisha *substation* kutoka Urambo, Nguruka mpaka Kidahwe na mwakani tunakamilisha, hiyo ya kwanza. Ya pili ni kutoka Kigoma hadi Nyakanazi kilometra 283 kutoka Nyakanazi tunapeleka KV220 Kigoma mpaka Kidahwe, hiyo ni ya pili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunaanza kutekeleza Malagarasi, niipongeze sana Serikali wiki iliyopita tumepata dola milioni 140 kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi wa Malagarasi. Napo tunajenga mradi kutoka Malagarasi kilometra 53 mpaka tena Kidahwe, hiyo ni njia ya tatu. Ya nne ni kutoka Sumbawanga hadi Mpanda mpaka tena Kigoma jamani, wananchi wa Kigoma mtafurahi tu muda sio mrefu. Tunashukuru sana kwa ushirikiano wenu lakini Serikali imejipanga vizuri sana katika hilo. Tuvumilieni kidogo lakini Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan amejipanga vizuri, Makamu wa Rais yuko vizuri, Waziri Mkuu ndio usiseme anatuongoza vizuri tutawafikishia umeme wa gridi Kigoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vivyo hivyo hata Mpanda tumeanza kutekeleza mradi mzuri wa kutoka Tabora kuititia Ipole, Inyonga mpaka Mpanda. Juzi akaeleza Mheshimiwa Mbunge mwininge tupitishe mpaka Nsimbo, tutapita Nsimbo kwa sababu gridi inapita maeneo yale yale. Kwa hiyo, tuna matumaini kwamba umeme wa gridi utafika maeneo yote. Kwa wakati huu tuna vifaa ambavyo vitakwenda kurekebisha tatizo kwa muda mfupi lakini suluhisho la muda mrefu kwa wananchi wa maeneo hayo linakuja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata wananchi wa Simiyu, Simiyu ni Mkoa unaojenga viwanda, tumeanza kujenga gridi ya Taifa kutoka Ibadakule Shinyanga umbali wa kilometra 109 kwa kutumia fedha ya ndani, eneo la Imalilo tumeanza kutengeneza muda si mrefu. Kwa hiyo, ni matumaini yetu tutakamilisha vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, deni la *ZECO* na *TANESCO*. Kwanza niishukuru Serikali mwaka juzi kulikuwa na deni la VAT la shilingi bilioni 22. Kwa umakini wa Serikali yetu deni likaondolewa, tunawapongeza sana viongozi wetu. Limebakilishi deni la *KVA charge*, nitoe tu mrejesho kwamba linakwenda vizuri, *technical team* ya masuala ya Muungano, kwa taarifa nilizopewa leo imekaa mwezi uliopita na tarehe 8 na tarehe 9 mwezi huu itakaa kwa ajili ya kufanya kazi jambo hili kwa sababu liko kwenye Serikali ya Muungano na litakamilishwa muda si mrefu. Kwa hiyo, wenzetu wa Zanzibar mtuvumilie kwa sababu najua kamati ile ya masuala ya Muungano inalifanya kazi kwa kina sana *Inshaalah* najua matokeo yake yatakuwa mazuri zaidi kama ambavyo imekuwa siku za nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nzungumze kidogo kuhusiana na vituo vya mafuta vijijini. Tunaposema kupeleka nishati vijijini naomba isitafsirike kwamba ni umeme peke yake. Nishati vijijiji ni pamoja na mafuta vijijini pamoja na *gas* ya mitungi vijijini. Tumeanza, katika mwaka uliopita tumepeleka takriban vituo vidogo 221 vijijini vya mkono mmoja walau wananchi wanaomiliki bodaboda na taksi waweze kupata mafuta kule vijijini. Hivi viroba vya mafuta kubebwa kwenye bodaboda

tunataka yafike mwisho ili wananchi nao wapate huduma hii kulekule vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumejipanga vizuri na wenzetu *EWURA* tuliwaambia wafanye mapitio upya pamoja na taasisi nyingine kuondoa mlolongo na ukiritimba na gharama kubwa ya uanzishwaji wa vituo hivi; ambavyo vinafanya Watanzania washindwe kuviendesha. Kwa hiyo, matumaini yetu tutakwenda vizuri katika eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, imeelezwa vizuri kuhusiana na deni la Mradi wa Bomba la Gesi Madimba. Serikali yetu inalipa na tunakwenda vizuri na mradi hauna mashaka. Deni lilikuwa ni Dola za Marekekani bilioni 1.2 tumeshalipa zaidi ya milioni 221 na tunakwenda kulilipa vizuri. Kwa *trend* ya kulilipa ni nzuri na wenzetu wa Hazina wanatupa ushirikiano mzuri tunakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ameelleza Mheshimiwa Mwijage ni mtaalam mzuri sana. Mheshimiwa Mwigaje nakupongeza sana kwani umenisaidia sana. Kwa kweli bei hupangwa na soko la dunia. Masuala haya ya mafuta na gesi kuna wakati bei kwenye soko la dunia kwa sababu mbalimbali inaweza ikashuka. Mkiona hapa tumeshusha bei maana yake na kule imeshuka. Sisi huwa tunatangaza bei inayopangwa pia kwenye soko la dunia. Bahati nzuri sana bei inapopanda kwenye soko la dunia na huku ikapanda huwa tunapiga kelele lakini ikishuka kule na huku ikishuka huwa sisikii watu wakipiga kelele. Hiyo ndiyo *fluctuation* ya soko la dunia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hili lazima tuelezane ukweli. Kwa hiyo, ndugu zangu kazi yetu ni kufuattilia, je, vyanzo vya bei hivi ni halisi? Niwaombe sana wenzetu Wakala wa Mafuta (*EWURA*) kuanza kufuattilia kisasa bei za soko la dunia katika mafuta ili Watanzania waweze kuelewa vizuri zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda ambao umenipa, naomba labda nirudie jambo moja tu katika mradi

wa *EACOP*. Watanzania wanataka kujua kuhusu semina kuelezea manufaa ya mradi huu na ule wa *LNG*. Tumetaka kuwa na semina kwenye maeneo ambako miradi inapita kwa ajili ya kuwajengea uwezo na ufahamu wananchi namna ya kushiriki kwenye miradi hii ya kimkakati. Semina hizi tumezianza katika maeneo ya Nzega lakini Waheshimiwa Wabunge mnaotoka katika maeneo ya miradi ya Kagera, Geita, Shinyanga mpaka kufika Tanga tunategemea kuanzia wiki ijayo tunaanza semina. Tunapenda sana tuwashirikishe Wabunge wawasaide wananchi ili miradi hii iwe na manufaa na wajiandae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na kuwashirikisha katika kazi za bomba, tumeandaa kanzidata (*database*) kwa ajili ya makampuni yote. Makampuni yote ya ndani yameorodheshwa kupitia Kanzidata ya *EWURA*. Kwa hiyo, niombe kama kuna kampuni ya kizalendo, ya kitanzania na ina uwezo, sifa na nia ya kufanya kazi katika miradi hii ipoleke *company profile* yake *EWURA* ili kusudi wakati wa mchuko tuzingatie makampuni ya kitanzania siyo makampuni yaliyosajiliwa Tanzania. Hii ndiyo itakuwa jambo lenye manufaa kwetu kwa ajili ya kunufaika na miradi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *LNG* tumeshalipa fidia ya shilingi bilioni 5.71. Tunachofanya sasa ni kufanya mapitio ya eneo ambako wananchi watanufaika. Yako maeneo ya Likong'o, Mtomkavu na Masasi ya Leo. Maeneo hayo yote tunataka wananchi washiriki ipasavyo katika mradi huu wa kimkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo kazi kubwa ni kuomba fedha na naomba mnitume tukakimbie tuwapelekee umeme kwenye vijiji, nisitumie muda mrefu sana, niwaomba Waheshimiwa Wabunge mtupitishie fedha zetu, sisi tupo tayari kwenda kufanya kazi. Ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia 100. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.  
*(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na uafanuzi mkubwa sana ambao umeutoa. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management.....Sh.3,066,285,000*

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri, tunaanza na Mheshimiwa Samweli Hhayuma lakini kabla hajasema kitu, kuna neno moja Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha ulisema mtaitana na Wabunge wa maeneo ambayo bomba hili linapita na kupeana semina. Ni jambo zuri sana lakini tunakushauri kwamba kwa miradi hii ya kielelezo na ya kimkakati ni vizuri Wabunge wote hawa wakapata semina.  
*(Makofi)*

Huu siyo mradi wa wale ambao unapita tu kwenye maeneo yenu, maana hizo kampuni zitakazoomba labda kama ni za maeneo hayo hayo vinginevyo ni lazima Wabunge hawa wote waelewe. Huu ni mradi mkubwa na ni jambo zuri sana kwa Serikali yetu ni vizuri uwelewa ukawa ni wa pamoja. Tafuteni namna namna tu, ninyi ni watu wakubwa, wizara kubwa hii.

Sasa nimuite Mheshimiwa Samweli Hhayuma. (*Makof*)

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mimi naomba ufanuzi kidogo kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri hasa kwenye hizi bei za umeme. Kwa mujibu wa maelekezo Na.10 ya 2016 watu wa vijijini wanaoanza kufungiwa umeme wanaingia kwenye daraja D1 ambapo umeme kwa *unit* 1 ni shilingi 100. Pale tu ambapo matumizi yake kwa mwezi yamezidi *units* 75 ndio anahamishiwa *unit*T1 ambapo bei hapo inapanda na ni kwa miezi mitatu mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku za karibuni watu wamekuwa wakihamishwa kwenda kwenye T1 bila kupewa taarifa na ni maeneo mengi nchini. Waziri nimeshaongea naye lakini naomba atoe kauli kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata majibu ya kutosheleza nitakamata shilingi. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kuhamisha watu, Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tatizo hili limejitokeza katika baadhi ya maeneo. Mimi nilitembelea Babati nikagundua tatizo kama hili lakini tumetoa maelekezo ya wiki mbili mfululizo toka wiki iliyopita wataalam wetu wapitie kila eneo ambako kuna tatizo la namna hiyo kurekebisha dosari hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nifafanue kidogo kuhusiana na jambo hili, mteja wa kawaida ambaye matumizi yake hayazidi *unit* 75 kwa mwezi, huyo kimsingi analipa Sh.100 kwa *unit*. Hata hivyo, wapo wateja wanaanza na matumizi madogo baada ya muda ananogewa anajenga nyumba ya pili, anaongeza vifaa, *automatically* mfumo unakuhamisha unaingia katika kundi la watumiaji wa daraja linalofuata ambapo bei yake kwa *unit* ni Sh.292. Nitoa angalizo pia na sisi tuijangalie katika matumizi yetu lakini hili la mfumo tumetoa maelekezo na tunakwenda kulifanyia kazi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eric Shigongo, nafikiri Waziri amejibu hoja yako lakini endelea kama bado unataka ufanuzi zaidi.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema kwa kweli Waziri amenijibu vizuri sana na nilipigiwa simu sasa hivi kwamba *DC* ametoa maelekezo kwamba wale jamaa wanaouza umeme kwa bei kubwa washughulikiwe mara moja. Kwa hiyo, naomba swali langu, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa uungwana. Mheshimiwa Fredy Mwakibete.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate ufanuzi na sina sababu ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa kuwa najua anakwenda kutekeleza aliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la Petroli Nchini, kwa mujibu wa Sheria ya *Oil and Gas Revenue Management Act*, 2015 walipewa *mandate* ya kufanya tafiti za *gas and oil* lakini pia kusambaza gesi majumbani. Hata hivyo, shirika halifanyi kazi vizuri wameweza kusambaza *cubic meter* 700,083 tu kwa sababu ya sheria hii ambayo ni asilimia 3 ya makusanyo yote yamekuwa *ring-fenced* na hawaruhusiwa kuzichukua wala kufanya maendeleo yoyote. Sasa Mheshimiwa Waziri atuambie kama haoni kuna kila sababu kwa Wizara yake pamoja na Wizara ya Fedha kuja na sheria mpya ili kuruhusu *TPDC* waweze kuzitumia fedha hizi ambazo ziko *ring-fenced* asilimia 3 za *GDP*ili waweze kusambaza gesi majumbani? Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEITI:** Ufanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Waziri, tafadhalii.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali hili kwa mara ya pili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka 2015 ilipitishwa Sheria ya *Oil and Gas Revenue Management Fund* ambayo kimsingi ilielekeza fedha zinazotokana na mapato ya gesi ziende kwenye Mfuko Maalum na zikihitajika mpaka ifike /eve/fulani ya mahitaji. Ndani ya Serikali tumeanza kukaa tuone namna gani ya kuzitumia fedha hizi kwa ajili ya utafutaji na utafiti wa gesi na mafuta.

Kwa hiyo, si muda mrefu tutapata namna nzuri ya kulitekeleza suala hili kwa sababu tulifanya hivyo tukijua wakati isingekuwa kikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda niipongeze *TPDC* imefanya kazi kubwa katika baadhi ya maeneo. Inafanya kazi kwa fedha ambazo inazipata ambazo kiasi kikubwa sana ni kupitia maombi na shughuli ndogo ndogo za kutangaza *tender* na nyingine na inafanya vizuri. Hivi karibuni mmesikia taarifa inafanya vizuri katika utafutaji wa mafuta katika eneo la Eyasi-Wembere. Yapo matumaini makubwa ya kupata mafuta kutoptana na fedha hizi *TPDC* inazotengeneza yenyewe. Kwa hiyo, inafanya kazi vizuri na hili suala la fedha kukaa Hazina kama nilivyosema tutalimaliza na fedha zitaanza kutumika kwa *TPDC* kuendeleza rasilimali ya gesi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Hiyo ni habari njema, Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami sina dhamira ya kushika shilingi lakini nataka tu *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Serikali ina dhamira ya kupeleka umeme vijijini na mijini na ndio maana tuna Dira ya Maendeleo ya Taifa kama nilivyosema mapema leo wakati nachangia. Malengo ya Mpango wa Pili ilikuwa kufikisha *megawatts* 4,915 kwa kipindi cha miaka mitano kwa maana kutoka *megawatts* 1,501 walitarajia kuongeza *megawatts* 3,414. Hata hivyo, kwa miaka yote mitano waliweza kuzalisha *megawatts* 104 tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Malengo ya Mpango wa Tatu tunatarajia kufikisha *megawatts* 5,000 kwa maana ya kutoka *megawatts* 1,600 liliyopo sasa hivi mpaka *megawatts* 5,000. Kushindwa kutekelezwa kwa malengo haya ya mpango ni kwa sababu Serikali haipeleki fedha tunazopitisha hapa na ambazo zimeombwa na Mawaziri. Waziri amekuja na mipango madhubuti kwa ajili ya kutatua changamoto ya kukatika kwa umeme na kupeleka umeme kwenye maeneo yote lakini tutapitisha fedha, kwa mfano, sasa hivi tunawapitishia trilioni 2.3 lakini kama Serikali haiweki *commitment* ya kuzipeleka itakuwa kama mwaka wa fedha uliokwisha tuliwapitishia trilioni 2.17 mpaka Mei, miezi 11 wamepokea trilioni 1.35 tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka *commitment* ya Serikali tunapopitisha hizi fedha wahakikishe wanazipeleka zote au walau hata kwa asilimia 90. Vinginevyo malengo ya Mpango wa Tatu hautafikia na Watanzania hawatapata umeme kama inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu *commitment* ya Serikali kupeleka fedha ili hawa Mawaziri wenye morali waweze kufanya kazi na kupeleka umeme maeneo yote. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Umeeleka Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi hii mikubwa na ya kimkakati na ambayo inalenga kuchochea uchumi na inabadilisha maisha ya ya Watanzania, Serikali haina kigugumizi cha kutoa fedha. Jambo pekee ambalo limefanyika ni kwa sababu huu mradi ulikuwa una kazi ngumu sana za mwanzo zile za kuweka mambo sawa. Utaratibu wa Serikali kulipa ni kwa *certificate* na mpaka hivi tunavyoongea hakuna *certificate* ambazo hazijalipwa kwa sababu hakuna fedha. Fedha zipo, isipokuwa lazima kazi ifanyike kwa uangalifu mzuri na Wizara inasimamia vizuri sana na tunawasiliana na ndio maana yale

ambayo yanaonekana kukwama Mheshimiwa Waziri ametoa uhakika kwamba tutakaa na kuyamaliza.

Kwa hiyo, hata utoaji wa fedha kwenye maeneo haya ambayo ni ya msingi tutajitahidi kama Wizara na kama Serikali kuhakikisha hatukwamishi shughuli hizo ambazo zinakwenda kubadilisha kabisa uchumi wa nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyikiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na kama alivyosema hana dhamira ya kushika shilingi, ashike *commitment* hiyo ya Serikali na tumejipanga na Mama mwenyewe amesema kazi iendelee na kazi itaendelea. Sisi kama Wizara ya Fedha tutahakikisha kwamba fedha zinatoka kwa wakati. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hata Mwenyekiti anakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu hata ninyi Wabunge mnaotoka kwenye halmshauri mbalimbali kama mnafuatilia mtaona kwa kweli ahadi za Serikali kwa safari hii fedha imekuwa inakuja kwenye halmashauri huko katika namna ambayo haijapata kutokea. Kwa kweli tunawashukuru sana muendelee na utaratibu huo. Kama alivyoulizwa Mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi wasiwasi wetu tu msije tena mkarudi kule, hilo tu basi lakini utoaji wa fedha kwa kweli safari hii mnakwenda vizuri, hongereni sana. (*Makof!*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Francis Ndulane. (*Makof!*)

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi pia sina dhamira ya kushika shilingi kwa Wizara yetu hii ya Nishati kwa sababu kazi inayofanyika ni nzuri na inatia matumaini kwa wananchi wetu. Isipokuwa nilikuwa nina shida kwenye eneo moja la utekelezaji wa REA //na REA III. REA //kuna Kijiji changu kimoja cha Hanga, Kata ya Kibata, mkandarasi bado hajakamilisha kazi japokuwa muda wa utekelezaji wa mradi umeshapita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndulane swali hilo siyo la sera. La kijji chako tena, hilo ungechangia tu kwa maandishi au vinginevyo lakini halihusiani na sera.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kwa ujumla wake napenda uharaka ufanyike kwa sababu hata kwenye *REA* / / nimeongea hata na majirani zangu hapa inaonekana katika maeneo yao wakandarasi wameshafika lakini kwangu bado hawajafika kumalizia vijiji 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante labda kwa kwa sekunde tu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako lile la malipo kama naweza nikaongezea kidogo tu. Serikali kama ulivyo sema kwa sasa inalipa vizuri sana. Katika mradi wetu wa Julius Nyerere, sasa hivi tumeshalipa triliioni 2.46 na katika mkataba tuliokuwa tumeingia na wakandarasi kwa mashaka hayo hayo walikuwa wamesema mkiweza kulipa kwa mfufulizo mara tatu bila kuchelewa tunaongezea asilimia moja ya *CSR*. Tume-*qualify* na wametuongezea asilimia moja ya *CSR*. Nimeona hilo niliongezee ili Wabunge wafahamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupeleka wakandarasi maeneo yote, hili tutalisimamia na Mheshimiwa Mbunge ambako mkandarasi hajafika tutawasiliana tumfualitie ili aweze kufika. Pia katika maeneo yote ya Waheshimiwa Wabunge ambako wakandarasi hawajafika tutawasukuma waweze kufika ndani ya muda ili waanze kazi mara moja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niseme tu kabisa kaka

yangu Mheshimiwa Kalemani mbali na utendaji wako nisiporidhika na majibu nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nilzungumzia ni namna gani kama Serikali tunakuwa wazito kusimamia mikataba hata pale inapotu-*favour*. Nikazungumzia kwa upande wa Songas na Pangea wakati ikiwa imefanya ukarabati wa miundombinu kwenye mgodi wa Buzwagi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Songas Mwenyekiti wewe ni shahidi, Kamati yako 2018 ilisema kabisa huu mradi hauna tija kwa Taifa letu. Mbali ya kwamba Serikali imewekeza mali pale, ina hisa lakini bado Songas hawakufuata makubaliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe unajua Serikali ilikuwa ina hisa asilimia 40. Kupitia taasisi zake; *TPDC* ina hisa 28, *TANESCO* ina hisa asilimia 9, ukizijumlisha Serikali ina hisa kuliko Songas lakini hawana *say*.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* illiachia mali pamoja na madeni, mali zisizohamishiki zina thamani ya dola 1,000,000. Vilevile tulitoa sehemu ya *Ubungo Complex*, tukatoa sehemu ya ardhi ya bomba la gesi na tukakubaliana Songas ilipe dola za Kimarekani milioni 45,000,000. Mbaya zaidi mpaka sasa hivi tangu 2018 mbali na maagizo ya Bunge na *CAG* kupendekeza, *TANESCO*inalipa kupitia ankara za kila mwezi. Kwa nini tunashindwa kusimamia mkataba na bado tunakubali kunyonywa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaeleza kwa upande wa Pangea, tulikubaliana Pangea na *TANESCO* wafungue akaunti ya pamoja, kuna hela ilikuwa inakatwa dola 3,500 mpaka 5,000 kwa ajili ya kutengeneza miundombinu lakini zile pesa zilikubaliana ziende *TANESCO* miaka kumi akaunti ya pamoja haijafunguliwa. Hivi tunavyozungumza *TANESCO* walikuwa wanakarabati Buzwagi kwa pesa zao na *ten billion* hawajapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika nitashika shilingi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ngoja upate maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kukumbushia tena suala hili. Nifanye masahihisho kidogo tu, kwanza siyo *TANESCO* kuachana na Songas au *TPDC*, Songas ni jina la pamoja. Kuna *Globeleq*, *TANESCO*, *TPDC* ndiyo wanaunda Songas. Nimeona kidogo nimpe taarifa hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili nimeeleza awali kwamba Serikali yetu ilianza kufanya mapitio ya mikataba yote ya kuzalisha na kuuziana gesi. Tumemaliza katika kuzalisha gesi sasa hivi ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inafanya mapitio ya mikataba hii hii ikiwemo na Songas. Tuwape muda, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikishakamilisha itatoa maelekezo na hatua ambayo tutakuwa tumefikia lakini anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, tunataka mikataba yote iwe na manufaa kwa Watanzania, itakapoonekana hivyo, tutachukua hatua hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Pangea na *TANESCO* ni la mahesabu zaidi na wamekuwa wakifanyiana mahesabu kutegemea na miundombinu. Miundombinu inagemea na *valuation* ilipokuja na hali ya sasa hivi. Tuko katika hatua za mwisho sana kwa *TANESCO* na Pangea kulimaliza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuyafanya kazi ili yakamilike na tutampa taarifa. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaingia katika *guillotine*.

## **FUNGU 58 – WIZARA YA NISHATI**

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resource Management</i> .....	Sh. 3,066,285,000
Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 865,900,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh.1,261,316,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.476,302,000
Kifungu 1005 – <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh.496,608,000
Kifungu 1006 – <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh.481,783,000
Kifungu 1007 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh.480,495,000
Kifungu 1008 – <i>Environment Management Unit</i> .....	Sh.317,674,000
Kifungu 1009 – <i>Management Information System Unit</i> .....	Sh.526,572,000
Kifungu 3001 – <i>Electricity and Renewable Energy</i> .....	Sh.1,971,329,000
Kifungu 3002 – <i>Petroleum and Gas</i> .....	Sh.17,280,417,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

## **FUNGU 58 – WIZARA YA NISHATI**

Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh.2,968,128,000
Kifungu 3001 – <i>Electricity and Renewable Energy</i> .....	Sh.2,336,884,338,000
Kifungu 3002 – <i>Petroleum and Gas</i> .....	Sh.18,903,662,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri, Taarifa.

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Sasa kama ilivyo ada, Kanuni zinatutaka tulifanyie uamuzi jambo hili la hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwamba sasa Bunge mkubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote kabisa wameafiki, kwa kauli moja bajeti ya Wizara ya Nishati imepita. (*Makofi*)

*(Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa kweli, tunawapongeza sana kama Bunge, mnaona hata *approval/rate* ya Wabunge ni kubwa sana kwa sababu wanakubaliana kabisa na juhudzi za Serikali zinazoendelea kuhusiana na sekta hii. Tukianza kwa

kumpongeza Rais mwenyewe, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa hili jambo la bomba la mafuta kutoka Uganda na kwa ujumla usimamizi wa Wizara hii, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri mwenyewe, Naibu, Katibu Mkuu na wataalam wenu wote kabisa, tunawapongeza sana. Ni sekta ngumu na ina mambo mengi, ninyi wenyewe mmejadili, mmeona jinsi ambavyo inabidi wageukie kwenye petroli, gesi, umeme yaani ni sekta yenyenye mambo mengi mapana. Hata baadhi yenu mkawa mnayopendekeza kwamba bora hata ziwe Wizara mbili, Wizara ya Petroli na Wizara ya Nishati nyengine hizi lakini ni kwa sababu ya ukubwa huo. (*Makofii*)

Tunawapa pongezi sana, muendelee kufanya kazi hiyo. Tunawaomba Wizara ya Fedha kama walivyopendekeza baadhi ya Wabunge katika upande wa Wizara ya Nishati hebu fedha zao za maendeleo zitoke kama tulivyozipanga hapa itakuwa ni jambo la maana sana. (*Makofii*)

Tunawataki kila la kheri katika eneo la kutafuta mafuta, kwa sababu wenzetu Waganda wamepata mafuta, wenzetu wa Kenya wamepata mafuta na sisi ni nchi kubwa kuliko wote wawili wakijumlishwa. Sasa kwa mwendo huo, kwa nini sisi tusiwe na mafuta? Yatakuwa tu mahali fulani huku Bara na hata kule Visiwani mafuta yapo mahali. Basi tuongeze juhudii katika kusaka naamini Mwenyezi Mungu siku moja atatufungulia njia. (*Makofii*)

Tumefariji sana na majibu yako kuhusu vituo vya mafuta vijijini kama ambavyo tumelalamika siku zote. Ila sasa hawa *EWURA* na wale rafiki zangu wa *NEMC*, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira atakumbuka hata wakati ule nilisema sana kuhusu jambo hili, hawa wasipobadilika hilo haliwezekani, itabaki *wishful thinking* basi yaani ule udhibiti ni ukiritimba. Kama ni mabadiliko ya sheria zile mlete *miscellaneous* hapa maana kitu kidogo mpaka kwa Waziri, hivi ni baadhi ya vikwazo kidogo. Maombi madogo *EWURA* mpaka Bodii ikutane, mpaka itangaze sijui siku ngapi kwenye

Gazeti la Serikali, sijui nani anapinga, nani hapingi, kijijini anapinga nani bwana wewe? (*Kicheko/Makofi*)

Zile taratibu zimejaa ukiritimba ambao hauna sababu mpaka jirani akaulizwe na yeze unataka, hutaki kituo kianzishwe hapa. Sasa mwenye vivu anasema hapana. Kwa hiyo, wabadi like tu, hasa hawa wawili; *EWURA* na *NEMC* hili eneo la mambo ya vijijini linaweza likaenda *faster* na vizuri na Serikali itapata hela nydingi zaidi kwa sababu hii ya kuuza kwenye chupa Serikali haipati chochote, itapata fedha nydingi zaidi kwa ajili ya maendeleo. (*Makofi*)

Wabunge kupata elimu kuhusu hili bomba na mradi wenyewe tunaliomba sana. Ikiwezekana kabla hawajaondoka hapa ikafanyika *seminar* fulani tukapata mwanga. Kusema ukweli, Wabunge wengi wanaskia hili neno lakini hawalielewi vizuri undani wake na nini kipo. (*Makofi*)

La umeme kukatikakatika hili sasa ndiyo kubwa zaidi, likashughulikiwe. Maana kampuni ya *TANESCO* ni maarufu sana mnajua? Yaani sijui kama kuna Mtanzania haijui *TANESCO*, wachache sana labda vijijini sana lakini walio wengi wanajua *TANESCO*, hata watoto wadogo wanajua.

Kuna dada mmoja alienda likizo huko Kongwa kijijini ambako hakuna umeme kabisa na watoto wake wadogo. Sasa imefika usiku ule kwa bibi pale giza maana hata umeme haujafika hapo, kale katoto kadogo kabisa kanamwambia mama *TANESCO* wabaya. Mama yake anamuuliza *TANESCO* wabaya kwa nini? Wamemkatia umeme hata bibi. Wakati nyumba yenewe hata umeme haina lakini hata watoto wameshakariri kwamba mahali ambapo pana giza ni *TANESCO* wamekata umeme. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, *TANESCO* wanatakiwa kuji-rebrand hivi wawe ni kampuni ambayo itapendwa na watu. Kwa sasa hivi kama ni *rating* wako chini sana. Huenda siyo kwa makosa yao lakini nao waongeze tu juhudhi. Kama alivyosema nadhani Mheshimiwa Jumanne Sagini yaani umeme ukikatika huko kwenye mitandao ya kijamii ya kwenye majimbo utasikia tu,

wamekata tena na majina mengi ya ajabu ambayo *TANESCO* wanaitwa. Mbona hali mwanzo haikuwa hivyo, maana yake ni kwamba tunaweza tukarekebisha tu jambo hili likakaa vizuri pia. Kama linahitaji Wizara ya Fedha kufanya kitu, hebu waangalieni kipekee, nasema endapo linahitaji hivyo. Waangalieni kipekee kwa sababu ina athari kubwa sana katika uchumi wa nchi hata makusanyo na mambo mengi yana *slow down* umeme ukiwa *unreliable*. (*Makofi*)

Kwa kweli, sina la kusema zaidi ya kuwashukuru mno. Tunataraja sasa Waziri wa Maliasili anajienda na Naibu wake ili kesho na keshokutwa nao waje kinishati nishati hivi. (*Makofi/Makofii*)

Basi sasa mnikubalie tuahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.50 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 4 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*